Nipashe
Ijumaa Novemba 1, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580064
www.ippmedia.com
The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710



# Kijana aliyefungwa minyororo miezi 2 afunguliwa na kuogeshwa

UKURASA 3




UKURASA 13

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MO DEWJI ASIMULIA MAPYA ALIVYOTEKWA, WALIOMTEKA**

MFANYABIASHARA mashuhuri nchini, Mohamed Dewji maarufu kama MO, amefichua namna alivyoteswa na watu walimteka kwa muda wa siku tisa mwaka jana...

UKURASA WA 26

**UPEPO WAEZUA NYUMBA MIKOA RUVUMA, KATAVI**

UPEPO mkali ulioambatana na mvua ya wastani umeezua nyumba sita na vibanda vya biashara sita katika Kijiji cha Mgombasi, Kata ya Mgombasi...

UKURASA WA 26

**DODOMA WATANGAZIWA NEEMA MAELFU VIWANJA**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, ametangaza neema ya viwanja zaidi ya 9,000 kwa ajili ya uwekezaji pamoja...

# BABA JELA KUBAKA BINTIYE

UKURASA 3

# Madai ya rushwa yatua Takukuru

**Viongozi** kata watuhumiwa kupokea mlungula kupitisha wagombea, raia wa kigeni 55 wanaswa wakijiandikisha... Endelea ukurasa wa 2

Distributed via ippmedia



Mkuu wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Mara, Albert Rwelamira, akionyesha vitambulisho vya mpigakura kwa wanahabari Mjini Musoma jana, baada ya kuvikamata kwa watu 55, wanaodaiwa kuwa wahamiaji haramu. PICHA NDOGO: Baadhi ya vitambulisho hivyo. **PICHA: ADA OUKO**




Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play · App Store


# 'Mnada wa wabunge' wafungwa kwa uchafu

UKURASA 2

**MICHEZO** SABABU MWADUI KUITOBOA SIMBA UK. 32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mkurugenzi ashtukia ufisadi ujenzi stendi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, amenusa harufu ya ufisadi katika mradi wa ujenzi wa stendi kubwa katika eneo la Olasiti.

Kutokana na hali hiyo, amegoma kulipa fidia ya Sh. bilioni 1.9 kwa wananchi wa Kata ya Olasiti na kuwaonya baadhi ya viongozi wa Vijana wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) na baadhi ya watumishi wa halmashauri wanaotumika kumhujumu katika utendaji wake ili wale fedha za serikali.

Dk. Madeni aliyasema hayo jana katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani, baada ya kutakiwa kutoa ufafanuzi juu ya madai kuwa baadhi ya wananchi wa kata hiyo wanatumiwa vibaya na mafisadi hao na kuandamana wakishinikiza kulipwa fidia.

Alisema kwa taarifa alizonazo, eneo hilo la ekari 29.5 limenunuliwa na watu wawili ambao wanashinikiza wananchi waandamane ili walipwe fidia hiyo.

"Kweli siko tayari kulipa watu wanaofanya ufisadi. Wajue sasa blanketi walilokuwa wanajifunika limetoboka na hivi ni vita kati ya mafisadi na waaminifu maana kuna watu wanakula fedha halali kwa njia ya kifisadi,"alisema.

Alisema wanachokifanya wananunua ekari moja kwa Sh. milioni 10 Halafu wanauzia halmashauri Sh. milioni 80 au 100 bei ambayo haipo popote nchini na kwamba kamwe hataikubali.

"Kama sasa hivi tunajenga hospitali ya wilaya kwa Sh. milioni 800 kwa kutumia fedha za ndani, eti niache nipeleke kulipa mafisadi? Sikubali na katika hili niko tayari hata nifukuzwe kazi kama wanavyotaka na kunichafua kwa kusimamia fedha za Rais (John Magufuli). Niko tayari kwa kuwa nasimamia haki," alisema.

"Katika sakata hili utaona wazi ufisadi ulivyo maana katika muhtasari wa Februari 24, 2017 unasema walipwe fidia ya Sh. bilioni 1.1 lakini mwaka huo huo ukaandikwa muktasari Machi 6, 2017 kwenda Tamisemi wakiomba kibali cha kuchukua mkopo benki ya NMB wa Sh. bilioni 1.9. Hii uliona wapi duniani kama si ufisadi?"alihoji.

Alisisitiza stendi itajengwa eneo la Bondeni City ambako wamepata ekari 30 bure na kuokoa fedha hizo ambazo zitatumika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo.

Mkurugenzi huyo alielezea kushangazwa na mafisadi hao kutumia wananchi wanyonge na kuwaachisha mama ntilie kupika siku hiyo kwa kuwashikisha

INAENDELEA UK. 8

# Malalamiko rushwa mikononi Takukuru

**Na Waandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), mkoani Dodoma, imepokea malalamiko nane ya vitendo vya rushwa katika mchakato unaoendelea wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Aidha, watu wanaodaiwa kuwa ni wahamiaji haramu 55 wametiwa mbaroni na Idara ya Uhamiaji mkoani Mara, wakati wa kujiandikisha kwenye daftari la orodha ya wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa taasisi hiyo mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema malalamiko hayo yamepokelewa kutoka kata mbalimbali za mkoa huo.

Alisema wakazi wa maeneo hayo walilalamika baadhi ya wagombea kutoa fedha wakishinikiza majina yao yapitishwe kwa ajili ya kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Hata hivyo, Kibwengo alisema pamoja na kupata taarifa hizo, Takukuru inaendelea na uchunguzi wa malalamiko hayo ili hatua za kisheria zichukuliwe.

"Mpaka sasa nimepokea malalamiko nane yenye viashiria vya rushwa, nasi tunayafanyia kazi kujiridhisha kama malalamiko hayo yana ukweli sheria itachukua nafasi yake," alisema Kibwengo.

Aliwashukuru wananchi wa maeneo mbalimbali kupata uelewa wa kupiga vita rushwa katika uchaguzi huo.

"Kuna taarifa nyingine kutoka vijiji vya ndani kabisa, lakini Takukuru ikifuatilia inabaini kweli malalamiko hayo yana mashiko, ndio maana tupo mstari wa mbele kushirikiana na wananchi," alisema bila kueleza malalamiko yanahusu vyama gani vya siasa.

Aliwataka wananchi kuwa makini na kutopokea rushwa ndogo kutoka kwa wagombea ili wawachague.

"Wananchi msikubali kurubuniwa na watu waliojitokeza kuwania uongozi, kwa sababu watashindwa kufanya maendeleo katika mitaa yenu," alisema Kibwengo.

Kadhalika, Kibwengo aliwataka viongozi katika halmashauri kutoa taarifa za vitisho wanazopata kutoka kwa watu wanaojiita makamanda wa Takukuru kutokana na kuibuka wimbi la matapeli wa aina hiyo.

Alisema kuna matapeli wanajifanya maofisa wa Takukuru wamekuwa wakipiga simu za vitisho kwa viongozi wa halmashauri, ikiwamo

INAENDELEA UK. 8



Mkazi wa Kata ya Oldshinyanga, Manispaa ya Shinyanga, aliyefungiwa ndani huku akiwa amefungwa minyororo na ndugu zake kwa miezi miwili, Shadrac Johanes (26), akiwa amefunguliwa na kutolewa nje jana, huku akianza kupatiwa matibabu ya ugonjwa wa afya ya akili na wauguzi, baada ya kuogeshwa na kuvalishwa nguo safi. Kushoto ni wauguzi kutoka Kituo cha Afya cha Kambarage na Oldshinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 'Mnada wa wabunge' wafungwa kwa uchafu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MACHINJIO ya Msalato jijini Dodoma yamefungwa na kutozwa faini ya Sh. milioni tano na Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kutokana na kuendesha shughuli za uchinjaji kwenye eneo chafu.

Eneo la machinjio hayo maarufu kama 'Mnadani' limekuwa likihudumia wateja wengi hususan wabunge kwa ajili ya kula nyama choma na vinywaji siku za Jumamosi.

Halmashauri ya Jiji la Dodoma ndiyo mmiliki wa machinjio hayo maarufu kwa walaji wa nyama jijini na yamekuwa yakitumika kwa kiasi kikubwa kwa mnada wa kila Jumamosi.

Kufungwa kwa machinjio hiyo kumetokana na agizo la Naibu Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Mussa Sima, wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira iliyokuwa ikikagua machinjio hayo na Kiwanda cha Kusindika Nyama cha TMC.

Naibu waziri huyo alisema machinjio hayo yalipokaguliwa, yalibainika ni machafu na yana hali mbaya, hivyo kuhatarisha afya za walaji.

"Kila eneo tunalofanyia ukaguzi liwe sakafu, iwe mfumo wa majitaka, majisafi maeneo yote ni ya ovyo kwa manufaa ya afya za binadamu, serikali haiwezi kuruhusu shughuli za machinjio kuendelea, namwagiza Mkurugenzi Mkuu wa NEMC (Dk. Samwel Gwamaka), kuchukua hatua," Sima aliagiza.

Kutokana na agizo hilo, Dk. Gwamaka alitangaza kuyafunga machinjio na kuitaka halmashauri kulipa faini ya Sh. milioni tano na haitaruhusiwa kufanya kazi hadi hapo watakapojiridhisha kuwa wamefanya marekebisho katika majengo na mifumo ya majisafi na taka kwenye eneo hilo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Bunge, Kanali mstaafu Masoud Ali Khamis, alisema hali ni mbaya katika machinjio hayo na kuitaka NEMC iongeze umakini katika ufuatiliaji wa machinjio.

"Leo (jana) tumekuja hapa ghafla ndiyo hali ipo kama hivi, pengine katika maeneo mengine hali ni mbaya zaidi, ni hatari katika afya za watu wetu. NEMC tumieni sheria zilizotungwa na Bunge kuhakikisha kuwa machinjio yanakuwa katika hali ya usafi kwa faida ya afya za walaji," alishauri.

Alipoulizwa kuhusu kufungwa kwa machinjio hayo na uendeshaji wa mnada wa Jumamosi, Ofisa wa Mifugo wa Jiji la Dodoma, Gration Mwesiga, alisema ng'ombe na mbuzi hawatachinjwa tena katika mnada huo na utaratibu utakaotumika ni wafanyabiashara kwenda kuchukua nyama kwenye Kiwanda cha TMC na kusafirisha kwa magari kwenda mnadani wakati ukarabati ukiendelea.

## HABARI KITAIFA



Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andegenye, akizungumza na maofisa na askari wa jeshi hilo, mkoani Mwanza jana, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani humo, yenye lengo la kuhakikisha vikosi hivyo vinafanya kazi kwa uweledi na kuepukana na rushwa ikiwa na kutunza vifaa vya ukoaji ndani ya jamii. **PICHA: ROSE JACOB**

# Aliyefungwa minyororo miezi miwili afunguliwa

Distributed via ippmedia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHADRACK Johanes (26), mkazi wa Old Shinyanga katika Manispaa ya Shinyanga, aliyekuwa amefungwa minyororo chumbani kwa miezi miwili, amefunguliwa na kufanyiwa usafi, kuvishwa nguo na kuanza kupatiwa matibabu ya afya ya akili.

Kijana huyo alifunguliwa minyororo hiyo jana mara baada ya Nipashe kuripoti habari kuhusu ukatili uliokuwa unafanywa dhidi ya na ndugu zake.

Kijana huyo kwa miezi miwili alikuwa amefungwa minyororo mikono na miguu akiwa mtupu huku akila chakula kwenye chumba ambacho alikuwa anajisaidia haja kubwa na ndogo.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Shinyanga, Panuela Samwel, alisema kijana huyo amefunguliwa minyororo hiyo na serikali itatoa matibabu kwake bila malipo.

Alisema wameambiwa na wataalamu wa afya kuwa matibabu ya kijana huyo yanatarajiwa kuchukua muda wa miezi sita hadi mwaka mzima.

Ofisa huyo wa serikali alisema kama kijana huyo hatapona, watampatia rufani kwenda jijini Dodoma kupatiwa matibabu kwenye Hospitali ya Mirembe jijini Dodoma.

"Tukio alilofanyiwa kijana huyu ni la kinyama sana, nashukuru vyombo vya habari kwa kuliibua, bila ninyi huenda kijana huyu angefia ndani.

"Sisi sasa kama serikali, tutamtibu kijana huyu bure kabisa, na leo (jana) anaanza kupatiwa dawa ambayo itachukua muda wa miezi sita hadi mwaka mzima."

Akiwa kwenye familia ya kijana huyo jana, ofisa huyo aliitaka isimnyanyapae tena, badala yake imweke kwenye mazingira mazuri pasi na kumfunga minyororo.

Mratibu wa Magonjwa ya Afya ya Akili, Brigita Nyangare, alisema kijana huyo hana tatizo kubwa sana la akili kwa kuwa bado ana uwezo wa kuongea na hajapoteza kumbukumbu. Alisema atakuwa karibu na kijana huyo muda wote wa matibabu yake na atakuwa anafuatilia anavyoishi nyumbani hadi pale atakapojiridhisha amepona. Akizungumza kwa shida, Johanes aliwaomba ndugu zake wasimfungie ndani tena.

Ndugu wa kijana huyo waliomba msamaha kutokana na kumfungia na kuahidi kufuata maagizo waliyopewa na serikali.

# Afungwa maisha kwa kumpa ujauzito bintiye

**Na Gurian Adolf,** MPANDA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, imemuhukumu Lazaro Charles (35) mkazi wa Mtaa wa Mjimwema Manispaa ya Mpanda kutumikia kifungo cha maisha baada ya kupatikana na hatia ya kumpa ujauzito mtoto wake mwenye umri wa miaka 14.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Gasper Luoga, baada ya mahakama kuridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ambao ulikuwa ukiongozwa na wanasheria wa serikali, Gregory Muhangwa, ulikuwa na mashahidi watano huku upande wa utetezi uliwakilishwa na shahidi mmoja ambaye ni mke wa mtuhumiwa. Muhangwa aliiambia mahakama kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo kwa nyakati tofauti Januari Mosi, 2017 hadi Aprili 29, mwaka huu.

Alidai kuwa mshtakiwa alikuwa akitenda kosa hilo nyumbani kwake wakati mke wake, ambaye ni mama mzazi wa mtoto huyo, alipokuwa amesafiri ndipo alipokuwa akiingia kwenye chumba alichokuwa akilala mtoto huyo na kumbaka kwa nguvu.

Mwendesha mashtaka huyo alieleza mahakama kuwa mtuhumiwa baada ya kuwa anambaka, alikuwa akimwekea majani kwenye sehemu zake za siri mtoto huyo kama dawa ya kienyeji kwa ajili ya kumwondolea maumivu sehemu za siri.

Muhangwa alidai kuwa hali ya mtoto huyo ilianza kubadilika kitendo kilichosababisha walimu wake waamue kumpeleka hospitalini na kufanyiwa vipimo vilivyoonyesha kuwa mwanafunzi huyo alikuwa mjamzito na alipoulizwa alimtaja baba yake mzazi, Lazaro Charles kuwa ndiye mhusika.

Hakimu Luoga alisema mahakama imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka pasipo kuacha shaka kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo.

Kutokana na ushahidi huo, alisema mahakama imemtia hatiani kwa kifungu cha sheria namba 158 (1)(a) sura ya 16 ya Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Kabla ya hukumu, Luoga alimtaka mshtakiwa kama atakuwa na sababu ya msingi ambayo inaweza kuifanya mahakama kushawishika kumpunguzia adhabu aitoe, hivyo akaiomba mahakama apatiwe nakala ya hukumu ya mwenendo wa kesi hiyo tu kwani hana utetezi wowote zaidi ya hapo. Baada ya ombi hilo, Muhangwa aliiomba mahakama itoe adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwa wazazi wengine wenye tabia kama hiyo.

Hakimu Luoga baada ya kusikiliza pande hizo mbili, alisoma hukumu na kusema mtuhumiwa amepatikana na kosa kwa mujibu wa sheria, hivyo anahukumiwa kutumikia kifungo cha maisha jela kuanzia jana.


## SHUKRANI

Familia ya RICHARD SEMGALAWE MRISHO wa NHC Michungwani Muheza Tanga wanapenda kutoa shukrani za dhati kwa watu wote walioshirikiana nao katika mazishi ya mpendwa wao **Mwl. LUIZA HERIETH MRISHO** tarehe 31/08/2019 na kwenye misa ya kumbukumbu tarehe 11 na 12 Octoba, 2019 katika Kanisa la Mt. Raphael Mdote Muheza Tanga. Shukrani za pekee wanazitoa kwa Padre NGODA wa St. Raphael Mdote, Padre LINZA wa Lusanga kwa Yesu, Dr. MSETI wa Ocean Road Hospitali, Dr. KIBOKO na Dr. KIANGI wa hospitali ya Mzena Dar es salaam. Wapendwa ni vigumu kumshukuru mtu mmoja mmoja lakini kwa tangazo hili tunaomba kila mmoja anayelisoma basi amwambie na mwenzake kwamba familia ya MRISHO wanashukuru sana kwa kushirikiana nao katika msiba huu.



Mwl. LUIZA HERIETH MRISHO

Mwenyezi Mungu ailaze Roho yake MAHALA PEMA PEPONI.

"Bwana ametoa nae ametwaa Jina la Bwana lihimidiwe AMINA.



## SUNDI (T) LIMITED

### TANGAZO KA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliopewa na Akiba Commercial Bank PLC tunauza kwa mnada wa hadahara nyumba nane(8) za wadaiwa sugu

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | SHARIFI ULADI NAMTAYA | SHARIFA LADI NAMTAYA | NYUMBA,CHATEN=MBO MKURANGA | 9/11/2019 4:00ASUBUHI |
| 002 | MACK MOHAMED MADIGADI | MACKY MOHAMED MADIGADI | NYUMBA, KIJIJI CHA KAZOLE-MKURANGA | 9/11/2019 8:00 ASUBUHI |
| 003 | FREDRICK BALTAZAR PETER | FREDRICK BALTAZAR PETER RE | NYUMBA, ULONGONI B ILALA | 12/11/2019 4:00 ASUBUHI |
| 004 | DEOGRATIUS WILSONCHAULA | OCTAVIAN SEVERIN NYAMBI | NYUMBA MAKANGANYA KINONDONI | 14/11/2019 4:00 ASUBUHI |
| 005 | HUGOLINE LEONARD KARIA | HUGOLINE LEONARD KARIA | NYUMBA, MBAGALA KUU MGENI NANI | 16/11/2019 4:00 ASUBUHI |
| 006 | JOYCS MICHAEL SAMSON | MOHAMED JUMA FERUZI | NYUMBA, CHARAMBE NZASA A. TEMEKE | 20/11/2019 4: ASUBUHI |
| 007 | MUSSA NG'OMBE NKOBA | ZUHURA ISSA FERUZI | NYUMBA MWONGORO MAKUBURI-UBUNGO | 23/11/2019 4:00 ASUBUHI |
| 008 | ASIA TIMOTHY KITUMBIKA | ASIA T. KITUMBIKA | NYUMB, MEONGORO MAKUBURI-UBUNGO | 23/11/2019 4.00 ASUBUHI |

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 20% siku hiyo yam nada ya bei iliyofikiwa
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishidwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona,kukagua,kuhamisha umiliki, na zingine zitamuhusu mnunuzi.

KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NASI KUPITIA ANUANI
MUKURUGENZI MTENDAJI
SUNDI (T) LIMITED
P.O BOX 40057
0715549782 AU 0713893706

115493402

# Bandari Mtwara kupokea meli ya mafuta tani 40,000

**Na Mary Geofrey,** MTWARA

BANDARI ya Mtwara inatarajia kupokea meli yenye shehena ya mafuta takribani tani 40,000 kwa ajili ya kuhudumia mikoa ya ukanda wa kusini na nchi jirani.

Meli hiyo inatarajiwa kutia nanga katika Bandari ya Mtwara, mapema mwezi Novemba kwa lengo la kuongeza bidhaa hiyo nchini ili kusambaza katika mikoa ya kusini na kukuza uchumi.

Meneja wa Bandari ya Mtwara, Juma Kijavara, akizungumza na waandishi wa habari walipotembelea bandari hiyo mapema wiki hii, alisema kuja kwa shehena hiyo kutaisaidia kushuka kwa gharama ya mafuta kwa wakazi wa mikoa ya kusini.

"Ujio wa meli hii pia utasaidia sasa mafuta yapatikane kwa wingi katika ukanda huu wa kusini, lakini pia kusaidia kuuzwa kwa bei nafuu, ina maana kama ni mengi na gharama nazo zitakuwa chini kwa sababu tunapokea wenyewe mzigo kutoka bandarini tofauti na miaka ya nyuma tulipokelea bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa kwa magari kuja Mtwara," anasema Kijavara.

Vile vile, alisema mwaka 2017/18 walipokea tani 15,000 za mafuta yaliyopita katika bandari hiyo.

"Kila mwezi tunahudumia meli moja ya mafuta ambayo siyo chini ya tani 4,000," alisema Kijavara.

Kadhalika, alisema katika kuboresha biashara hiyo ukanda wa kusini, bandari hiyo ipo katika mchakato wa kuanza kuhudumia shehena ya mafuta aina ya petroli na dizeli itakayosafirishwa kwenda katika nchi za Malawi, Msumbiji na Zambia.

Alisema baada ya kufanya vizuri katika kuhudumia mafuta kwa ajili ya mikoa ya kusini, wanasubiri kukamilika kwa utaratibu wa kupata vibali vya kuhudumia shehena ya mafuta nje ya nchi.

"Tunafatilia kibali kutoka mamlaka husika ya kuanza kusafirisha mafuta ya diseli na petroli katika nchi za ukanda wa kusini mwa Tanzania na kuhudumia mafuta kwa miundombinu iliyopo," alisema Kijavara.

Naye Kwa Ofisa Ununuzi na Ugavi wa Bandari hiyo, Abdilah Salim, alisema mbali na biashara ya mafuta wanayotegemea katika bandari hiyo, tayari mamlaka hiyo imeipa punguzo la bei ya usafirishaji kampuni ya kuzalisha Saruji ya Dangote kwa ajili ya kusafirisha shehena kupitia Bandari ya Mtwara na katika makubaliano hayo kampuni hiyo itakuwa inasafirisha tani 120,000 kwa mwezi.

Alisema, pia wameipa kampuni ya Market Insight kwa ajili ya kusafirisha makaa ya mawe kutoka mkoa wa Ruvuma kupitia bandari hiyo kwenda katika masoko ya nje.

"Lengo ni kuwa na watumiaji na wafanyabiashara wengi wanaotumia bandari yetu. Tunatarajia kusafirisha tani 70,000 kwa mwezi za shehena ya makaa ya mawe usafirishaji huo utakapoanza," alisema

Distributed via ippmedia



Muuza matunda akipita jirani na chemba ya maji machafu ya Ofisi ya Rufaa za Kodi, iliyoziba na kutiririsha maji taka jirani na ofisi ya Bodi ya Filamu Tanzania, Barabara ya Samora, jijini Dar es Salaam jana, kusababisha kero ya harufu mbaya wiki tatu sasa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mo Dewji afichua mapya ya kutekwa

**Na Joseph Mwendapole**

MFANYABIASHARA mashuhuri nchini, Mohamed Dewji maarufu kama 'MO', amefichua namna alivyoteswa na watu waliomteka kwa muda wa siku tisa mwaka jana.

Akizungumza na kipindi cha BBC Dira ya Dunia, MO alisema alidhani maisha yake yamefika mwisho kutokana na namna watekaji hao walivyokuwa wakimtishia.

Dewj alisema aliona gari nyuma yake ambalo liliegeshwa pembeni yake mara alipofika kwenye hoteli ambayo hufanya mazoezi kila siku asubuhi. Alisema watu hao walimvamia na kuanza kupiga risasi juu huku wengine wakimtishia na kumlazimisha alale chini jambo ambalo alisema aliamua kutii ili kuokoa maisha yake. "Walinibeba wakaniweka kwenye gari lao wakaanza safari ambayo kwa kweli ilikuwa ngumu sana kwa sababu walinivua nguo wakidhani kuwa nina kifaa maalum ambacho kinaweza kusababisha watu wakajua nilipo," alisema MO.

Alisema walimfunga kamba kwenye mikono yake na kumvalisha kitambaa usoni ili asione wanakoelekea huku wakimtaka asizungumze kitu chochote wakati huo.

"Walikuwa wanazungumza lugha nisiyoijua, mimi nimeishi mikoa mingi hapa Tanzania, hivyo limegundua kuwa lugha waliyokuwa wakiizungumza siyo ya Tanzania... waliniweka ndani ya chumba chenye godoro na wakanifungua miguu ili niweze kutembea," alisema.

Alisema watekaji hao walikuwa wakimlazimisha kula, ingawa muda mwingi alikuwa akikataa kula chochote kutokana na muda mwingi kulia akihofia maisha yake na kufikiria kuhusu familia yake.

"Usiku ilikuwa ndiyo mtihani mkubwa kwangu kwa sababu walikuwa wakinifunga mikono nyuma, hivyo nashindwa kabisa kulala. Kama umefungwa mikono nyuma huwezi kulala kawaida lazima uteseke," alisema. Alipoulizwa iwapo waliomteka ni washindani wake wa kisiasa, MO alisema ingawa kuna ushindani katika siasa, lakini bado Tanzania haijafikia hatua ya watu kufanyiana mikasa ya aina hiyo. Alisema watu hao walimpeleka hadi Gymkana na kumtupa nje ya gari na ndipo alielekea hoteli ya Southern Sun na kukuta walinzi ambao walimpigia simu baba yake.

MO Dewji alitekwa Oktoba 11, 2018 na watu wasiojulikana alfajiri alipokuwa akielekea mazoezini alipofika katika hoteli moja ya kifahari katika eneo la Oysterbay jijini Dar es Salaam kama ilivyo ada yake kila siku alfajiri kwa ajili ya kufanya mazoezi ya viungo.


**KUPOTEA KWA VYETI**



**SHANGWE MPULE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0863/0011kilichotolewa na MWADUI TECH SEKONDARI mwaka 2001. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba P605/056 kilichotolewa na UHURU SEKONDARI mwaka 2009.Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**DAR/URA/RB/428131/2019 na DAR/URA/RB/428135/2019.**

1154942O2

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**SONGEA LILILOKO SONGEA**
**MAOMBI NAMBA 71/2019**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF MUTAMAL TAALIM AL-ISLAM................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. THE BOARD OF THE REGISTERED TRUSTEES OF MUTAMAL TAALIM AL-ISLAM
2. CASPAL SAVIO MBILINYI
3. CHARLES URICK KOMBA
4. ABDULKARIM ATHI SAIDI............WAJIBU MAOMBI

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

Wajibu maombi wa pili na watatu hapo juu mnaarifiwa kuwa mwombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu. Hivyo basi mnatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wenu, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 27/11/2019 saa 2:30 asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zenu za utetezi. Zingatia pia kushindwa kwenu kufika na kuleta hati ya utetezi kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili bila kujali uwepo wenu.

Imetolewa nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 30/10/2019.

115493302

**MARUDIO YA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, CHAMPION AUCTION MART** tutauza kwa mnada wa hadhara Kiwanja/Eneo la mdaiwa sugu, Ndugu ZAINABU HUSSEIN NJOVU kilichopo/lililopo Mtaa wa Mgeninani, Kata ya Kijichi. Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo anaodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 06/11/2019, mahali dhamana ilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi. **CHAMPION AUCTION MART: 0688056805/0742983700 Tujijenge: 0718068335/ 0717956315.**

**SHULE INAUZWA/ INAKODISHWA**

Shule awali ya Victoria Daycare Centre (Usajili namba 738) inauzwa/inakodishwa ina wanafunzi takribani 35 ipo kwenye mazingira mazuri. Inapatikana Ukonga – Moshi Bar. Bei maelewano.

Mawasiliano: 0715 904259 / 0758512235.

115493502

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**YAHAYA OMARY MASSARE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SCANIA yenye namba za usajili T 573 BHL.Chassis No.3643936. Engine No.8125640.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/428373/2019.**

115494102

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**YAHAYA OMARY MASSARE.** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya ZHONGTONG yenye namba za usajili T 950 CGU.Chassis No. LDY4GS2C290003226. Engine No.87650872.Y

eyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/428369/2019.**

115494102

TANGAZO




Distributed via ippmedia

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Iwapo tulimaliza plastiki, ukatili hautatushinda

**TAARIFA** za ukatili kwa binadamu zilizoripotiwa jana na gazeti letu zinaonyesha jinsi ambavyo vitendo vya udhalimu huko Shinyanga vilivyosababisha mwana familia kufungwa minyororo mikononi na miguuni kwa zaidi ya miezi miwili.

Aidha, Nipashe inavitaja vitendo vingine vya ukatili kwa watoto vinavyohusisha ubakaji na ulawiti, ambavyo vimewaumiza mamia ya watoto mkoani Kilimanjaro.

Tukiangalia zaidi ukatili dhidi ya watoto, inaelezwa kuwa tangu kuanza mwaka huu takribani watoto 127 wamefikishwa katika Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi kutibiwa kutokana na ukatili dhidi yao, unaohusisha ubakaji na ulawiti.

Wataalamu kutoka Mawenzi wanasema kesi (visa) za ubakaji zilizofikishwa hospitalini hapo ni 90 wakati za ulawiti ni 37. Hayo ni matukio kutoka mkoa wa Kilimanjaro na kwenye hospitali moja pengine idadi ni kubwa zaidi kutoka hospitali mbalimbali na kwenye vituo vya polisi vingine nchini kote.

Tunaona kuwa hili si jambo la kupuuzwa hata kidogo. Ni kama kuliangamiza taifa na kusababisha mlolongo wa matatizo kwa watoto wetu.

Ikumbukwe kuwa unyanyasaji na mateso dhidi ya watoto wetu ni chanzo kikuu cha umaskini kwenye jamii zetu pia ni kikwazo cha kufikia maendeleo endelevu ambayo taifa linayatazamia na kuwa na mikakati ya kuyafikia inayoandaliwa kila wakati.

Ukatili huu unawatia watoto wetu ulemavu. Aidha, unawatumbukiza kwenye kitanzi cha umaskini kwa kuwa mabinti hawa wanaobakwa na kulawitiwa ni wazi kuwa watashindwa kusoma na matokeo yake wanazidi kuwa mbumbumbu na maskini.

Tukumbuke kuwa kuwanyanyasa watoto kingono kunawaingiza kwenye kukosa haki za msingi kama kukua na kuwa na viungo na akili timamu. Kunawanyima pia haki ya kuwa na afya njema na kuwasababishia msongo wa mawazo unaotokana na uharibifu wa maumbile yao na zaidi huwaongezea umaskini katika maisha yao. Tunaona kuwa watoto kutoka kaya maskini na zile zenye walezi au wazazi maskini au wenye ulemavu ndiyo wanaokuwa na hali mbaya zaidi.

Kutokana na ugumu wa maisha wanashindwa pengine hata kutoa taarifa polisi au kufika hospitalini. Hawa ndiyo ambao kutokana na kukosa ulinzi na umaskini nyumbani kwao wanazidi kunyanyaswa na kudhulumiwa kingono. Kutokana na uovu huo wanazidi kuwa maskini na kwa vyoyote vile wanaendelea kuishi katika umaskini mkubwa.

Kwa upande wa wasichana ukatili huu unasababisha washindwe kusoma shuleni na pengine hupata maradhi yakiwamo ya kujamiiana mfano kaswende, pangusa, maambukizi ya mkojo na hata VVU na Ukimwi.

Yote haya kwa vile hawawezi kupata matibabu husababisha waendelee kuugua na kushindwa kwenda shuleni. Kwa wengine unyanyasaji huo ni chanzo cha kufeli mitihani yao, kukimbia shule, utoro na kurudi tena kwenye uteja wa adui ujinga.

Kwa watoto wote bila kujali kuwa ni wakike au wa kiume athari hizo ni wazi kuwa kubakwa au kulawitiwa kutasababisha washindwe kusoma, wataishi kwenye umaskini kwa vile hawatakuwa na fursa za kupata kazi bora wala mafunzo ya kuendeleza maisha yao.

Ndiyo maana tunaona kuwa ni lazima kuwa na mikakati ya kuwalinda watoto wetu. Tunahitaji kuwa na utaratibu ndani ya vijiji, mitaa, vitongoji na kila mahali kuwasaidia watoto wasinyanyaswe kingono.

Tunahofu kuwa tusipofanya hivyo tutaendelea kubakia na umaskini na ujinga na maradhi maadui ambao tangu uhuru walitelisa na wanaendelea kuliumiza taifa letu.

Kama taifa tunahitaji kuandaa mikakati ya ulinzi endelevu wa watoto kwani Tanzania isiposimamia na kumaliza janga hili, haitakuwa tofauti na msemo kuwa ukicheza na nyani utavuna mabua. Ni sawa na kusema tusipolinda watoto taifa hili litaangamia. Hebu tuchukue hatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Mwanzo msimu korosho, RC Pwani atutia moyo

Distributed via ippmedia

**KOROSHO** ni zao linalouongezea mapato mkoa wa Pwani. Ili serikali na wakulima wanufaike nako, kuna kila haja ya hatua kuchukuliwa, kuhakikisha serikali na wakulima wananufaika.

Pamoja na kuonekana mkombozi kwa wakulima na serikali, kuna baadhi ya watu wamekuwa wakilalamikiwa kwamba si waaminifu katika kufanikisha matakwa ya zao hilo na hususan mchakato wa mauzo.

Hiyo ni kwamba, wanakuwa si waaminifu hata kusababisha serikali kujipanga kwa kulisimamia zao hilo, ili iweze kumkomboa mkulima ajiongezee kipato.

Kuna historia ndefu ya kuzalisha zao hilo. Moja ya maeneo ni kuwapo baadhi ya watu kutokuwa waaminifu na kuwafanyia wakulima hujuma nyingi.

Haikuwa jambo jema hata kidogo, katika baadhi ya maeneo kuna wakulima waliopatwa na madhila hata wakaamua kuacha kulima, wakahamia mazao mengine.

Kwetu Pwani, sasa ni mwezi huu wa kuuza korosho. Mtazamo bayana utumike kuliletea taifa mapato, ikiwamo kuwanufaisha wakulima kupitia zao hilo.

Wakulima wamekuwa wakilima korosho na wanapouza wanatarajia kunufaika na zao hilo, mbali ya wakulima kunufaika, pia serikali inatarajia panapouzwa korosho wananufaika kutokana na fedha zinazopatikana kupitia zao hilo.

Hivyo basi, serikali imekuwa ikiwawezesha wakulima pembejeo ili waweze kunufaika na kilimo hicho.

Katika mkoa wa Pwani, hivi karibuni Mkuu wa Mkoa, Evarist Ndikilo, ameziagiza kamati zote za ulinzi na usalama za wilaya kuwachukulia hatua watu wote watakaogundulika kufanya ubadhirifu kwa wakulima wa korosho.

Anazitaka kamati hizo kumpa taarifa za utekelezaji huo ndani ya siku saba.

> **Wakulima wamekuwa wakilima korosho na wanapouza wanatarajia kunufaika na zao hilo, mbali ya wakulima kunufaika, pia serikali inatarajia panapouzwa korosho wananufaika kutokana na fedha zinazopatikana kupitia zao hilo**

Ni kauli yake, alipofungua mkutano wa wadau wa korosho Mkoa wa Pwani, uliofanyika wilayani Mkuranga. Jambo zuri sana kwetu wakulima.

Ndikilo anazitaka taasisi zote za fedha zilizoshiriki katika kufanya malipo kwa wakulima wa korosho, kutoa ushirikiano wa kutosha kwa vyombo vya ulinzi na usalama za wilaya, ili kubaini kasoro zinazochangia wakulima kutopata fedha zao

Aidha, anaipongeza serikali kufanya malipo kwa wakulima wa korosho kiasi cha Sh. bilioni 47.7 na imebaki Sh. bilioni 18.1, ambazo wakulima hawajalipwa.

Mhandisi Ndikilo, amewahakikishia wakulima wa korosho wa Pwani, kwamba korosho zilizokusanywa na serikali zimeshauzwa na anawataka wawe na subira, wakati serikali inamalizia uhakiki, ili kila mkulima apate fedha zake.

Ni jambo linalochukua sura hiyo mkoani, huku Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, anasisitiza kwamba hatovifumbia macho vyama vya msingi au viongozi wa vyama watakaoshiriki kufanya ubadhirifu na kurudisha fedha

"Tunataka wakulima wanufaike na zao hilo, yeyote atakayefanya ubadhirifu atachukuliwa hatua kali za kisheria," anasema.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Francis Alfred, anasema wao wanaahidi kutoa mafunzo kila kijiji cha mkoa wa Pwani katika zao la korosho, ili kulifanya zao hilo mkoani Pwani linakuwa na ubora kama ilivyo mikoa mingine.

Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Pwani (CORECU), chenyewe kimetakiwa kuandaa magunia mapema kwa ajili ya kujiandaa na msimu unaoanza na wakulima wakitakiwa kutochanganya korosho na michanga au taka zingine.

**TANGAZO**

BancABC part of atlasmara

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,521 | 3,705 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,015 | 7,367 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 33,025 | 32,774 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,548 | 4,452 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (48) | 190 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 91,839 | 94,037 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 130,381 | 132,226 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 33,902 | 34,172 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 4,109 | 4,391 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **315,291** | **314,314** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 91,364 | 97,633 |
| 18 | Amana za Wateja | 97,865 | 89,299 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 25 | 50 |
| 27 | Dhima Nyingine | 5,869 | 6,303 |
| 28 | Madeni | 68,364 | 67,881 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **263,487** | **261,165** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **51,804** | **53,149** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 116,014 | 116,014 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | 1,284 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (61,839) | (63,123) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,433) - | 2,091 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,062 | 1,065 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **51,804** | **53,149** |
| | | - | (0) |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 7,711 | 8,130 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 21,077 | 22,303 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 16,060 | 19,807 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16.4% | 16.9% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 14.4% | 14.8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 77.4% | 81.3% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 41.4% | 42.1% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 82.7% | 83.8% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1.2% | -3.5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.3% | -0.8% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-19 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Sep-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,859 | 11,825 | 32,045 | 39,116 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,699) | (5,074) | (14,152) | (17,214) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **6,160** | **6,751** | **17,894** | **21,902** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa/ Yaliorejeshwa | 566 | - | 1,663 | (8,327) |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (700) | (1,434) | (2,154) | 596 |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,380** | **1,707** | **3,997** | **4,221** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 434 | 718 | 1,432 | 1,439 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 814 | 300 | 2,191 | 799 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 132 | 689 | 374 | 1,983 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(8,704)** | **(8,232)** | **(24,695)** | **(23,495)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,750) | (2,454) | (8,077) | (7,567) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (5,953) | (5,778) | (16,618) | (15,928) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,297)** | **(1,208)** | **(3,297)** | **(5,103)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (45) | - | (136) | (48) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,342)** | **(1,208)** | **(3,433)** | **(5,151)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,342)** | **(1,208)** | **(3,433)** | **(5,151)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 156 | 156 | 156 | 156 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.55) | (0.49) | (0.35) | (0.52) |
| 15 | | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 7 | 7 | 7 | 7 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.71% | -1.42% | -1.45% | -3.02% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -10.23% | -8.45% | -8.72% | -18.02% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 115.43% | 97.33% | 112.81% | 89.94% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.64% | 2.95% | 3.53% | 4.79% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-19 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,297) | (790) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 1,588 | 1,560 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,054 | 1,463 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,297 | (6,807) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (250) | 1,801 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (459) | 2,522 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 507 | (923) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (45) | - |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **3,395** | **(1,173)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (35) | (163) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(35)** | **(163)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | 2,738 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **2,738** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 3,361 | 1,401 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 109,562 | 108,161 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **112,923** | **109,562** |

Distributed via ippmedia

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 116,014 | - | (67,756) | - | 1,284 | 1,065 | 50,607 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (3,433) | - | - | - | (3,433) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,284 | - | (1,284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | 4,633 | - | - | (3) | 4,630 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 116,014 | - | (65,272) | - | 0 | 1,062 | 51,804 |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 116,014 | - | (69,349) | 9,118.58 | 1,114 | 1,384 | 58,282 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (7,355) | - | - | - | (7,355) |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 9,118 | (9,118) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (170) | - | 170 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (320) | (320) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 116,014 | - | (67,756) | 0 | 1,284 | 1,065 | 50,607 |

Katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka huu, BancABC iliadhibiwa TZS milioni 145 na Benki Kuu ya Tanzania kufuatia uvunjaji wa sharia ya AML / CFT.

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 25-Oct-19 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 25-Oct-19 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 25-Oct-19 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkurugenzi | Dr J P. Kipokola | | 25-Oct-19 |
| 2 | Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 25-Oct-19 |

# Malalamiko rushwa mikononi Takukuru

INATOKA UK. 2

wakurugenzi wakidai wawapatie fedha.

Alisema hakuna kamanda wa Takukuru anayedai fedha ili asitoe taarifa, isipokuwa taarifa yoyote kuhusiana na vitendo vya rushwa inapokelewa bure kutoka kwa mhusika.

"Wananchi msikubali kudanganywa katika simu hakuna kamanda wa Takukuru anayempigia simu mtu ili watoe pesa hao ni matapeli, toeni taarifa hatua kali zichukuliwe," alisema Kibwengo.

### 55 watiwa mbaroni

Wakati huo huo, watu 55 wanaodaiwa kuwa wahamiaji haramu wamekamatwa na Idara ya Uhamiaji mkoani Mara, wakati wa kujiandikisha kwenye daftari la orodha ya wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Imeelezwa kuwa watu hao walikamatwa wakati wa mchakato wa kujiandikisha uliomalizika Oktoba 17, mwaka huu.

Ofisa Mkuu wa Idara hiyo, Albert Rwelamira, alisema katika ukaguzi huo watu hao walikutwa na vitambulisho vya mpigakura vilivyotumika kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Aidha, alisema walifanikiwa kukamata kwa ushirikiano na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), viongozi wa serikali za mitaa, vijiji, vitongoji na waandikishaji wapigakura kwenye daftari hilo.

Alisema kujiandikisha kupiga kura ni kinyume cha sheria kwa kuwa hawatakiwi kushiriki shughuli yoyote ya siasa hadi watakaposajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki na kutambulika kama wakazi wenye vibali vya kuishi nchini.

"Tumewakuta wana vitambulisho vya kupiga kura vya mwaka 2015, ikiwa na maana labda mwanzo walijiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura na wengine tumewakuta na vyeti vya kuzaliwa wakati hawakuzaliwa hapa, tunaendelea na uchunguzi wetu," alisema.

Rwelamira alisema katika uchunguzi wao uliofanikisha kukamatwa kwa watu hao, walibaini kuwapo kwa udhaifu mkubwa kwa baadhi ya viongozi na watendaji wa serikali za mitaa wakiwamo wenyeviti kwa kuwaandikisha barua ya utambulisho wageni ambao si raia wa Tanzania wanaofika kwenye makazi yao na kudanganya uraia wao.

"Tumejiandaa kama mkoa kudhibiti wahamiaji haramu sambamba na kutoa elimu kwa viongozi hawa kuwa jukumu lao ni kuwatambulisha wakazi wa maeneo yao, kinyume cha hilo siyo jukumu lao kueleza uraia. Suala la uraia mpaka waletwe kwetu tufanye upelelezi na mahojiano ya kina na hatimaye tuweze kujiridhisha kwamba mtu ni raia," alisisitiza.

Naye msimamizi wa uandikishaji wapigakura wa uchaguzi wa serikali za mitaa, John Masero, alisema kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa ya mwaka 2019, mpigakura ni lazima awe makazi wa mtaa na hakuna pingamizi lolote alilofikishiwa juu ya watu hao.

Alisema baada ya kumaliza uandikishaji walitakiwa kubandika orodha ya watu walioandikwa ili wananchi wa mtaa husika wawatambue na kama kuna tatizo lolote watoe pingamizi, jambo ambalo lilitekelezwa na hakukuwa na pingamizi lolote.

"Katika kanuni ya 12 ya uchaguzi wa mwaka 2019 pingamizi kuhusu uandikishwaji ni kwamba mkazi ambaye amejiandikisha kwenye orodha ya wapigakura anaweza kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa na kuwa mpigakura kabla ya kumalizika kwa muda wa kukagua orodha ya wapiga kura ambayo ilikuwa ni siku saba," alisema Masero. Uandikishaji wa wapigakura ulianza Oktoba 8 hadi 17, mwaka huu, na uchukuaji wa fomu ulianza Oktoba 28 na utamalizika Novemba 4.

Takribani watu milioni 19 wamejiandikisha kupiga kura katika uchaguzi huo kati ya watu milioni 22.9 waliokadiriwa.

**Imeandikwa na Renatha Msungu, Dodoma na Ada Ouko, Musoma**

## Mkurugenzi ashtukia ufisadi ujenzi stendi

INATOKA UK. 2

mabango ya kuandamana kushinikiza kulipwa fidia wakati si wakazi wa eneo hilo na matokeo yake waliwatumikisha katika mbinu zao chafu kwa kuwapa ujira wa Sh.10,000. "Mimi sitishiki na mafisadi ambao naamini bado wapo kwenye chama na halmashauri na nitaendelea kupinga ufisadi wa kiharamia unaofanyika katika Jiji hili na baadhi ya watu,"alisema.

Naye Naibu Meya, Paul Matthysen, alisema baraza hilo halitishwi na linaheshimu maazimio yake kuwa stendi kubwa ijengwe Bondeni City na hawatabadili msimamo wao kwa maandamano.

Alisema wao halmashauri waliingia ubia na Bondeni City mwaka 2015 na kupata eneo la ekari 30 ambalo gharama kubwa kama hizo hakuna.

Aidha alimpongeza mkurugenzi Dk.Madeni kufanikisha kupatikana kwa eneo hilo na kuwaonya mafisadi wanaomchafua Mkurugenzi huyo kwa maslahi yao kuacha mara moja kwani hawatafanikiwa na wao hawarudi nyuma. Diwani wa Kata ya Ngarenaro Isaya Doita alisema hakuna haja ya kujadili suala hilo ambalo walishapitisha maazimio yao sababu kuendelea kulizungumza sawa na kuotesha mbegu juu ya jiwe.

Kabla ya kikao hicho Oktoba 30 mwaka huu wananchi wa Mtaa wa Oloresho Kata ya Olasiti zaidi ya 80 waliandamana wakiwa na mabango, wakipinga mradi wa ujenzi wa stendi kubwa kuhamishiwa eneo la Bondeni City, huku wakiliacha eneo lao la ekari 29.5 lililotengwa mwaka 2012 katika Kata ya Olasiti, ambalo lilipitishwa kujengwa stendi hiyo na kuamriwa kulipwa fidia kwa wananchi wa eneo hilo.

Distributed via ippmedia




# CRDB kuwekeza miradi mikubwa

**Na Salome Kitomari**

BENKI ya CRDB imesema itaendelea kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa miradi mikubwa ili kufikia uchumi wa viwanda.

Aidha, benki hiyo imepata faida ya Sh. bilioni 92 ndani ya muhula wa tatu kutoka Sh. bilioni 52, baada ya kodi ikiwa ni ongezeko la asilimia 76. Pato hilo limetokana na riba lililokuwa kwa asilimia 22, na nje ya riba kutokana na huduma za kawaida asilimia 13, na kwamba kwa ujumla riba za mikopo zimepungua kufikia asilimia 14.

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema mafanikio hayo wamefanya vizuri kwa muhula wa kwanza, wa pili na tatu jambo linaloonyesha kuwa iko imara.

Alisema miradi ambayo hadi sasa benki hiyo imeingia ni mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere na reli ya kisasa, na kwamba wanaangalia kasi sekta zote za msingi ili kuendana na kasi ya serikali ya maendeleo ya viwanda.

Aidha, alisema benki hiyo imejikita kwa kiasi kikubwa kwa wajasiriamali wa chini na kati, kuhakikisha kila mmoja anapata huduma aliko ikiwamo kuongeza mikopo inayotolewa.

Nsekela alisema wanatoa mikopo na kuisimamia kwa weledi kwa kuhakikisha inarejeshwa kwa wakati na kuongeza wigo wa mikopo, na kwamba mikopo chechefu imepungua hadi asilimia 7.5 na lengo ni kufikia chini ya asilimia 5, huku wakijihadhari na mikopo hatarishi.

"Tumeweka kinga ya mikopo kwamba likitokea tatizo tusiyumbe, tumetenga pato la kutosha kutoka asilimia 60 hadi 75.1, maana yake mikopo tuliyonayo tunaihimili na benki kuendelea kuwa imara," alifafanua.

Alisema wamepunguza kupunguza gharama kwa mlaji kwa kupeleka huduma kidigitali, na kwa sasa asilimia 70 ya huduma za kibenki zinafanyika nje ya asilimia 30 ndani ya benki, na kuondokana na kutoa huduma kwa historia bali kwa kulingana na mahitaji ya mteja.

# Kiboko aua mchimba madini

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

MKAZI wa Kijiji cha Namasakata, Tunduru mkoani Ruvuma, Ismail Juma (59), amefariki dunia baada ya kushambuliwa na kiboko wakati akijaribu kujiokoa kushambuliwa na kundi la tembo.

Juma alikumbwa na mkasa huo Jumanne wiki hii majira ya 12:30 asubuhi akiwa njiani kuelekea katika machimbo ya vito eneo la Msimbo, Kijiji cha Misechela.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema Juma alikutana na kundi la tembo ambao walianza kumfukuza hali ambayo ilimfanya kukimbilia katika maji ya Mto Ruvuma ambako alikutana na kiboko huyo.

Walisema baada ya tukio hilo, Juma ambaye alikuwa amejeruhiwa kwa kung'atwa na meno ya kiboko na kuvunja mifupa ya paja na mkono wa kushoto, alifariki dunia wakati akiwa njiani akipelekwa hospitalini kwa matibabu. Kaimu Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Limbega Ally, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba tayari amekwisha peleka askari wa idara hiyo kwa ajili ya kumsaka kiboko huyo.

Alisema maeneo ya Misimbo ndiyo makazi ya viboko, hivyo wananchi wanaokwenda katika maeneo hayo wanatakiwa kufanya shughuli zao kwa tahadhari.

HABARI KITAIFA

# AfDB kuipa Tanzania tril. 1.5/- ujenzi uwanja ndege Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imepongeza uamuzi wa Rais John Magufuli wa kuhamia Dodoma na kuahidi kuidhinisha dola za kimarekani milioni 455 (sawa na zaidi ya shilingi trilioni 1.5) kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato sambamba na ujenzi wa barabara za mzunguko jijini humo.

Rais wa AfDB, Dk. Akinwumi Adesina, ameyasema hayo katika Ofisi za Makao Makuu ya Benki hiyo Abijdan, Ivory Coast wakati wa mazungumzo yake na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi na kuongeza kuwa benki hiyo itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Rais Magufuli katika kipindi chake cha Uenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) lakini na kwa Tanzania.

Alisema benki hiyo imeshaidhinisha dola za Marekani milioni 180 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mzunguko jijini Dodoma na kwamba kiasi kingine cha dola milioni 275 kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato kinatarajiwa kuidhinishwa mwezi huu.

Dk. Adesina aliongeza kuwa AfDB ina imani na mageuzi ya kiuchumi yanayotekelezwa chini ya uongozi wa Rais Magufuli ukiwamo utoaji wa huduma za kijamii kama elimu bila malipo, afya na maji pamoja na mapambano dhidi ya rushwa na kuleta uwajibikaji katika taasisi za umma, na kwamba iko tayari kuunga mkono jitihada hizo kwa kuwekeza katika sekta ya miundombinu.

Aidha, Dk. Adesina alielezea nia yake ya kutaka kushuhudia Bara la Afrika likipiga hatua kubwa za kimaendeleo sasa na kwa haraka na sio kusubiri baadaye na kwamba katika kipindi chake cha uongozi katika AfDB atapambana kuhakikisha azma hiyo inatekelezeka.

Naye Prof. Kabudi aliishukuru AfDB kwa ushirikiano inayoutoa kwa Tanzania hususan katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa, ambayo kimsingi yalikuwa ni maono ya Baba wa Taifa,

Hayati Mwalimu Julius Nyerere kwa nia ya kuiwezesha Tanzania kujitegemea kiuchumi na hatimyae bara zima la Afrika.

Prof. Kabudi aliongeza kuwa AfDB iko tayari kufadhili ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha kutoka Isaka hadi Kigali nchini Rwanda na kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) baada ya kukamilika mchakato wa utoaji wa fedha hizo, ambapo mazungumzo ya awali kuhusu ufadhili huo yameanza.



Vijana wakiwa wamebeba viroba vya mchanga waliouchota kwenye Mto Msimbazi eneo la Kigogo, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kwenda kuuza ili wajipatie riziki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kisarawe wahakikishiwa maji

**Na Frank Monyo**

NAIBU Waziri wa Maji, Juma Aweso, amewahakikishia wakazi wa Wilaya ya Kisarawe kuwa ndani ya siku tatu watasahau kero na shida ya maji walioipata kwa miaka mingi, baada ya kukamilika mradi wa ujenzi wa tangi la ujazo wa lita milioni sita.

Aweso pia ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa) kwa kutekeleza mradi huo uliotumia Sh. bilioni 10 kwa kutumia fedha zake za ndani.

Akizungumza na wanahabari baada ya kukagua mradi huo wilayani humo, Aweso alisema kukamilika kwake ni ishara tosha kuwa Dawasa inaweza kumaliza kero ya maji kwa kutekeleza miradi mikubwa bila kutegemea fedha za wahisani.

Alisema baada ya kukamilika anawakaribisha wawekezaji katika wilaya hiyo kwani sasa maji yapo ya kutosha kufanya shughuli mbalimbali.

Kaimu Mkurugenzi wa Miundombinu na Uwekezaji wa Dawasa, Mhandisi Ramadhan Mtindasi, alisema utekelezaji wa mradi huo umekamilika kwa asilimia 99.

"Mpaka sasa tumelaza bomba kuu linalotoa maji Kibamba, maji yanayotoka mtambo wetu wa Ruvu Juu kuja hapa, lakini pia tushalaza bomba kilometa 34 katika mji wa Kisarawe," alisema.

Aliongeza kilichosababisha mradi huo usianze kazi juzi ni kutokana na mafundi wa Tanesco kukabiliana na changamoto ya kukamilisha kwa wakati.

"Sisi tumepokea agizo la Naibu Waziri, ndani ya siku tatu tutahakikisha maji yamefika ndani ya Kisarawe... tunawasihi wananchi kwenda katika Ofisi za Dawasa kujaza fomu kwa ajili ya kuunganishwa maji kwa mkopo na watalipa ndani ya miezi 12," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, alisema kukamilika kwa mradi huo unakwenda kutatu kero ya muda mrefu kwa wananchi wa Wilaya ya Kisarawe na kuinyanyua wilaya hiyo kiuchumi.

## Agizo warajisi ushirika kuwabana wabadhirifu

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Titus Kamani, amewaagiza warajis wa vyama vya ushirika nchini, kushirikiana na vyombo vya dola kuwakamata waliohusika na ubadhirifu wa mali za wana ushirika.

Aidha, ametoa siku 14 kwa warajis wasaidizi wa mikoa, kuzichambua taarifa za vyama na kuanza kuchukua hatua.

Dk. Kamani alitoa agizo hilo hivi karibuni, baada ya kikao kazi cha makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kilichofanyika jijini Dodoma.

Katika kikao hicho pamoja na mambo mengine tume ilipokea ripoti ya jumla ya ukaguzi wa vyama vya ushirika uliofanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (Coasco) kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

"Nataka kupata taarifa ya kila hatua, na mimi nitafuatilia ana kwa ana. Hatuwezi kuendelea kuwalea watu wasiotaka kuwajibika kwa dhamana waliyopewa na wanachama na hakuna jiwe ambalo halitapinduliwa kuhakikisha mali na fedha za wanachama zinalindwa," alisema.

Aidha, aliwataka wasimamizi wa vyama vya ushirika wakiwamo warajis wasaidizi wa mikoa kuchukua hatua stahiki kutokana na madhaifu yaliyobainishwa katika ripoti ya jumla ya ukaguzi wa vyama vya ushirika uliofanywa na Coasco.

"Kwa kuwa ripoti ya Coasco huwasilishwa katika mikoa husika, nawaagiza warajis wasaidizi wa mikoa kuchukua hatua stahiki kama ilivyoshauriwa na wakaguzi, kama kuna viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika wamehusika katika kuhujumu mali za wanaushirika; shirikianeni na vyombo vya dola katika maeneo yenu ili kunusuru mali za wanaushirika," alisisitiza Dk. Kamani.

Aidha, alisema ni lazima ajulishwe kila hatua kwa kuwa ushirika hauwezi kuendelea kutafunwa na wajanja wachache.

Kuhusu uhamasishaji na uanzishwaji wa vyama vya ushirika nchini, alisema kwa miezi mitatu yaani Julai hadi Septemba, mwaka huu, Tume hiyo imesajili jumla ya vyama vya ushirika vya msingi 79 na chama cha mradi wa pamoja kimoja.

Alisema idadi ya vyama vya ushirika imeongezeka na kufikia 11,410. Vyama vipya vilivyoanzishwa vina jumla ya wanachama 5,630.

## Vikundi miradi vyaomba mikopo

**Na Sabato Kasika**

ZAIDI ya vikundi 10 vya miradi ya kiuchumi vikiwamo Vicoba vinavyonunua hisa na kukopeshana vya Musoma mkoani Mara, vimeomba mkopo wa fedha, katika Taasisi Jamii Impact Ltd ya Kanisa la Menonite Tanzania (KMT).

Kanisa hilo lilifungua ofisi za kutolea mkopo eneo la Nyabange KMT Mission, mjini Musoma, Septemba mwaka huu na kukaribisha vikundi mbalimbali vya ujasiriamali kuomba mkopo wa fedha.

Ofisa Mikopo wa taasisi hiyo, William Mdemu, alisema, hadi sasa imeshapokea maombi ya vikundi zaidi ya 10, inaendelea kuyajadili ili kama vimekidhi masharti, vipewe mkopo.

Mdemu alisema baadhi ya vikundi, ambavyo vimeomba mkopo katika taasisi hiyo, vinatoka katika kata za Nyambono, Suguti, Kiriba, Ifulifu na Nyakatende, zilizopo Musoma Vijijini.

Alisema, miongoni mwa vikundi hivyo vinajishughulisha na kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara na vimeomba mkopo wa fedha kwa ajili ya kufanikisha shughuli za kiuchumi.

Hata hivyo, alisema kuna masharti ambayo kila kikundi kinatakiwa kuyatimiza ili kiwe na sifa ya kukopesheka ikiwa ni kufika ofisini za taasisi kikiwa na taarifa ya miaka mitatu, kununua hisa na kukopeshana.

"Lazima kikundi kiwe kilichosajiliwa na kutambulika kisheria, kiwe na akaunti benki, ni lazima kikundi kiwe na wanachama wasipungue 30 na katika hao, asilimia 50 wanatakiwa kuwa wanawake na vijana," alisema Mdemu.

# Mama mtoto aliyefanyiwa ukatili atoa ushahidi kortini

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa wa Chakechake chini ya Hakimu Luciano Makoye Nyengo, imeendelea kusikiliza ushahidi wa shauri la udhalilishaji dhidi ya mtoto, linalomkabili mshtakiwa Juma Hamad Said (30), mkazi wa Chonga.

Mama mzazi wa mtoto aliyefanyiwa kitendo cha udhalilishaji na kijana huyo, alidai siku ya tukio Septemba 12, mwaka 2018, majira ya mchana alikuwa nyumbani kwake akipika, na kuwa baada ya muda mfupi, alitokea mtoto wake mwenye umri wa miaka 15, na kumwambia ameshiba hahitaji kula tena kwa muda ule.

Shahidi huyo alidai alimuuliza mtoto wake kuwa alipata wapi chakula na kumjibu kuwa alikula harusini akiwa na mtuhumiwa.

"Aliniuliza mama unamjua yule kaka Juma wa kina Ochu? Nikamwambia ndio namjua, akaniambia walipofika huko alinichukua na kumpeleka chooni halafu akamvua suruali," alidai mama huyo.

"Baada ya kupata maelezo hayo, nilimwangalia sehemu zake za siri za nyuma, kwa kweli sikuona chochote ndipo nikaamua kwenda Polisi na nikaenda hospitali kwa uchunguzi," alieleza.

Alidai baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kidaktari, daktari alitueleza hakufanywa kitendo, ingawa alimgusisha sehemu zake za siri kwenye sehemu zake za siri.

Shahidi nambari mbili, ambaye ni askari mpelelezi kutoka Polisi Chakechake, Fatma Mbarouk Ali, alidai Juni 16 mwaka 2019 akiwa ofisini kwake, alipata jalada kutoka kwa mkuu wake wa kazi na kumwelekeza kwenda kulifanyia upelelezi shauri hilo.

"Nilisoma jalada nikajua kosa na ndipo nilipomtafuta mshtakiwa na kwenda kwenye eneo la tukio kwa ajili ya uchunguzi," alidai.

Alidai kuwa alifika kwenye eneo la tukio Gobani Chonga, akiwa ameambatana na mtoto, mama mzazi pamoja na mshtakiwa na mzazi wake, ambapo walifika kwenye jengo kubwa ambalo bado halijamaliziwa kujengwa.

Mpelelezi huyo alidai kutokana na uzoefu alionao kwa muda wa miaka sita wa shughuli yake ya upelelezi, na maelezo aliyoyaeleza mtoto huyo, aliunganisha moja kwa moja kwamba mshtakiwa alimfanya kitendo hicho.

Wakili wa Serikali, Ramadhan Suleiman Ramadhan, alidai shauri hilo lipa kwa ajili ya kusikilizwa mashahidi na wamepokea mashahidi wawili, ambapo walianza kusikilizwa.

Baada ya mahakama kumaliza kusikiliza ushahidi huo, mtuhumiwa aliomba apatiwe dhamana, ombi ambalo lilikataliwa na mahakama kutokana na kutotimiza masharti aliyoelezwa.

"Dhamana iko wazi, timiza masharti yako upatiwe dhamana, unatakiwa kuwa na mdhamini mmoja atakayesaini bondi ya shilingi milioni mbili pamoja na wewe mwenyewe kusaini kiasi kama hicho," alisema hakimu.

Awali ilidaiwa mtuhumiwa alitenda kosa Septemba 12, mwaka jana akiwa na nia ya kukidhi matamanio ya kingono, alimgusisha sehemu zake za siri kwenye sehemu za siri za nyuma za mtoto huyo wa kiume.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 139 (1) (a) (2) (b) cha Sheria nambari 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Novemba 11, mwaka huu kwa ajili ya



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akikabidhi cheti cha shukrani kwa Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Benjamin Nkaka (kushoto), kwa kutambua mchango wa benki hiyo katika kufanikisha kongamano la wanawake lililopewa jina la 'Madirisha' lililoandaliwa na kampuni ya GS1 kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) na Taasisi ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (PASS), jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya GS1, Jumbe Menye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hukumu kesi wanaodaiwa kulisha mashamba ya wakulima wiki ijayo

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

USHAHIDI wa kesi ya kujeruhi iliyokuwa ikiwakabili wafugaji watatu wa jamii ya wafugaji wanaoshtakiwa kuingiza mifugo kwenye msitu wa hifadhi wa asili wa kijiji cha Kihondo Wilaya ya Mvomero umekamilika, na hukumu inatarajiwa kutolewa wiki ijayo.

Hukumu hiyo itatolewa na Mahakama ya Mwanzo Mvomero mkoani Morogoro Novemba 6, mwaka huu.

Kesi hiyo iliitwa mahakamani juzi na kuelezwa kuwa ushahidi wa pande zote umekamilika ikiwamo ushahidi wa mpelelezi wa kesi hiyo askari polisi mwenye namba G 4290 DC Adonis wa Kituo cha Polisi Doma.

Akitoa ushahidi mpelelezi huyo alidai Oktoba 8, mwaka huu majira ya jioni, alipokea taarifa ya kuwapo kwa vurugu kwenye kijiji cha Kihondo, hivyo waliongozana na askari mwenzake, DC- Juma hadi eneo la tukio na kukuta vurugu zimekwisha. Alidai waliamua kwenda eneo lililokuwa na watu wengi kijijini hapo na kubaini kuwapo kwa majeruhi wawili ambao walikimbizwa zahanati ya kijiji kwa matibabu na baadaye kuhamishiwa Kituo cha Afya cha Kororo kisha kupelekwa Hospitali ya Rufani mkoani Morogoro kutokana na hali zao kuwa mbaya.

DC Adonis alidai baada ya majeruhi kupelekwa hospitali, alirejea ofisi ya mtendaji wa kijiji na kabla hajafika alikutana na kundi la ng'ombe 179 ambao hawakuwa na mchungaji, ambao walifanana na 12 waliokamatwa awali, hivyo kuamua kuwaweka pamoja na kufikia 191. Aidha, alidai washtakiwa hao watatu walifika Polisi Oktoba 10 na kutoa maelezo baada ya kuitwa kwa njia ya simu kupitia kwa wazazi wao kutokana nakudaiwa kukimbia na Oktoba 11, kesi yao ilifikishwa mahakamani.

Mashahidi upande wa utetezi akiwamo mzazi wa mshtakiwa namba 1 na 3, Kishakwii Kailanga (45), alidai wachungaji wake wa ng'ombe wapo wawili ambao walikwenda kuchunga siku ya tukio, na kwamba alipowahoji kabla ya kwenda polisi wamefanya nini walipotoka kuchunga, wadai hawakufanya chochote.

Awali washtakiwa hao namba moja Sperwa Kishakwii (16) na mshtakiwa namba tatu Kashuma Kishakwii (18), walidai mahakamani kuwa siku ya tukio hawakwenda kuchunga ng'ombe badala yake walienda watoto wengine waliopo nyumbani kwao na kuwataja kwa majina moja moja kuwa ni Nuhu na Leba.

Mshtakiwa namba mbili, Daniel Babalai (18), alidai mahakamani kuwa siku ya tukio hakuwa na mchungaji, na kuwa walichunga watoto wengine na yeye aliitwa Polisi kukagua ng'ombe wake walipotea baada ya kukamatwa Polisi kisha kuwekwa rumande.

Awali ilidaiwa mahakamani kuwa washtakiwa hao waliwajeruhi kwa fimbo na marungu askari wa kamati ya ulinzi wa msitu wa asili wa Kihondo uliopo Kata ya Doma ambao ni Emmanuel Willnely aliyejeruhiwa kwa kuvunjwa mguu wa kulia na Exavery Pius aliyejeruhiwa kichwani na mkono wa kushoto.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Mussa Lilingani, alisema aliamua kuahirisha kesi hiyo ya kujeruhi namba 155/2019 yenye kifungu namba 228 hadi Novemba 6, mwaka huu kwa ajili ya hukumu, na kwamba dhamana ya washtakiwa inaendelea kuwa wazi.

# Watakiwa kudhibiti mimba za utotoni katika mashule

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WARATIBU elimu kata, walimu na wazazi wametakiwa kushirikiana kudhibiti mimba za utotoni kwa wanafunzi katika shule mbalimbali za mkoa wa Arusha.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini (Tarura) Mkoa wa Kilimanjaro, Charles Marwa, alisema hayo hivi karibuni wakati wa mahafali ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kiranyi iliyoko mjini hapa.

Marwa alikuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo ya 12 ambayo wanafunzi 320 walihitimu kidato cha nne.

Alisema suala la mimba za utotoni kwa wanafunzi linahitaji kudhibitiwa kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali kwa kuwa limekuwa tatizo kubwa katika shule mbalimbali, hivyo kukatisha malengo ya watoto wa kike.

Pia aliwataka wadau mbalimbali wa maendeleo kuhakikisha wanashirikiana kuwatafuta wale wote wanaowarubuni watoto wa kike na kuwakatisha masomo yao.

"Tutahakikisha tunawashughulikia wale wote wanaoturibia watoto wetu na naomba sana wazazi na walezi, mkiwagundua msisite kuwataja maana hao mko nao katika jamii yenu na mnawajua. Tukifanya hivyo tutawaokoa wasichana wetu katika janga hilo," alisema.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Sayuni Tarimo, alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika taaluma, lakini bado inakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo ya ukosefu mabweni ya wanafunzi.

Alivitaja kikwazo kingine kuwa ni mimba kwa wanafunzi wa kike na kwamba tangu Januari, mwaka huu, wanafunzi watano wameshindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya ujauzito.

Tarimo alisema wanakabiliwa pia na uchakavu wa miundombinu vikiwamo vioo vya madirisha, sakafu kuchakaa na uhitaji wa viti 92, vyumba vitatu vya maabara ambavyo havijakamilika, hivyo kusababisha wanafunzi kushindwa kufanya mafunzo kwa vitendo.

Kutokana na matatizo hayo, aliomba wadau mbalimbali kuwajengea vyumba vya madara kwa sababu vilivyopo sasa vinawafanya wanafunzi kusongamana na kukaa zaidi ya 60 darasa moja.

Mmoja wa wahitimu, Winnie Albert, akisoma risala klwa niaba ya wenzake, alisema wamekuwa wakikabiliwa na tatizo kubwa ya ukosefu wa viwanja vya michezo na vifaa kwa ujumla, hali ambayo ambayo inawasababishia kushindwa kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali.

Tatizo lingine, alisema ni wazazi kutolipia chakula kwa baadhi ya watoto hali inayochangia watoto kupata elimu duni.



Wananchi wa Kata ya Olasiti mkoani Arusha, wakiwa wamefunga barabara jana, kupinga maamuzi ya Baraza la Madiwani wa Halmashuri ya Jiji la Arusha, la kutaka kuhamishwa kwa ujenzi wa stendi kubwa katika eneo hilo, kwenda Bondeni City, huku fedha Sh. bilioni 10 zikiwa zimetolewa na serikali kwa ajili ya kulipa fidia wananchi na kuanza kwa ujenzi huo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Mrembo wa Dunia atembelea Anapa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MREMBO wa Dunia, Silvia Vanessa, juzi alitembelea Hifadhi ya Taifa ya Arusha (Anapa) na kujionea makundi ya wanyama wakiwamo twiga na nyumbu pamoja na aina za ndege walioko katika Ziwa Momela.

Akizungumza baada ya kutembelea hifadhi hiyo, alisema amefurahishwa na vivutio adhimu vilivyopo ambavyo ni vya asili.

Aliwataka watu kutoka nchi mbalimbali kutembelea hifadhi za Tanzania ambazo zinaongoza kwa vivutio vingi na mazingira ya asili.

"Hakika nitatangaza vivutio vya kipekee duniani ili watalii wengi waje hapa kwa kuwa watanufaika na vivutio vingi vya asili vilivyoko Tanzania," alisema.

Vanessa alisema amevutiwa na nchi ya Tanzania na kuahidi kurudi nchini kwa mara nyingine kutembelea vivutio mbalimbali vilivyoko maeneo mengine.

"Kila nitakakokwenda nitahamasisha watu kuja kuona vivutio vilivyopo Tanzania kwani ni vizuri na vya asili," alisema.

Mrembo wa Tanzania (Miss Tanzania) mwaka 2019, Silvia Sebastian, alisema ziara ya mrembo huyo wa dunia inalenga kutangaza Tanzania na kutangaza utalii kwa ujumla na kufanya shuguli za kijamii.

Ofisa Mhifadhi Utalii wa Anapa, Jerome Ndanzi, alisema wamefurahishwa na ujio wa Mrembo wa Dunia kwenye hifadhi hiyo kwa kuwa utasaidia kutangaza hifadhi hiyo kimataifa na kuvutia wageni wengi kufika kuitazama.

# Millya ataka kuziba mianya utoroshaji madini

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

MBUNGE wa Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, ameviomba vyombo vya usalama kuziba mianya yote ya utoroshaji madini Mererani ili wananchi wake wanufaike.

Alitoa ombi hilo juzi wakati wa kikao cha siku moja cha wadau wa madini na viongozi wa serikali, kilichofanyika ofisi ya Madini Mererani kwa lengo la kupeana mbinu za kufanya ili kuongeza mapato ya madini kwa pande zote.


Millya alisema kuna baadhi ya watu wanajinufaisha na madini hayo, hivyo ni vyema vyombo hivyo vikawabana hata kama ikibidi kubaki na wanunuzi wachache lakini waadilifu.

"Inauma sana kuona wananchi wanateseka halafu baadhi ya watu wananufaika na madini haya. Tena wale wanaonufaika wanakwepa hata kodi, hii haikubaliki," alisema. pia alionya baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) walioko wilayani hapa kuonea wananchi walioko Mirerani kwa kuwapelekea barua za uonevu kuwadai kodi.

"Katika hili sikubaliani nalo ni uonevu. Nalipeleka bungeni kwenda kulisemea. Lazima nchi hii tufike mahali tusioneane kila upande unufaike na tutendeane haki," alisema.

Alipongeza ujenzi wa ukuta huo kwa sababu umeongeza manufaa kwa wachimbaji wadogo, wakubwa na kati, japo wako watu wanaopinga kwa maslahi yao.

"Lakini ukuta huu umeongeza thamani kubwa kwa watu wetu kwani kila mmoja ananufaika. Achaneni na baadhi ya watu wanaopinga, hao wanania zao mbaya," alisema.



# Walimu wafundwa uwekezaji miradi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

SERIKALI imesema walimu 1,500 wa shule za msingi na sekondari wa wilaya ya Same, wana kila sababu ya kuhamishia akili na nguvu zao katika uwekezaji wa vitega uchumi binafsi, badala ya kutegemea mishahara peke yake ili kuendesha maisha.

Mkuu wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule, alitoa ushauri huo kwa walimu, baada Chama cha Akiba na Mikopo cha Same Teachers Saccos, kumpa taarifa kwamba kimetoa zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kuwakopesha walimu mitaji.

Senyamule alielezwa hayo jana, wakati wa maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa chama hicho.

"Huu ni mpango mzuri sana wa kuwasaidia walimu kukopa ili wafanye mambo ya kiuchumi ambayo yanahitaji kuwa na mtaji. Wako walimu wanaokaribia kustaafu, sasa ili usiharibu mipango yako, ukicheza na mikopo hii unaweza kukabiliana na hali ngumu ya maisha na ukafanya maandalizi ya kujiimarisha kiuchumi kabla ya kustaafu utumishi wa umma," alisema.

Mwasisi wa Saccos hiyo na Mwenyekiti wa Bodi, Omary Mchome, alimweleza Mkuu huyo wa Wilaya kwamba kwa miaka 20 wamewajengea wanachama wao nyumba, kununua magari na kuwapa mitaji ya biashara inayofikia zaidi ya Sh. bilioni 10.

Alisema Saccos hiyo ambayo haina deni na inajiendesha kwa faida, imekuwa suluhisho la mitaji kwa walimu kutokana na upatikanaji wa mikopo ya riba nafuu.

Kwa mujibu wa Mchome, chama hicho kimekuwa msaada mkubwa kwa wananchi wengi hususani wenye kipato cha chini, kwa kuwa riba za mikopo ambayo mara nyingi ni kwa ajili ya mitaji ya biashara, ununuzi wa pembejeo za kilimo, upatikanaji wa zana za uchimbaji wa madini na bidhaa mbalimbali ni nafuu kulinganisha na taasisi nyingine za kifedha.

Alisisitiza kuwa vyama hivi vya ushirika vinawapa wanachama nguvu ya pamoja katika masuala mbalimbali kwa kuwa huwaunganisha watu wenye jambo fulani linalowaweka pamoja.



Viongozi wa koo na wa kidini katika Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wakipanga mkakati wa kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto wa kike unaoendelea, walipokutana wilayani humo jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wizi mifugo, ujambazi vyamtikisa DC

**Na Godfrey Mushi,** HAI

Distributed via ippmedia

KUANZA kuchomoza kwa matukio ya wizi wa mifugo na ujambazi wa kutumia nguvu katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro kumeanza 'kumtikisa' Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya.

Kutokana na hali hiyo, Ole Sabaya anapanga mkakati wa kuwakabili wanaohatarisha amani na usalama wa wilaya hiyo, akitaka kwenda kila kata ili kubaini watuhumiwa wa wizi wa mifugo katika wilaya hiyo.

Akizungumza jana na Nipashe baada ya kuzima jaribio la ujambazi wa kutumia nguvu ambalo mlinzi wa kampuni moja ya ulinzi anadaiwa alikuwa akitengeneza mchoro wa uporaji wa Sh. milioni 70 za taasisi ya fedha ya Brac, mkuu huyo wa wilaya alisema hawezi kukubali hali hiyo kuendelea kuhatarisha kibarua chake na atashughulika na watu hao.

Alisema jaribio la kutaka kuporwa fedha hizo, limemshtua kwa kuwa liliratibiwa na mlinzi wa kampuni iliyopewa kazi ya ulinzi na kusafirisha fedha za taasisi hiyo ya Brac.

Ole Sabaya na timu yake ya maofisa wa Polisi, alizima jaribio hilo juzi baada ya kuweka mtego uliosababisha kukamatwa kwa mlinzi huyo, akiwa tayari anatoa mwongozo kwa waporaji kuhusu gari litakalotumika kubeba fedha na wapi wanakwenda.

Walifanikiwa kuzima jaribio hilo la ujambazi ambalo lingesababisha kuporwa kwa fedha za Taasisi ya Brac katika eneo la Kata ya Masama, wilayani hapa.

Akizungumza na madereva wa bajaj na bodaboda katika mji wa Bomang'ombe, Ole Sabaya alisema: "Hawa wezi wamekuja wameiba nguruwe pale karibu na nyumbani kwangu wameiba nguruwe wa jirani yangu na tumekwenda tumefuatilia mpaka Kijiji cha Narumu wanapopeleka nguruwe hao na tumempata na tumemrudisha.

"Nyie madereva bajaj na bodaboda mnatuhumiwa kusafirisha mifugo hiyo inayoibwa, halafu wakishafanya yao hao wezi, wanawavunjia heshima wanawapa majina mabaya, mnaonekana madereva wa bajaji na pikipiki wote waovu, wote wa ajabu, wote wahuni."

Kuhusu wizi wa mifugo, aliwaonya madereva wa pikipiki na bajaji wilayani humo kuacha kushiriki kwenye vitendo vya wizi ikiwamo wizi wa mifugo kwa kuwasafirisha wanyama hao pindi wanapoibiwa.

Badala yake, aliwataka kuacha kazi hiyo haramu na kufanya kazi ambazo zitawaingizia kipato na kuwafanya kuwa huru katika biashara yao ya kusafirisha abiria.

# Waitara aonya nyaraka za siri mitandao ya kijamii

**Na Mary Mosha,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, amesema watumishi wa umma wanaoendelea kutuma au kuchapisha nyaraka za siri za serikali na zile za wazi katika mitandao ya kijamii wanafanya jinai.

Akizungumza jana katika Manispaa ya Moshi na watumishi wa umma wanaounda Chama cha Kitaaluma cha Watunza Kumbukumbu na Nyaraka Tanzania (Trampa), Waitara alisema watumishi wa umma kufanya hivyo ndio wanaosababisha mkanganyiko wa taarifa au upotoshaji kwa jamii.

Alisema ni lazima wataalamu wa kutunza kumbukumbu na nyaraka, waache tabia ya kuvujisha baadhi ya taarifa kwa njia ya mtandao, lakini ifike mahali wawe na mipaka ya kiutendaji baina yao na wanasiasa wanaowatumia.

"Ni marufuku kwa watumishi wote nchini kutuma nyaraka za siri na za wazi kwa njia ya mitandao ya kijamii kwa sababu kufanya hivyo kunaweza kusababisha mkanganyiko wa taarifa au upotoshaji kwa jamii," alisema Waitara.

Kutokana na tatizo hilo kuathiri utendaji wa serikali, alisema Tamisemi imeagiza makatibu tawala wa mikoa watoe maelekezo kwa maandishi katika ofisini zote za wilaya na taasisi za umma juu ya onyo hilo.

Lakini, Waitara ameagiza makatibu tawala wa mikoa kuwahoji wakurugenzi wa halmashauri za wilaya ambao wamezuia ruhusa wa watunza kumbukumbu na nyaraka wasihudhurie mkutano huo muhimu ambao pamoja na mambo mengine, unalenga kubadilishana uzoefu na wenzao.

"Wapo wakurugenzi katika halmashauri nchini wamewanyima kwa makusudi baadhi ya watunza kumbukumbu ruhusa ya kufika kwenye mkutano huu wa wataalamu na wengine wameruhusiwa, lakini hawakupewa stahiki zao kama posho ya kujikimu na nauli. Sasa naagiza kila mkoa, RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) awahoji wakurugenzi na nipate majibu kwa maandishi," aliagiza Waitara.

Kabla ya Waitara kutoa maelekezo hayo, Rais wa Trampa, Josephine Manase, alielezea masikitiko yake akisema wako baadhi ya wanataaluma wanadharauliwa na wakurugenzi na wamenyimwa kwa makusudi kwenda katika mkutano huo.

"Wanataaluma ambao hawajafika hapa ni wengi sana kwani kila halmashauri kuna watunza kumbukumbu zaidi ya watano na kwa ujumla wao, wanaweza kufika zaidi ya 3,000 nchi nzima, lakini hadi sasa wapo zaidi ya 600 tu," alisema Manase.

Devota Mrope, mtunza kumbukumbu kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Morogoro, alisema upo umuhimu mkubwa wa wanataaluma kukutana na kila mwaka kwa lengo la kukumbusha majukumu yao na kubadilishana uzoefu wa kazi.



## 'Lugha gongana' taasisi za kimataifa inaathiri maendeleo nchi wahitaji

Ukurasa 19

UCHUMI



## Wizara Mifugo yajitosa upya ubora wa malisho wanyama

Ukurasa 14


# BUFE

Ijumaa Novemba 1, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




TOSCI & MSIMU ULIOFIKA;

# Darasa sahihi kutajirika kwa kilimo muhogo, tahadhari zake

Ukurasa 16


UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

# Wizara Mifugo ya ubora wa malisho

• Wataalamu wakutana Mpwapwa kunoa ubongo
• Ikifanikiwa, wadai mwisho mapigano wafugaji

**Na Renatha Msungu, aliyekuwa Mpwapwa**

UELEWA wa pamoja katika uzalishaji wa mashamba ya malisho, utunzaji wa nyanda za malisho na maeneo ya machunga, ni chachu kuinua sekta ya

mifugo kuleta tija kwa jamii na taifa kwa ujumla, ikiwamo kuwainua kiuchumi wafugaji.

Hivi karibuni, wadau na wataalamu wa malisho nchini walikutana na kujadili namna ya kukabiliana na changamoto ya malisho katika maeneo mbalimbali, ili nchi ijitosheleze kwa chakula cha mifugo.

Kongamano hilo lilifanyika wilayani Mpwapwa Dodoma, Liliwakutanisha wadau na wataalamu wa sekta ya mifugo nchini, lengo ni kujadili kwa kina mikakati ya kuzalisha malisho bora na ya kutosha.

Mafunzo hayo yamefanyika, kukiwapo ukweli kwamba katika sehemu nyingi nchini zimekumbwa na changamoto ya uhaba wa machunga na nyanda za malisho ya mifugo, jambo ambalo kuna wakati liliibua migogoro kati ya wafugaji na wakulima.

**JITIHADA SERIKALINI**

Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Angello Mwilawa, anasema wadau na wataalamu wa malisho kutoka mashamba ya serikali, wanapaswa kuona namna bora nyanda za malisho na maeneo ya machunga, zinaboreshwa kutosheleza malisho ya mifugo.

Anasema, lengo ni kuwa na malisho yanayozaa kwa wingi na yenye ubora unaomsaidia mnyama kupata virutubisho sahihi, ili azalishe bidhaa bora zitokanazo na wanyama.

"Kuna wakati nchi iliwahi kukumbwa na ukame na idadi kubwa ya mifugo ilikufa. Sitamani kuona hali hii inajirudia tena wakati wataalamu wapo," anasema Dk. Mwilawa.

Anafafanua kwamba, wizara imekuwa ikitekeleza mikakati ya upatikanaji malisho na maji nchi nzima, ili kuhakikisha wafugaji wanapata tija, wanufaika na jamii kwa ujumla.

Dk. Mwilawa anashauri ni vyema mafunzo wanayopata kila mara kuyatumia kwa vitendo, kusaidia kuongeza uzalishaji malisho katika nyanda tofauti wanazotoka, jambo litakalowasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji.

"Serikali imekuwa ikihakikisha zile nyanda zetu za malisho wafugaji wanapata elimu ya kutosha na watumiaji wengine wa nyanda za malisho

kwa kuhakikisha kunakuwa na matunzo na matumizi endelevu ya malisho," anasema Dk Mwilawa.

Anafafanua kwamba kumekuwapo na mikakati ya wizara kudhibiti magonjwa ya mifugo na matumizi ya dawa na

viuatilifu, kuhakikisha afya ya mifugo inakuwa katika ubora unaotakiwa.

Dk. Mwilawa anasema mikakati hiyo hivi sasa inaendelea kufanyiwa kazi, kuhakikisha kila kona



Ng'ombe wa kisasa wakipatiwa lishe.

> **"Tufike sehemu kama taifa, tuwe na ghala la malisho hata itakapotokea njaa ya malisho kwa miaka miwili, kusiwe na mifugo inayokufa, bali ilishwe kupitia hifadhi ya malisho itakayokuwapo," anasema Mzava.**

kunakuwapo akiba kubwa ya malisho, inapotokea upungufu kulingana na majira yaliyopo, kuwapo uwezekano wa kulisha mifugo.

**MKUU CHUO LITA**

Moses Mlahagwa, ni Mkuu wa Chuo cha Mifugo (Lita), anasema ili mifugo izalishe maziwa na nyama ya kutosha, ni lazima wapate chakula cha kutosha na chenye malisho.

Mlahagwa anaeleza kuwapo changamoto katika uzalishaji wa mazao ya mifugo, kutokana na mifugo mingi kuwa na lishe duni inayosababishwa na uhaba wa maeneo ya machunga na nyanda za malisho.

Anasema, mafunzo yamekuwa yakitolewa kila mara na Wizara ya Mifugo kwa wataalamu wa malisho, ili yawe chachu ya kubuni mbinu na mikakati inayohakikisha wanaongeza uzalishaji.

"Ni vizuri wataalamu matumie mafunzo haya kuongeza uzalishaji

> **"Kwenye mafunzo yale, tumeona changamoto ni kubwa ya vyakula vya mifugo, inayosababisha kudumaa sekta ya mifugo. Sasa tunaweza kuchukulia hiyo kama fursa ya kupiga hatua kwenye uzalishaji," anaeleza.**

wa malisho lengo ni kuona mifugo yetu inapata chakula cha kutosha," anasema Mlahagwa.

Anasema chuo chake kipo kwenye mpango wa kuwa na maeneo makubwa ya uzalishaji malisho, hivyo ni fursa nzuri kwao kuhakikisha wanaingia kwenye eneo la uzalishaji kwa kupata uzoefu wa kutosha kutoka kwa wadau wengine.

"Kwenye mafunzo yale, tumeona changamoto ni kubwa ya vyakula vya mifugo, inayosababisha kudumaa sekta ya mifugo. Sasa tunaweza kuchukulia hiyo kama fursa ya kupiga hatua kwenye uzalishaji," anaeleza.

**CHANGAMOTO WATENDAJI**

Ofisa Mifugo na Mkuu Idara ya Malisho na Rasilimali ya Vyakula, kutoka Wizara ya Mifugo, Israel Kilonzo, anasema serikali inatoa mafunzo ya kila mara kuhusu malisho, ili wataalamu waelewe, pia uzalishaji wa malisho na kutunza

# jitosa upya wanyama

nyanda zake.

Anasema, hicho kinafanyika ili kutoiangusha sekta kwa sababu wao ndio wataalamu na wanapaswa kuwa mstari wa mbele kusambaza elimu ya utunzaji malisho kwa wafugaji.

Kilonzo anasema ni vyema kuanzia sasa, kero ya upatikanaji duni wa malisho ifike mwisho, kwa sababu wataalamu wapo na ujuzi wameongezewa

**BOSI NARCO**

Meneja Masoko la Mamlaka ya Ranchi za Taifa (NARCO), Mzava Emmanuel, anakumbnusha wakati nchi ilikumbwa na ukame na mifugo kufa, hivyo sasa haipaswi kujirudia tena kwa kuwa hakuna sababu ya hulo kutokea.

"Tufike sehemu kama taifa, tuwe na ghala la malisho hata itakapotokea njaa ya malisho kwa miaka miwili, kusiwe na mifugo inayokufa, bali ilishwe kupitia hifadhi ya malisho itakayokuwapo," anasema Mzava.

Anasema, hilo lilikifanyika itafikia mwisho wa kuwapo migogoro ya wakulima na wafugaji, ambayo imeshuhudia katika baadhi ya maeneo nchini.

**UZALISHAJI UKOJE?**

Ofisa Mifugo kutoka la Mifugo la Mabuki, ambaye pia ni na mtaalamu wa malisho, Asteria Mwaya, anasema ili kuwa na mbegu bora ya malisho, kunapaswa shamba liandaliwe vyema, kuvunwa na kuhifadhiwa kwa ubora.

Anataja mbinu za kuepuka uharibifu wa nyanda za malisho, ni kuchunga na kubakiza kiasi cha malisho ambayo inaweza kuchipua, iwe na ladha ya kupendeza mdomoni mwa wanyama, akimtaja kwa upekee ng'ombe.

Asteria anasema kuwa, nyanda za malisho nchini, zina mchanganyiko wa malisho ya aina mbalimbali za nyasi, akitaja mfano katika jina la kitaalamu 'Themeda' zinazopendwa sana na mifugo.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, sehemu kubwa ya mbuga za malisho nchini, ziko kwenye ardhi kame na ndio sababu mifugo mingi iko kwenye eneo hilo na kuna uharibifu wa ardhi na malisho, ambalo liko wazi bila ya majani wala miti.

Asteria, anafafanua kwamba ni chanzo cha kupotea majani ya asili na nafasi yake kuchukuliwa na magugu na majani yasiyofaa kwa mifugo, hivyo kuepuka uharibifu wa nyanda za malisho, anashauri kuchunga na kubakiza kiasi cha malisho kinachoweza kuchipua haraka.

**UPANDAJI MALISHO**

Dk. Mwilawa anataja mambo ya kuzingatia wakati wa kupanda malisho, ni uwiano wa mbegu na eneo linalopandwa.

Anasema kila aina ya mbegu ina kiasi cha kupanda kwa eneo na haitakiwi mbegu zote nyingi katika eneo dogo, ili kuepuka msongamano na ushindani wa kupata virutubisho, mwanga na maji kwa mimea hiyo.

Anataja mbegu hizo zinapatikana katika mashamba ya serikali ya kuzalisha mbegu za malisho ya Vikuge (Pwani); Langwira na Uyole (Mbeya) na SaoHill, Iringa.

Dk. Mwilawa anasema, ili kuyalinda na kutoharibu malisho. ni muhimu kuzingatia idadi ya mifugo kulingana na ukubwa wa eneo lililopo na vyema mkulima kupata mbegu za malisho zilizohakikiwa na wataalamu, zinazopatikana katika mashamba ya serikali.



Ng'ombe wakiwa machungani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Digitized via ippmedia

Picha ya tukio la moto wa treni. **PICHA:MTANDAO.**

# Treni yawaka moto, abiria 65 wafariki

- Mlipuko stovu ya chai Karachi, Pakistan

TAKRIBAN abiria 65 wamefariki wakati treni iliyokuwa ikisafiri kutoka mji wa Karachi Pakistan, kuelekea Rawalpindim, mara iliposhika moto.

Waziri wa Reli, Sheikh Ahmed, amesema kwamba moto huo umesababishwa na kulipuka kwa mtungi wa gesi uliokuwa ukitumiwa na abiria kupikia kifungua kinywa asubuhi.

Moto huo unadaiwa kusambaa hadi katika mabehewa matatu, kwa mujibu wa maofisa waliohukuliwa katika vyombo vya habari vya eneo hilo na waathiriwa wengi walifariki, walipojaribu kuruka kutoka kwa treni hiyo ilitokuwa katika mwendo mkali.

Pia, kuna watu wengine 30wameripotiwa kujeruhiwa na maofisa wanasema kwamba idadi ya waliofariki huenda ikaongezeka.

"Majiko mawili aina ya 'stove' yalilipuka. Walikuwa wakipika na walikuwa na mafuta ya kupikia ambayo yalichochea moto huo kuongezeka," alisema Waziri Sheikh Rashid Ahmed.

Inaelezwa kwamba, abiria wanaoingia na 'stove' katika treni imekuwa tabia kupika chakula wakati wa safari ndefu na imekuwa suala la kawaida na waziri huyo aliongeza kwamba abiria wengi walikuwa wakielekea katika kongamano lililoandaliwa na vuguvu la dhehebu la Kisuni Tablighi Jamaat.

Ajali hiyo ilitokea karibu na Rahim Yar Khan Kusini mwa Mkoa wa Punjab na ilikuwa ikisafiri kutoka Karachi kupitia maeneo mengi ya Pakistan hadi Rawalpindi.

Treni hiyo iliyopata ajali inatajwa ni mojawapo ya treni za zamani ambayo ni maarufu sana nchini humo.

Pakistan ina historia ya ajali za gari moshi zinazosababisha maafa mengi na waathirika huwa wengi katika ajali hizo za treni zinazobeba watu zaidi ya viwango rasmi vilivyoidhinishwa.

Mnamo Julai 11 mwaka huu kulikuwapo ajali, pia watu walifariki katika ajali na wengine wanne katika ajali nyingine mwezi Septemba.

Mwaka 2007, takriban watu 56 walikufa na wengine zaidi ya 120 kujeruhiwa katika ajali ya treni karibu na eneo la Mehrabpur.

Mwaka 2005, zaidi ya watu 130 walikufa wakati treni tatu zilipogongana katika mkoa wa Sindh, katika kile kilichotajwa kuwa ajali mbaya zaidi inayohusisha treni kuwahi kutokea.

UCHUMI

TOSCI & MSIMU ULIOFIKA;

# Darasa sahihi kutajirika kwa kilimo muhogo, tahadhari zake

- Hii hapa staili ya kulima, wadudu, magonjwa

**Na Christina Haule, Morogoro**

MIHOGO ni vyakula vinavyotumika kwa namna nyingi. Kuhimili njaa, mlo wa kawaida, pia biashara,

Hivi sasa wakulima nchini wanatakiwa kutumia vyema msimu wao, kwa kupanda kwa wakati kipindi hiki ili kuzalisha kwa tija, kwani wanapozalisha kitaalamu kutumia takriban tani 18 hadi 19 za mbegu kwa hekta moja huwaletea tija ya kilimo hicho.

Mkurugenzi wa Udhibiti wa Ubora wa Mbegu kutoka Taasisi ya kudhibiti ubora wa mbegu nchini (TOSCI), Dk. George Swella, anazungumzia msimu wa kilimo cha mihogo unaoanza mwezi Oktoba kila mwaka, akiwataka wakulima kuwa makini kuzingatia ushauri wa kitaalamu wanaopewa.

Anasema, wakulima wana uwezo wa kupata mbegu bora au mazao bora yatakayosaidia kukuza uchumi wao na kuleta manufaa ya kilimo hicho pia kwa Taifa.

Hivyo, anawataka wakulima kuona umuhimu wa kutumia mbegu bora na zinazothibitishwa ubora na TOSCI, kutoka kanda mbalimbali za kilimo, kupitia ofisi za TOSCI nchi nzima.

Dk. Swella anasema, anayelima hekta moja ya mihogo wa ajili ya mbegu, anayefuata ushauri wa kitaalamu kwa kupanda kati ya umbali wa sentimeta 50 na akizingatia matumizi ya mbolea na anavuna wastani wa kuvuna kati ya tani 19 hadi 20 kwa hekta.

Pia, anasema kwa kutumia vipimo hivyo wanaweza kuvuna mihogo ya chakula hadi tani 14 kwa shamba hilo hilo

Anasema la mihogo ni zao linalostahimili ukame na inamuwezesha mkulima kuwa na akiba ya chakula wakati wote, kutokana na mavuno mengi.

Ofisa wa Udhibiti Ubora wa Mbegu za Mihogo, kutoka TOSCI, Zera Mwankemwa, anawashauri walima mihogo kutumia mbegu kulingana na maeneo waliopo, ili kuleta tija ya kilimo hicho nchini.

**AINA ZA MBEGU**

Kitaalamu kuna aina 20 za mbegu za mihogo zinazotumika katika maeneo tofauti, kulingana na hali ya udongo wa eneo husika na kwamba mkulima akitumia mbegu isiyofaa kwa udongo wa eneo lake, huenda asipate mazao yanayolingana na maelekezo ya zao hilo.

Mwankemwa anasema, Kanda ya Ziwa nchini wanapaswa kutumia mbegu aina ya Mkombozi, Kanda ya Mashariki mbegu aina ya Mkuranga, kanda ya kati na kusini ni mbegu aina ya Kiroba.

Anasema mbegu hizo zinapolimwa kitaalamu zinaweza kuzalisha vyema na kwamba mbegu aina ya Mkombozi hutoa tani 18 kwa hekta, Mkuranga tani 19 kwa hekta, Kipusa tani 18 kwa hekta na Mumba tani 19.

Mtafiti Msaidizi kutoka TOSCI, Matengia Swai anasema tangu mwaka 2013 hadi sasa kuna aina 20 za mbegu za mihogo, ambazo zimekuwa zikifanya vizuri kilimo nchini na kuendelea kufanyiwa utafiti kwa matokeo chanya.



Majani ya muhogo yaliyoathiriwa na ugonjwa michirizi ya kahawia. Picha nyingine, muhogo zao la muhogo ulioathirika. **PICHA: MTANDAO WA MOGRICUTURE.**

> **“Tanabui au Utitiri wa Kijani wa Muhogo; ni mdudu mdogo mwenye rangi ya kijani na manjano, asiyeonekana kirahisi. Idadi yao huongezeka wakati wa ukame na hupungua wakati wa mvua, inapoanza hata hatua ya matone.**

Swai anasema mkulima anapaswa kutumia mbegu bora, kwa sababu ya kuwapo uzao wa aina nyingi inayoweza kuvumilia ukame.

Anasema, wakulima wanaweza kupambana na changamoto ya uzalishaji mdogo na magonjwa ya mimea, watakapoamua kugeuka wakijikita na ushauri wa kitaalamu, kuzingatia matumizi ya mbegu bora.

**CHANGAMOTO**

Kwa mujibu wa Mtandao wa Mogriculture, kilimo cha muhogo, kama zilivyo mazao mengine ya mizizi, kinazongwa na changamoto za wadudu na magonjwa wanaochangia kwa kiasi kupunguza mavuno na ubora wa mazao.

Pia, wadudu athari zao ni kuongeza gharama za uzalishaji ambazo hazikutarajiwa. Hivyo, inaelezwa kitaalamu ni muhimu mkulima kuwa na ufahamu sahihi, ili aandae mazingira bora yatakayozuia kuenea kwa wadudu na magonjwa ya mihogo.



Muhogo uliochibwa kutoka shamba lililostawi. **PICHA: MTANDAO.**

**WADUDU WAHARIBIFU**

Wadudu waharibifu zaidi wa mihogo kwa mujibu wa mtandao wa Mogriculture wanaitwa Utitiri wa Kijani wa Muhogo, Vidung'ata, Nzi Mweupe, Vidugamba Weupe wa Muhogo na Mchwa na wanaweza kusababisha hasara kubwa kupunguza mavuno hata kwa asilimia 10 hadi 100.

Wakulima wanaaswa kuwa na ufahamu wa wadudu hao hasa Nzi Mweupe, kwa sababu wanaweza kusambaza virusi vya magonjwa ya batobato na michirizi kahawia.

Tanabui au Utitiri wa Kijani wa Muhogo; ni mdudu mdogo mwenye rangi ya kijani na manjano, asiyeonekana kirahisi. Idadi yao huongezeka wakati wa ukame na hupungua wakati wa mvua, inapoanza hata hatua ya matone.

Ni wadudu wanaoweza kusambaa kwa kutembea, kupeperushwa na upepo, pia kupanda mbegu yenye wadudu hao.

Dalili zake ni jani la muhogo kupauka kwa rangi njano au kupauka ya kutoboka mithili ya kutumiwa sindano na inadhibitiwa kwa kutumia mbegu kinzani dhidi ya mashambulizi au kutumia wadudu wanaokula utitiri.

Wadudu Vidung'ata, huonekana kama unga mweupe uliofunika sehemu ya juu ya mimea inayochipua, wakikwa na rangi ya maziwa, utando mweupe na umbo mfano wa aina hawana mabawa, zaidi wanapatikana katika msimu wa kiangazi.

Hao wanasambazwa na upepo na athari zake ziko kuanzia hatua ya asilimia 10 ya mazao, dalili kuu pingili za muhogo huwa fupi na majani ya kileleni huonekana kama fundo.

Katika udhibiti, njia mojawapo inayotumiwa ni wadudu manyigu; pia kuloweka pingili kwenye viuatilifu kwa kutumia vipimo sahihi na kung'oa na kuchoma mimea iliyoathirika.

Nzi mweupe; hao ni wadudu wadogo wenye mabawa meupe wanaopendelea kuishi chini ya majani machanga na wanaenea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa kuruka au kupeperushwa na upepo.

Nzi weupe; ni vigurusha (vector) wanaoeneza magonjwa ya batobato na michirizi ya kahawia. Wanapunguza ufanisi wa utengenezaji chakula cha mmea na wanaweza kusababisha upotevu wa mavuno kati ya asilimia 40 hadi 75.

Dalili muhimu zinatajwa kuwa wanaharibu majani ya mmea wa muhogo na maji wanayodondosha husababisha fangasi kuzaliana na kuleta ukungu mweusi kwenye majani ya mmea.

Udhibiti wake ni kwa kutumia wadudu adui wao kama vile dudukobe na vizuizi vya asili kama misitu.

Vidugamba weupe wa muhogo (Cassava white scales); ni wadudu weupe kwenye shina la muhogo, wanaofyonza maji toka kwenye shina la mmea na kupotezea maji mengi, ikiishia kupunguza mavuno.

Dalili zake ni kama mchanga mweupe uliofunika sehemu za shina la muhogo. Udhibiti unatumika ni kuung'oa na mmea uliyoshambuliwa na kuuchoma.

Pia, inatumika kubadilisha mazao na kupanda jamii ya mazao ya mikunde, baada ya zao la muhogo kuongeza rutuba ya udongo au kuchovya pingili za muhogo kwenye maji yaliyochemshwa au kwenye viuatilifu.

Mchwa; ni mdudu anayeshambulia shina la muhogo wakati wa kiangazi na kusababisha kukauka. Kipindi cha mvua, mchwa hufanya kazi ya kuozesha masalia ya mimea na kuimarisha mzunguko wa hewa katika udongo.

Udhibiti wake ni kupanda mapema wakati udongo una unyevu wa kutosha na kutumia tumbaku kuwafukuza mchwa. Pia, uchimbaji vichuguu ndani ya shamba inapunguza mazalia yake ya kupa miti ya minyaa.

## BIASHARA KATIKA PICHA



Kaimu Mkurugenzi wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna akiongea kwenye mdahalo ulioandaliwa na shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), kuhusu usawa wa kijinsia makazini na kufanyika jijini Dar es Salaam jana. Mdahalo huo ulikutanisha wakurugenzi kutoka taasisi za fedha, wajasiriamali na jinsia nchini. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani na Hodan Addou kutoka Umoja wa Mataifa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mchuuzi wa ndizi mbivu (kushoto), akizipanga vizuri katika makutano ya mtaa wa Mkwepu na Makunganya, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, kabla ya kuingia mitaani kusaka wateja. **PICHA: JOHN BADI**



Wachuuzi wa bidhaa mbalimbali wakiwa wamezipanga kwenye barabara ya waenda kwa miguu na kusababisha usumbufu, nje ya soko la Mabibo, jijini Dar es Salaaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

BIASHARA




Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati), akizungumza na wafanyabiashara wa mifugo katika Wilaya ya Longido. **PICHA ZOTE: NOVATUS MAKUNGA.**

MENEJA KIJAVARA:

# Bandari Mtwara tunajipanga kimataifa, korosho ilitupotezea mzigo robo tatu

**Na Mary Geofrey, MTWARA**

BANDARI ya Mtwara imo katika orodha ya bandari kuu tatu nchini katika mwambao wa Bahari ya Hindi, chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Bandari nyingine kuu ni Dar es Salaam na Tanga, pamoja na zile za maziwa makuu, ambazo kwa mujibu wa Sheria ya Bandari ya mwaka 2004, zote ikiwa chini ya TPA tangu mwaka 2006, ikipanuliwa wigo wa majukumu zaidi ya kumiliki na uendeshaji.

Meneja wa Bandari ya Mtwara, Mhandisi Juma Kijavara, anasema ina uwezo wa kuhudumia kwa usalama meli zenye urefu wa mita 222 na kina kisichozidi mita 9.5 katika gati lenye urefu wa mita 385 na katika kufanikisha kutoa huduma hizo kwa ufanisi, wanafanya kazi kwa saa 24 kila siku saba za wiki.

Mhandisi Kijavara anasema bandari ya Mtwara inatumika kufanikisha biashara kwa bidhaa zitokazo nchini kwenda nchi za nje hasa Msumbiji, Comoro, India na Vietnam.

"Bandari hii pia inatumika kwa biashara ya ndani ya nchi hasa kati ya Mtwara na Visiwa vya Unguja na Mafia," anasema Kijavara na kufafanua kwamba, bandari hiyo imekuwa ikihudumia zaidi shehena za korosho ambayo ni zao kuu la biashara kwa mikoa ya Kusini, kwa maana ya Lindi, Mtwara na sehemu za mikoa ya Pwani na Ruvuma, huku akiitaja kwa upekee Kilwa na nafasi yake.

Pia, anataja mzigo mingine ni shehena za saruji, bidhaa za vyakula, mitambo kwa ajili ya miradi mbalimbali na shehena ya 'majimaji' kama vile kemikali na mafuta.

**UWEZO WA SHEHENA**

Mhandisi Kijavara, anasema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 shehena zilizohudumiwa na bandari ya Mtwara, kwa jumla zilikuwa tani 106,170.

"Utendaji huu ni pungufu kwa asilimia 71 ya shehena tani 363,287 zilizohudumiwa mwaka 2017/18. Kupungua kwa shehena iliyohudumiwa kulitokana na kutosafirisha shehena ya korosho pamoja na makaa ya mawe kama ilivyokuwa katika matarajio ya bandari," anasema Kijavara.

Anaeleza kwamba, uwezo wa bandari hiyo ni kuhudumia tani 400,000 kwa mwaka na kwamba mwaka 2016/17 walihudumia tani 377,590.

Mhandisi Kijavara anatoa mchaganuo kwamba, walishusha tani 91,378 na tani nyingine 286,212 zilipakiwa kutoka Mtwara kwenda mikoa mingine na nje ya nchi.

Anasema, pia mwaka 2015/16 walihudumia jumla ya tani 268,055 na kati yake, tani 126,202 zilishushwa katika bandari hiyo na 141, 833 na zilisafirishwa kwenda nje ya Mtwara.

Katika mwaka 2014/15 anasema, walihudumia tani 296,577 na kati yake tani 167,691 zilishushwa katika bandari hiyo na nyingine 128,886 zilipakiwa.

> "Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, idadi ya meli zilizohudumiwa katika bandari hii zilikuwa ni meli 141 ikilinganishwa na meli 66 zilizohudumiwa mwaka wa fedha 2017/18, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 113 linalotokana na kuongezeka kwa meli za mwambao," anasema meneja huyo.

Mwaka 2013/14 jumla ya shehena zilizohudumiwa katika bandari hiyo ni 356,356 na kati yake tani 221,022 zilipakuliwa katika bandari hiyo na 135,334 zilipakiwa kwenda maeneo mikoa mingine na nchi jirani.

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, idadi ya meli zilizohudumiwa katika bandari hii zilikuwa ni meli 141 ikilinganishwa na meli 66 zilizohudumiwa mwaka wa fedha 2017/18, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 113 linalotokana na kuongezeka kwa meli za mwambao," anasema meneja huyo.

Mhandisi Kijavara, anafafanya kuwa, katika mwaka wa fedha 2016/17 walihudumia meli 105 na kati yake, 56 ni za mwambao na 49 zilikuwa za kimataifa.

Anasema mwaka 2015/16 walihudumia meli 118 kati yake 87 zilikuwa za mwambao na 31 zilikuwa za kimataifa.

Kijavara anasema katika mwaka wa fedha 2014/15, walipokea meli 409 na kati yake, 363 zilikuwa za mwambao na 46 za kimataifa.

Kwa mujibu wa meneja, takwimu za mwaka 2013/14 zinabainisha walipokea meli 544 na kati ya hizo 479 zilikuwa za mwambao na 65 za kimataifa.

Kuhusu mapato na matumizi anasema, katika kipindi cha mwaka 2018/19 Bandari ya Mtwara ilipata Sh. milioni 5.645, ikilinganishwa na Sh. milioni 30.920 za mwaka 2017/18, ambayo ni sawa na upungufu ya asilimia 82.

Anasema kulikuwapo matumizi ya kawaida ya Sh. milioni 16.787 yaliyopfanyika katika mwaka 2018/19 ukilinganisha na Sh. milioni 21.238 katika mwaka 2017/18.

"Kupungua kwa mapato kumetokana na kutosafirisha shehena ya korosho kwenda masoko ya nje," anasema Kijavara.

**MIRADI MAENDELEO**

Mhandishi Kijavara, anasema mamlaka sasa inawekeza katika miradi ya maendeleo, ikiwamo mpango wa ununuzi wa vifaa vya utekelezaji ujenzi wa miundombinu ya bandari kwa kuzingatia mpango mkuu na mpango mkakati wa mamlaka.

"Serikali ina mpango wa kupanua bandari ya Mtwara kwa kujenga gati nne mpya na kuifanya kuwa ya kisasa kwa ajili ya kuhudumia shehena ya gesi, mafuta na mazao ya kilimo katika ukanda wa maendeleo wa Mtwara unaojumuisha mikoa iliyoko Kusini na nchi za jirani za Malawi, Zambia na Msumbiji," anasema Kijavara.

Anaeleza kuwa, ili kuongeza ufanisi wa bandari hiyo, wameanza ujenzi wa gati anayoitaja 'Namba Mbili' katika bandari hiyo na awamu ya kwanza ya utekelezaji unahusisha ujenzi wa gati la urefu wa mita 300 la kuhudumia shehena mchanganyiko.

Meneja anasema, mkataba kati ya TPA na Mkandarasi ambaye ni muunganiko wa kampuni anazojitajka za China Railway Construction Engendering Group (CRCEG) na China Railway Major Bridge Engineering Group (CRMBEG), ulitiwa saini Machi 4 mwaka 2017 na unatarajiwa kukamilika Machi 20, mwaka ujao.

"Ujenzi wa gati hili unatarajiwa kukamilika Machi mwakani. Hadi sasa kazi ya usanifu imekamilika na ujenzi inaendelea na imefika asilimia 55 na itakapokamilika utawezesha bandari kuhudumia takribani tani milioni moja," anasema Kijavara.

UCHUMI

# ‘Lugha gongana’ taasisi za kimataifa inaathiri maendeleo nchi wahitaji

**Na Nimi Mweta**



KILA wakati kunapokuwapo tukio au kumbukumbu fulani kimataifa, wataalamu na watawala serikalini katika fani tofauti, wanakutana kujadili yaliyomo katika medani hiyo au mada muhimu za kuzingtia, kuhusiana na hali ya taifa katika masuala hayo.

Kuna aina kadhaa za michango ya kitaaluma, kuacha maelezo kuhusu misimamo ya serikali ambayo kwa kawaida inatolewa na viongozi wa kitaifa au wasemaji wa wizara husika, kuwasaidia wataalamu kujua wapi serikali imesimama.

Pia, inaweza kufanya hivyo kuhakikisha wanaelewa suala hilo kwa mapana na marefu. Ni kufungua macho na kuwekana sawa.

Tatizo linakuja kutokana na mtawamyiko wa hisia na tofauti za kitaaluma zinazoendana na hisia hizo, ambazo katika ngazi ya fikra hugeuka mitazamo tofauti kuhusu mahitaji muhimu ya maendeleo na kwa maana hiyo, mbinu (nje ya mikakati mikuu) ambazo serikali inahitaji kuzitumia kufaulu.

Katika kujadili mbinu za wataalamu huwa wanakwepa kuijadili mikakati mikubwa, kwa sababu ya hofu kutofautiana wenyewe, pia watawala au kumhitaji kila mmoja aonyeshe hisia zake kuhusu mikakati hiyo. Inakuwa si mahali pale, ila michango yao kuhusu mbinu za uchumi inapindisha mikakati.

Baada ya kushiriki warsha au tamasha na kuwasikiliza wataalamu na wadau kutoka mashirika tofauti ya kimataifa, pamoja na wataalamu wengine wa ndani, ikiwajumuisha wanaharakati na wasomi huria wanaoaminiwa katika utafiti, inabidi washauri sera waangalie kwa makini. Hiyo inawapa kazi ngumu kuoanisha hisia zinazotolewa kila siku kuendana na mikakati mikuu ya serikali, mwelekeo au matazamo yake kiuchumi na kujifunza zaidi kinachoonekana katika jamii.

Kuna upande wa jamii, matokeo kiuchumi ndani ya sekta tofauti, zinavyohusiana na mikakati iliyopo kila siku.

Tatizo linaloonekana ni kinachoitwa kitaalamu ‘monads’ za kifikra (neno la mfikiriaji wa Ujerumani Gottfried Leibniz) kwa kila kinachosemwa, kinaonekana ‘ni kweli’ kutokana na kuzungumzwa na mtaalamu; naweza kuwa mtu mmoja mmoja au taasisi ya kitaalamu kama shirika mojawapo la Umoja wa Mataifa.

**USAHIHI U WAPI?**

Mfano, kwa fikra ya mtaalamu wa Kijerumani, Max Weber, mapema karne iliyopita, anakuwa na kofia mbili za kuwa sahihi; kwanza alikuwa mtumishi mwandamizi wa Umoja wa Mataifa au balozi wa nchi, pia msomi halisi.

> **Ndiyo maana inabidi kutambua mijadala kuhusu maendeleo, kwamba ina sura tofauti ambako mashirika ya Umoja wa Mataifa yanatoa michango kuhusu sekta tofauti na jinsi zinavyotakiwa kusimamiwa au jinsi kinachofanyika kinavyoweza kupimwa, kutolewa tathmini.**

Endapo washauri sera serikalini wataona kila linalozungumzwa na watu kama hao ni sahihi, swali linajitokeza watayajuaje makosa pale washauri wanapotofautiana au kwa usahihi zaidi, mada zao zinapotofautiana?

Ndiyo maana inabidi kutambua mijadala kuhusu maendeleo, kwamba ina sura tofauti ambako mashirika ya Umoja wa Mataifa yanatoa michango kuhusu sekta tofauti na jinsi zinavyotakiwa kusimamiwa au jinsi kinachofanyika kinavyoweza kupimwa, kutolewa tathmini.

Ni tatizo linalojitokeza katika mjadala mpana wa kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SGDs) ya Umoja wa Mataifa. Ni malengo yanayoangaliwa kwa mwelekeo tofauti, kila mmoja ukiunda taswira ya matokeo yanayohitajiwa na mbinu zinazotakiwa kufuatwa. Hapo ndipo zinapoangaliwa kwa karibu zinaweza tofautiana, ingawa hata mara moja ikazua mabishano hadharani.

Michango ya sera kama ilivyo ya siasa au bunge, ina hulka ya kujitosheleza, isiyohitaji hisia au siasa zake, kwa mfano kama mzungumzaji anapenda Ujamaa au Uhuria, usawa au kujilimbikizia mali, uchumi unaokua haraka kwa mbinu zozote zile au uchumi wa kizalendo hata kama haukui haraka.

Kila mzungumzaji atajaribu kuleta hisia kuwa mwelekeo anaotaka unaleta maendeleo ya haraka pamoja na kile anachokitaka, kwa mfano ushirikishwaji wanawake na kulinda viwanda nchini, hakuna anayekubali athari katika mikono ya mtazamo wake.

**UTAFITI UCHUMI**

Historia ya utafiti uchumi au nadharia ya ukuaji wake uchumi, kuna tofauti kubwa katika uchumi ambao msingi wake ni soko kwa ngazi tofauti za maendeleo na hata mifumo ya umiliki wa rasilimali kati ya sera zinazoleta usawa kati ya watu (Ujamaa) na zile zinazoleta uchumi kukua haraka (soko huria na uliberali).

Kupambanua kati ya maeneo hayo mawili ni ngumu, kwani ni nadra kumpata mtaalamu atakayetoa jibu sahihi. Atasimama katika mizania tofauti ya kupunguza pengo kati ya walionacho na wasionacho’ wakati tatizo katika maisha siyo ‘pengo’ la kipato ila ‘kumudu maisha.’

Kwa maana hiyo, kuna umuhimu mkubwa kwa washauri sera kuwa macho na aina tofauti za ushauri na athari zake kiuchumi, kwa msingi wa kuelewa au kuwa ‘macho makavu’ kwamba wanataka nini hasa katika maisha.

Takriban vijana wote wanaomaliza shule wanabakiwa kubangaiza hata siyo kusaka tonge, ambao ni ujasiriamali na ujana wa uwekezaji.

Nini njia ya kutatua mkwamo huo kama si kufungulia njia za biashara ambazo sasa zimeshikiliwa na wadau maalum wanaowakilisha uzalendo wetu, Uafrika wetu, Utanzania wetu na hata utu wetu?

Washauri sera inabidi waweze kupambanua kati ya matokeo tarajiwa ya mwelekeo mmoja au mwingine, na kwa mfano suala hili la kurahisisha mandhari ya kufanya biashara, kama ni kuwasaidia tu wageni ‘wanaosaka tonge’ nchini au ni suala pana la kuwezesha ajira na ustawi wa jamii kwa jumla - au ustawi wa jamii ni ujenzi wa reli, mashule, barabara, zahanati, uimarishaji wa utalii kwa ndege zetu.

UCHUMI

CTI NA TUZO ZA RAIS

# Majaliwa aonyesha safari ya viwanda nchini zinakoelekea

## • Chachu hai maendeleo; uchumi kitaifa

**Na Reubeni Lumbagala**

DIRA ya Maendeleo iliyopo sasa ni kuiunda 'Tanzania' ya Viwanda' na yenye 'Uchumi wa Kati' ifikapo mwaka 2025. Ni dira inayosimamiwa na kila wizara inayohusika nayo katika nafasi yake, kutekeleza majukumu hayo ipasavyo, ili kufanikisha azma na lengo tajwa ifikiwe.

Katika mchango wake, Shirikisho la WenyeViwanda Tanzania (CTI), limeandaa utaratibu wa kutunuku kampuni na wazalishaji wanaofanya vizuri katika kuchagiza maendeleo ya viwanda nchini.

Tarehe 17 ya mwezi huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alikuwa mgeni rasmi kumwakilisha Rais Dk. John Magufuli, katika utoaji tuzo za Rais kwa viwanda vilivyofanya vizuri mwaka jana.

Ni hafla iliyofanyika kwenye hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam, ambako Majaliwa alitamka:"Kila mmoja wetu anatambua umuhimu wa sekta ya viwanda katika kukuza uchumi wa nchi yoyote duniani.

"Viwanda ndivyo vimekuwa chimbuko la maendeleo ya haraka ya nchi mbalimbali duniani na mhimili mkuu wa kutegemewa katika kuondoa umaskini, kwa kutoa ajira nyingi na za uhakika kwa wananchi. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yanategemea sana sekta ya viwanda."

Sekta ya viwanda inajulikana kwa unyeti wake na inaaminika ikipata msukumo sahihi na wa kipekee, itasaidia kuleta mafanikio na maendeleo ya haraka nchini.

Viwanda vina nafasi kubwa katika kusaidia ukuaji wa sekta nyinginezo, kutokana na ushirikiano wa kisekta katika maendeleo ya viwanda.

Mathalani, inakuza sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, usafirishaji, maji, nishati na elimu. Hivyo basi, juhudi za kuikuza sekta ya viwanda, zinaambatana na ukuaji wa sekta nyinginezo, hivyo kusababisha ukuaji uchumi na maendeleo kwa ujumla.

Kazi kubwa inayofanywa na inaendelea kufanywa na serikali katika kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ni kuwekeza katika ulingo wa uchumi, kwani yapo maeneo mengi ambayo wawekezaji wanaweza kuweka mitaji yao na kupata faida.

Njia mojawapo ya kukuza sekta ya viwandani ni pamoja na serikali kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara ili kuwavutia wawekeze na wafanyabiashara kuwekeza, hatimaye nchi inufaike kwa ajira za raia na mapato kupitia kodi zitakazolipwa na wawekezaji hao.

Utaratibu wa CTI katika utoaji tuzo hizo kwa wazalishaji na kampuni zinazofanya vizuri, ni sehemu ya hamasa kubwa kwa wawekezaji kuendelea na juhudi za uwekezaji, serikali ikitambua na kuthamini kazi kubwa zinazofanywa kuchangia maendeleo ya viwanda na uchumi kwa ujumla.

Waziri Mkuu Majaliwa, anaendelea kusisitiza: "Takwimu zinaonesha kwamba mwaka jana, sekta ya viwanda imetoa ajira rasmi 306,180 ikilinganishwa na ajira 280,899 za mwaka 2017, ikiwa sawa na ongezeko la asilimia tisa.


Distributed via ippmedia

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipomwakilisha Rais John Magufuli, kwenye hoteli ya Serena Dar es Salaam, tarehe 17 mwezi huu, katika utoaji Tuzo za Rais kwa viwanda vilivyofanya vizuri mwaka jana.

> **'Tanzania ya Viwanda' na ya 'Uchumi wa Kati' itafanikiwa kwa wazalishaji na wawekezaji wa sekta ya viwanda kuhakikisha bidhaa wanazozalisha zinakidhi vigezo vya kimataifa.**

Majaliwa anaahidi serikali itaendelea kuchukua hatua zinazostahili, kuwezesha sekta hii zikue haraka na kutoa mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa, hivyo kuchangia kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa wananchi wetu.

Katika maendeleo ya viwanda nchini, wananchi wameweza kupata ajira na kuchangia moja kwa moja katika ukuaji uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.

Lingine analotaja ni kwamba uwepo wa viwanda vipya zaidi ya 4,000 nchini, kumesaidia kupatikana ajira mpya zaidi ya 482,601.

**TUZO ZILIVYO**

Tuzo za Rais za Viwanda, ina azma ya kuongeza hamasa ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi waanzishe viwanda na imefanikiwa kwa kiwango kikubwa, kutokana na ongezeko la viwanda vipya kipitia serikali iliyopo madarakani. Pia, kuna linaloelekezwa kwamba sekta ya viwanda imepata mwamko mkubwa wa kuendelea kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, baada ya kuona dhamira ya serikali kuwajali na hata kuwatunuku tuzo za kutambua kazi kubwa wanazofanya katika kuchagiza maendeleo na ukuaji wa uchumi nchini.

Ni tuzo zinazotoa mwamko na hamasa kwa wawekezaji na wazalishaji, kupongeza ubora wa uzalishaji bidhaa ili kuwezesha kupata soko la uhakika za bidhaa ndani na nje ya nchi.


Katika hafla za tuzo hizo, wazalishaji hupewa msisitizo na hamasa ya kuzalisha bidhaa bora na zenye viwango ili kuliteka soko la bidhaa wanazozizalisha.

'Tanzania ya Viwanda' na ya 'Uchumi wa Kati' itafanikiwa kwa wazalishaji na wawekezaji wa sekta ya viwanda kuhakikisha bidhaa wanazozalisha zinakidhi vigezo vya kimataifa.

Washindi wa tuzo hizo wanatakiwa kuhakikisha wanaendelea kuzalisha bidhaa bora, huku wale ambao hawakupata tuzo hizo wakiongeza bidii katika kuzingatia masharti ya kushinda kwa maendeleo ya viwanda na uchumi.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akimkabidhi tuzo ya ushindi wa jumla, Satbir Singh Hanspaul, Mtendaji Mkuu wa kampuni za Hanspaul, , katika utoaji tuzo za Rais kwa viwanda vilivyofanya vizuri, mwaka jana. Watatu kushoto ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa na kushoto Mwenyekiti wa CTI, Subhash Patel. **PICHA: BLOGU YAMICHUZI.**





Mwakilishi wa Shirika la Global Affair Canada, Stefan Paquette (kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo (wa pili kulia) wakinawa mikono kwenye moja ya vituo vya kunawia vilivyojengwa na Serikali ya Canada kupitia Mradi wa Uzazi Salama Rukwa katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo, juzi, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kupunguza vifo vya mama na mtoto mkoani humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Polisi yanasa maficho ya bodaboda za wizi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

POLISI mkoani Mbeya, inawashikilia watu sita kwa tuhuma za kuhusika na matukio ya wizi na uporaji wa pikipiki katika maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Akizungumza na wanahabari juzi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watuhumiwa hao walikamatwa kufuatia msako uliofanywa na jeshi hilo, sehemu mbalimbali.

Alisema msako huo ulifanyika kwa mfululizo kati ya Oktoba 25 na Oktoba 26 mwaka huu katika Jiji la Mbeya na katika wilaya za Mbarali na Rungwe na kuwanasa watuhumiwa hao wakiwamo waliowezesha uporaji na uhifadhi wa pikipiki hizo.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Solomi Msukwa, maarufu 'Wandonga' (43) mkazi wa Gombe jijini Mbeya anayedaiwa kupokea na kuhifadhi pikipiki zilizoporwa na kikosi hicho kwenye maeneo mbalimbali.

Aliwataja wengine kuwa ni Peter Mwansilu (31) dereva na mkazi wa Airport ya zamani jijini Mbeya, Jackson Mwakasege (41) anayeishi Kiwira Road wilayani Rungwe, Shukuru Mwakibete (41) kutoka Kijiji cha Rusese Igulusi wilayani Mbarali.

Wengine ni Kennedy Mwalukasa (30) kutoka Suma wilayani Rungwe na Martin Simbeye (50) mkazi wa Forest Mpya jijini Mbeya ambaye ni mfanyabiashara. "Tulipowapekua majumbani mwao tulikuta na pikipiki mbalimbali tunazohisi ni za wizi pamoja na vifaa vyake ambavyo vilishatumika na inaonyesha ni vifaa vya pikipiki ambazo huenda waliziiba, lakini wanakiri kuhusika katika matukio 36 ya wizi wa bodaboda," alisema Kamanda Matei. Alieleza watuhumiwa hao walikiri kuhusika na matukio mbalimbali ya kupora bodaboda pamoja na mbinu walizokuwa wanazitumia kwenye matukio hayo.

Kamanda Matei alisema walipofanya upekuzi nyumbani kwa Mwandonga ambaye ni mpokeaji wa pikipiki hizo walizikuta sita pamoja na vifaa mbalimbali vilivyohifadhiwa ndani.

Alivitaja vifaa hivyo kuwa ni taa, ngao, spika, namba za pikipiki, honi, kifaa cha kubebea injini, mikono ya vioo, vifaa vya kufungulia magurudumu pamoja na vipima umeme.

Alisema watuhumiwa wanaendelea kushikiliwa katika kituo cha kati cha polisi na aliwataka wananchi ambao waliwahi kuibiwa pikipiki zao kwenda katika kituo hicho kwa ajili ya utambuzi wa pikipiki hizo.

Aliwataka waendesha pikipiki mkoani humo kuwa makini na vikundi vya wahalifu hasa nyakati za usiku kwa kuepuka kuwabeba watu ambao hawawafahamu na wanaowatilia mashaka.

Alisema upelelezi unaendelea ili kubaini mtandao mzima wa uhalifu na wizi wa pikipiki na kwamba ukishakamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Distributed via inmedia

# Makandarasi wapewa mbinu za kushindana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKANDARASI na wazabuni wazawa kutoka mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wametakiwa kuwa na nidhamu na uadilifu kwenye utekelezaji wa miradi wanayokabidhiwa na serikali ili kumudu ushindani dhidi ya wageni.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Songwe, Mhandisi Yohani Kasaini, wakati wa kongamano la uwezeshaji makandarasi na wazabuni wa mikoa hiyo lililoandaliwa na Benki ya CRDB.

Aliwataka kukamilisha kwa wakati miradi wanayopewa kwani wanapoendelea kuchelewa kukamilisha serikali inakosa imani nao na hivyo kuendelea kuwaamini wageni ambao wanakamilisha kazi kwa wakati.

Alisema mpango wa serikali ni kuhakikisha inawanyanyua makandarasi wazawa ili na wao wakue na kupewa zabuni kubwa lakini inakwama pale inapoona hawana ushirikiano mzuri.

"Tunapogawa zabuni tunawaangalia sana ninyi lakini shida ni kwamba mkishapewa mnachukua muda mrefu sana kumaliza kazi tena inakuwa kama tunaanza upya kuwabembeleza, sasa msipobadilika mtaendelea kuwa wasindikizaji wa Wachina," alisema Mhandisi Kasaini.

Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts, alisema benki hiyo imeanzisha huduma mpya ya kuwawezesha makandarasi kupata mitaji itakayowafanya wajenge na kukamilisha miradi kwa wakati.

Alisema kutokana na huduma hiyo, makandarasi hawana sababu ya kuchelewa kukamilisha miradi wanayopewa na badala yake wakifuata taratibu watakuwa bora kuliko hata wageni wanaoaminiwa kwa sasa.

Alisema makandarasi na wazabuni wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii hasa katika kipindi hiki ambacho serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli inatekeleza miradi mikubwa ya maendeleo.

Alisema kwa sasa kuna shughuli nyingi za ujenzi wa madaraja, ujenzi wa vyumba vya madarasa, hospitali na vituo vya afya, madaraja na majengo mbalimbali.

"Nchi kwa sasa inajenga uchumi wa viwanda ambao unaambatana na kazi nyingi za ujenzi, hivyo makandarasi wana kazi nyingi za kufanya na wakati mwingine wanajikuta mitaji yao haitoshi ndiyo maana tumeanzisha hii huduma ya kuwawezesha," alisema Dk. Witts.

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwataka makandarasi wa mikoa hiyo ya Nyanda za Juu Kusini kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha za miradi ili ikamilike kwa wakati bila ya dosari.

Vilevile aliwataka kuwa na malengo mahususi ya kazi ili waweze kuaminiwa na hatimaye kukopeshwa na taasisi za kifedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi.

# Watishia kuacha kulima pareto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima wa pareto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wametishia kuachana na zao hilo kwa madai kuwa halina faida kama ilivyo kwa mazao mengine ya biashara.

Walidai kuwa wanatumia nguvu kubwa kuzalisha, lakini hakuna soko la uhakika kutokana na wanunuzi kuwa wachache ambao nao wanajipangia bei wanayoitaka isiyo na maslahi kwa wakulima.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti katika Kata za Shigamba na Ilembo, baadhi ya wakulima hao walisema wana mpango wa kuanza kuyabadilisha mashamba wanayoyatumia kuzalisha zao hilo ili kupanda mazao mengine wakitaja miti.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Mwazembe, alisema kwa sasa wana mnunuzi mmoja ambaye ni Pyrethrum Company of Tanzania (PCT) hali ambayo inafanya zao hilo kuuzwa bila ushindani na kufanya wakulima wasipate faida.

"Kuna baadhi wameshaacha kulima na kuanza kupanda miti ya kuni na mbao, mimi mwenyewe naona bora nilime mahindi na alizeti ili yakikosa soko nile na familia yangu kuliko haya masumu ambayo hatuwezi hata kula," alisema Mwazembe.

Petro Shilabi aliiomba serikali kuharakisha ujenzi wa kiwanda katika wilaya hiyo ili soko lipanuke kwa maelezo kuwa wanunuzi wa sasa wanapiga hesabu za usafirishaji kwenda Mafinga mkoani Iringa ambako ndiko kuna kiwanda.

Alisema endapo kiwanda kitajengwa jirani na maeneo yao hata usafirishaji hautakuwa wa gharama kubwa na hivyo kuwafanya wauze kwa bei nzuri itakayotoa hamasa kwa wananchi kuendelea kulima.

"Kwa sasa tunauza Sh. 2,400 kwa kilo, lakini kuna malipo mengine ambayo tunatakiwa tulipwe baada ya wanunuzi kwenda kupima viwango vya sumu, hapo ndipo tunapigwa na kuliwa maana hatushiriki kwenye upimaji huo," alisema Shilabi.

Hivi karibuni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alisema amepatikana mwekezaji ambaye anataka kujenga kiwanda wilayani Mbeya na hivyo akawataka wakulima kuendelea kulima zao hilo.





# Azaki zataka wananchi kutambua mchango wake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASASI za kiraia zimewahakikishia wananchi kuwa zinafanya kazi muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi na kuwataka kuachana na dhana potofu kuwa zina matumizi mabovu ya fedha.

"Kumekuwa na dhana potofu kwamba asasi za kiraia zimekuwa zinapata fedha na hazifanyi matumizi sahihi, naomba hili nilipinge, si zote bali zipo chache ambazo zinaharibu," alisema, Mkurugenzi wa shirika linalojihusisha na masuala ya wanawake(Wowap), Fatuma Toufiq. Fatuma ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum(CCM), alikuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu Wiki ya Azaki itakayoanza jijini Dodoma kuanzia Jumatatu wiki ijayo. Alieleza kuwa kumekuwa na asasi zinazofanya kazi kwenye sekta mbalimbali na zinaonekana kama vile elimu, afya na kilimo.

Aidha, alisema asilimia kubwa ya asasi za kiraia zimekuwa zikifanya kazi ya masuala ya maendeleo tena yanaonekana na kupinga kuwa zimekuwa hazifanyi matumizi yasiyo sahihi ya fedha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Uwezeshaji Asasi za Kiraia(FCS), Francis Kiwanga, alisema Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, atazindua maonyesho ya wiki hiyo kuanzia Novemba 4.

Alisema yatajumuisha zaidi ya asasi za kiraia 500 nchini.

Alisema lengo la maonyesho hayo ni kuimarisha ubia kati ya asasi za kiraia na wadau mbalimbali ili kutimiza azma ya kuiletea Tanzania maendeleo.

Aidha, alisema FCS itatoa tuzo za umahiri wa asasi hizo ili kutambua ufanisi na michango ya taasisi na watu binafsi katika kuchochea uimarishaji na utekelezaji wa sera ya maendeleo Tanzania.

Mwakilishi wa Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali, Charles Komba, alisema asasi hizo zinafanya kazi ambayo ilitakiwa kufanyika na serikali.

"Lakini kama mnavyojua kutokana na ufinyu wa bajeti serikali haiwezi kufanya kila kitu, asasi za kiraia zimekuwa ni wadau wakubwa sana katika kufikisha huduma kwa wananchi," alisema.

Alisema ofisi ya msajili itashiriki kikamilifu kupitia mijadala mbalimbali ili kutoa ufafanuzi wa hoja zitakazokuwapo.


Distributed via ippmedia

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Taifa, Magdalena Sakaya (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma juzi, kuhusu madai ya hujuma wanayofanyiwa wagombea wao na chama tawala kwenye mchakato unaoendelea nchini kote wa uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Taifa, Maftaha Nachuma na Mwenyekiti wa Wabunge wa chama hicho, Mussa Mbaruku. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mikoa kanda ya kati kuongezewa umeme

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme (Tanesco), litaboresha miundombinu na kuongeza ufanisi wa kuwahudumia wateja wa kanda ya kati kwa kukiongezea uwezo kituo cha kupoza umeme cha Dodoma kutoka megawati 48 za sasa hadi 400.

Tanesco kanda ya kati inayohudumia mikoa ya Morogoro, Singida na Dodoma, aidha, imeshaanza kufanya utanuzi wa kituo hicho cha kupoza umeme cha Dodoma.

Kwa mujibu wa Meneja wa Tanesco wa Kanda ya Kati, Mhandisi Atanas Nangali, uboreshaji mwingine wa kituo kipya cha Ifakara mkoani Morogoro, ambacho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 16, huku Singida kitaongezewa uwezo kutoka megawati 32 hadi 400 ni mambo mapya yanayofanyika.

Aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wa kujadili changamoto mbalimbali baina ya Tanesco, wawekezaji na wenye viwanda kutoka mikoa ya kanda ya kati ambayo ya Morogoro, Singida na Dodoma.

Meneja wa Tanesco, Kanda ya Kati alisema wamelazimika kuitisha kikao hicho ili kuangalia njia bora ya kuboresha huduma na kufahamu changamoto zinazowakabili katika kulipa madeni. "Historia ya shirika letu inaonyesha wenye viwanda na wawekezaji wote wakubwa wamekuwa wakichangia zaidi ya asilimia 50 ya pato la Tanesco hivyo kikao hiki ni muhimu kuangalia dhana bora ya kuboresha uhusiano kati yetu na wateja," alisema Nangali.

Awali katika mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alizitaja njia sita za umeme ambazo ni korofi na kulitaka shirika hilo kanda ya kati kuziboresha ili kuwavutia wawekezaji wa viwanda kwenye maeneo hayo. Alisema maeneo hayo kwa mujibu wa Dk. Mahenge ni Mpwapwa, Kongwa, Kibaigwa, Nala, Bahi na Chemba.

Aliwaambia washiriki kuwa maeneo hayo yanapaswa kufanyiwa maboresho ikiwamo kuongezewa uwezo wa utoaji wa huduma ya umeme ili kuwavutia wawekezaji kwenda kuanzisha viwanda.

"Naomba maeneo hayo myafanyie marekebisho lengo ni kuona kila sehemu umeme unawaka ipasavyo na kuondoa kero kwa wateja," alisema Dk. Mahenge.

Aidha, alilitaka shirika hilo kuanzisha kitengo cha huduma ya haraka kwa wateja wakubwa ili kuondoa vikwazo kwa wawekezaji kupata huduma ya umeme kwa haraka.

Dk. Mahenge alisema pamoja na kuwa sera zipo wakati mwingine shirika hilo wanapaswa kwenda mbali zaidi kubuni utaratibu ambao unawawezesha wawekezaji kupata kwa haraka huduma za umeme.

"Naomba ifike wakati mnatazama mbali zaidi, lengo ni kujenga wala sio kubomoa, hivyo ni vema kuwapa kipaumbele wawekezaji ili waanze kutoa huduma ya uwekezaji wa viwanda kwa haraka," alisema Dk. Mahenge.

# Serikali kuwekeza kwenye Tehama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, ameahidi kuwa serikali ya awamu ya tano, itaendelea kuwekeza katika sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) ili kufikia azma ya uchumi wa viwanda.

Aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati alipokuwa akifungua kongomano la nne la mtandao wa jamii katika nchi za Afrika uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom).

Alisema dunia ya sasa suala la teknolojia ya habari na mawasiliano ni jambo lisilokwepeka kwenye kuziwezesha jamii kuzifikia fursa mbalimbali.

"Mawasiliano ni nyenzo muhimu sana serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuimarisha mawasiliano kwa wote hadi kule ambako bado wananchi hawajafikiwa hasa maeneo ya vijijini," aliahidi Prof. Ndalichako.

Pia alisema kuwa sekta ya mawasiliano nchini imeendelea kukua kila siku na imekuwa ya pili kati ya zile zilizochangia katika ukuaji wa uchumi wa taifa.

Ndalichako aliwataka washiriki wa kongamano hilo kutumia fursa hiyo pia kufanya tathmini ya ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini na katika Bara la Afrika kwa ujumla.

"Nawaombeni mtumie kongamano hili pia katika kutathimini ukuaji wa mawasiliano nchini, barani Afrika lakini pia hata dunia kwa ujumla ili kuweza kuona ni vipi tunaweza kuwafikia wale ambao bado hawajafikiwa kwa haraka katika maeneo ya vijijini," alisema Waziri Ndalichako.

Aidha, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Profesa Faustine Bee, alisema mkutano huo umehusisha washiriki kutoka katika maeneo mbalimbali duniani.

Alisema kongamano hilo ni la nne na Tanzania imepewa wenyeji mwaka huu ambapo washiriki kutoka nchi za Kenya, Uganda, Cameroon, Liberia, Ghana pamoja na Uhispania wanahudhuria.

Alisema lengo la kongamano hilo ni kupeleka huduma kwa jamii kupitia mfumo wa mawasiliano kwa kutumia mawimbi ya televisheni ambayo yatazifikia taasisi zote za serikali zikiwamo shule katika maeneo yasiyofikiwa na huduma ya mtandao wa intaneti ifikapo 2025.



# Wadau wachangia samani mbalimbali

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TAASISI ya Muzdalifa kwa kushirikiana na Shirika la HHRD la Marekani wamekabidhi vifaa vya elimu kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, kwa ajili ya kuendeleza sekta ya elimu nchini.

Akipokea msaada wa viti na meza, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema kutolewa kwa samani hizo kutapunguza tatizo hilo kwa baadhi ya shule.

Alisema taasisi za kiraia zimekuwa na mchango mkubwa wa kusaidia sekta za kijamii ikiwamo elimu, hatua ambayo inapunguza changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi na taifa.

Aidha, Mohamoud, alisema msaada huo utasaidia kwa kiasi kikubwa kuchangia maendeleo yanayotokana na kodi zinazotolewa na wananchi kupita serikali za mitaa.

"Msaada huu utasaidia kodi za wananchi wetu kutumika katika shughuli nyingine tofauti za maendeleo kwa hiyo kupatikana kwake kutapeleka mbele maendeleo ya mkoa wetu," alisema Mahmoud.

Alizitaka taasisi hizo kuendelea kusaidia maendeleo ya mkoa huo ili kuona wananchi wanaimarika kiuchumi hadi taifa zima.

Mapema Katibu wa Jumuiya ya Muzdalifa, Farouk Hamad na wawakilishi wa Taasisi ya HHRD Tanzania, Hassan Kibwebwe, walieleza kuwa misada hiyo ni kwa ajili ya kuunga mkono jitihada zinazo fanywa na Rais wa Zanzibar, Ali Mohamed Shein za kuinua sekta ya elimu nchini pamoja na kuishukuru serikali kwa kuwaondolea kodi kwenye makontena waliyochukulia mizigo ya misaada.

Wakitoa shukrani kwa niaba ya wananchi wa wilaya mbili za Kusini na Kati, Mkuu wa Wilaya ya Kati, Hamida Mussa Khamis, alisema msaada huo utapunguza changamoto walizokuwanazo awali katika shule za wilaya hizo.

Makabidhiano ya vifaa hivyo yalifanyika katika ofisi za Mkoa wa Kusini Unguja ambapo viti 79 na meza 69 zimekabidhiwa kwa ajili ya kusaidia shule za mkoa huo, hafla hiyo ilihudhuriwa na wakuu wa wilaya na makatibu tawala wa mkoa huo na maofisa mbalimbali.

# Wafunzwa umuhimu hatimiliki za ardhi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WANAWAKE wameonywa kuacha kununua ardhi kiholela na kuhimizwa kuwa makini na kutafuta hatimiliki ili kuepuka uwezekano wa kuingia kwenye migogoro ya kunyang'anywa rasilimali hiyo.

Hayo yalielezwa na Ofisa Ardhi wa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar, Haji Mrisho Haji, wakati akizungumza na wananchi wa shehia ya Mpapa Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja, kuhusu umuhimu wa kuwa na hatimiliki ya ardhi hususani kwa wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema baadhi ya jamiii ya wanawake hawaona umuhimu wa kuwa na hatimiliki ya ardhi wanazozinunua au wanazoziendeshea shughuli mbalimbali za kilimo na hata makazi jambo linalopelekea baadaye kudhulumiwa kwa urahisi.

Alisema ni vyema wakawa na elimu ya umiliki wa ardhi ambayo itawasaidia kuepuka migogoro hiyo iliyopo katika maeneo ya vijijini, huku migogoro mikubwa ikiwa katika mashamba yanayotumiwa kwa kilimo.

"Wanawake wengi wanadhulumiwa ardhi zao kwa kuwa hawana elimu kuhusu umiliki wa radhi na hii inasababisha hata wanawake kushindwa kufikia azma ya kuwa na maendeleo kutokana na kurudishwa nyuma mara kwa mara ," alisema.

Aidha, Haji aliwafahamisha kuwa asilimia kubwa ya wanawake ndiyo washiriki katika shughuli za uzalishaji mali zinazotokana na kilimo, lakini cha kushangaza wanawake wanaomiliki ardhi kihalali ni wachache mno. Kwa upande wake Katibu wa Mtandao wa Ardhi Wilaya ya Kati, Bahati Issa, alisema wanawake walio wengi wanakosa haki zao za msingi ikiwamo umiliki wa ardhi unaochangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumo dume uliopo katika maeneo yao

Alisema wanawake wanadhulumiwa ardhi hizo na wanaume pale wanapoachana na baadhi yao zikiwa mali za urithi wa wazazi wao au mume anapofariki jambo linalosababisha kushindwa kuendeleza shughuli zao za kujiletea maendeleo.

Alisema Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) Zanzibar, kimekuwa kikitoa elimu hususan wanawake na wenye ulemavu ili kujua namna ya umiliki wa ardhi kisheria na kuepuka migogoro iliyopo na inayoweza kutokea.

Aidha, akizitaja baadhi ya sababu ambazo zinapelekea wanawake kudhulumiwa ardhi katika baadhi ya maeneo alisema mila na tamuduni ndicho kikwazo kinachomfanya mwanamke kukosa fursa ya kumiliki ardhi kwa kudhani kuwa jukumu la kulinda mali ni la mwanaume pekee.

Alisema sababu nyingine ni wanawake kuhama hama makazi iwe kwa kuolewa au kuvunjika kwa ndoa hali inayopelekea kudhulumiwa ardhi waliyoiacha.

Hata hivyo, Tamwa Zanzibar, imekuwa chachu ya kuwakusanya wajasiriamali wanawake kwa kuwapatia elimu ya ujasirimali wa kutengeneza bidhaa mbalimbali ili kupata pesa za kufuatilia umiliki wa ardhi kisheria




Ofisa mradi wa kutokomeza ukatili kwenye masoko ya Manispaa ya Shinyanga Mjini, Helena Daudi (kushoto), akizungumza na madiwani wa manispaa hiyo, juzi, kuhusu kampeni ya "Mpe Riziki si Matusi" inavyofanya kazi ya kutokomeza ukatili dhidi ya wafanyabiashara wanawake na wasichana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ataka wadau kusaidia elimu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, ameziomba Taasisi za Dubai Care pamoja na Milele Foundation kuendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu ili kuinyanyua sekta hiyo muhimu kwa maendeleo.

Naibu Waziri aliyasema hayo huko ofisini kwake Mazizini na kuongeza kuwa asasi zina mchango mkubwa wa kutoa ushirikiano na Wizara ya Elimu ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazozikumba shule na wanafunzi.

Alisema taasisi binafsi zimekuwa zikisaidia shule na wizara kupitia miradi mbalimbali ikiwamo vifaa na kuhamasisha wanafunzi kuona umuhimu wa kuzingatia masomo yao kwa maendeleo ya baadaye.

Aidha, katika mazungumzo yao na Naibu Waziri, alizishukuru taasisi hizo kwa kuendelea kutoa mchango katika sekta hizo na kutimiza lengo la kuiona Zanzibar ikizidi kufanya vizuri katika sekta ya elimu.

"Suala la kukua kwa elimu na kuhakikisha wanafunzi wanafanya vizuri linahitaji ushirikiano wetu sote. Hamasa kwa wanafunzi, walimu na hata upatikanaji wa vifaa vya kusomeshwa kwa wakati..." alisema Naibu Waziri.

Meneja wa Miradi wa Taasisi ya Dubai Care, Saeed Alismaily, alisema wameamua kuiunga mkono Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, katika suala zima la marekebisho ya mtaala wa maandalizi na msingi unaoendelea hivi sasa.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuinua kiwango cha elimu Zanzibar kwa kuanzia ngazi za chini katika madarasa yale ya msingi ili mwanafunzi hata akifika katika madarasa ya juu tayari alishajengewa msingi imara wa elimu tangu akiwa chini.

Aidha, kwa upande wa Meneja wa Miradi wa Milele Foundation, Khadija Shariff, alisema taasisi yao imekuwa ikiunga mkono Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, katika sekta mbalimbali ikiwamo huduma za afya, majisafi na salama na elimu, ambapo ameahidi kuendelea kutoa huduma hizo ili kuleta maendeleo Zanzibar kwa kutoa elimu bora itakayomnufaisha mtoto akimaliza masomo yake hapo baadaye.

# Sekta ya korosho yapata fursa

**Na Mwandishi Wetu**

KILIMO cha korosho kimepata fursa baada ya kuandaliwa mpango wa ukuaji na uboreshaji wa huduma za kibenki kwa wadau wa zao hilo.

Katika utekelezaji wa mpango huo, wadau wa kilimo hicho wamekutanishwa mkoani Mtwara ili kupata wasaa wa kujadili fursa mbalimbali za kibiashara.

Wadau hao walikutanishwa na Benki ya Exim Tanzania mapema wiki hii katika hafla ya chakula maalum kwa ajili ya wadau mbalimbali wa zao la korosho mkoani Mtwara.

Akizungumza kwenye hafla hiyo iliyohudhuriwa na wadau mbalimbali wa zao la korosho wakiwamo viongozi wa kiserikali, wafanyabiashara wakubwa na wadogo pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo, Mkuu wa huduma ya rejareja wa benki ya hiyo,

Andrew Lyimo, alisema kupitia hafla hiyo walilenga pia kutoa fursa miongoni mwa wateja hao ili waweze kufahamiana na kufungua wigo wa kufanya biashara pamoja.

"Pamoja na kushukuru kwa namna ambayo wateja wetu wamekuwa nasi hadi kufikia mafanikio ya ukuaji na ubora wa huduma zetu, hafla hii inatoa fursa kwa wateja wetu pia kufahamiana wao kwa wao na hivyo kufungua milango ya fursa baina yao," alisema Lyimo.

Alisema ukuaji wa benki hiyo unaoshuhudiwa kwasasa ni matokeo ya ushirikiano baina yake na wateja wake ambao kwa kiasi kikubwa wameonyesha imani kubwa kwa benki hiyo hali ambayo imekuwa ikiiwezesha benki hiyo kubuni huduma bora na rafiki za kibenki ili kulinda na kurejesha imani hiyo kwa wateja wa benki hiyo.

Pamoja na mambo mengine hafla hiyo ilipambwa na shuhuda mbalimbali kuhusu ubora wa huduma za benki hiyo kutoka kwa wadau hao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Emanuel Mwaigobeko, alisema mkoa huo umejipanga kwa dhati kuhakikisha ununuzi wa mkorosho unaenda vyema kwa kuzuia watu wachache kuharibu taswira ya serikali pamoja na sekta nzima ya kilimo cha zao hilo.

Mwaigobeko alizitaka taasisi zinazohusika na masuala ya fedha mkoani humo kusaidia katika kuwajengea uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya kifedha wakulima na wafanyabiashara wa zao hilo mkoani humo.

Alisema ni matarajio yake kwamba wakulima watakuwa waaminifu kupeleka korosho safi ili wasiharibu ubora wa korosho za Tanzania katika soko la ndani na nje.




Mkuu wa Bidhaa na Huduma za Tigo, David Umoh, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa uzinduzi wa simu yenye sifa za smartphone 'Kitochi 4G Smart' yenye uwezo wa 4G kwa bei nafuu. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, Tarik Boudiaf. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utendaji kazi wa Osha wakuna wenye viwanda

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), limesema limeridhishwa na utendaji kazi wa Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (Osha), kwa kuanza kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya biashara (blue print).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Makamu Mwenyekiti wa pili wa CTI, Shabbir Zavery, alisema kwa sasa kuna maboresho makubwa katika utendaji kazi wa Osha kwa wamiliki wa viwanda kutofautisha na miaka ya nyuma.

"Osha wameanza kutekeleza blue print, kwa sasa utendaji wao uko sawa, kuna maboresho makubwa, baadhi ya tozo kama tano wameziondoa ambazo zilikuwa kero," alisema Zavery.

Alisema wajumbe wa CTI walikutana na kujadiliana baadhi ya masuala na wakaamua kuwaalika Osha kwenye mkutano ili kufahamu zaidi utendaji wao, pamoja na wao kueleza baadhi ya kero ambazo bado zipo.

Naye Meneja wa Afya kutoka Osha, Jerome Materu, alisema wamekuwa wakifanya kazi kwa lengo la kumsaidia mmiliki wa kiwanda na siyo kumkomoa.

Alisema licha ya serikali kuagiza kupunguzwa kwa baadhi ya tozo ambazo zilikuwa kero kwa wafanyabiashara, wao waliamua kuzifuta kabisa.

Materu alizitaja baadhi ya tozo ni Sh. 500,000 kwa ajili ya vifaa vya kuzimia moto na zimamoto, kwamba mwekezaji au mwenye kiwanda alikuwa anatozwa mara mbili.

Alisema tozo nyingine ni gharama ya cheti ambayo mwekezaji alikuwa anatozwa na kwamba Osha walikuwa wanamtoza mwekezaji kiasi cha fedha kwa ajili ya kupata cheti cha ukaguzi.

Alisema Osha imeanza kutekeleza kwa asilimia 100 yaliyomo kwenye blue print, kama vile muda wa upatikanaji wa leseni umepungua kutoka saa moja hadi nusu saa, na usajili ni bure.

Alisema Osha inaunga mkono juhudi za serikali za kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara, hivyo wamedhamiria kuwa taasisi iliyo bora na siyo adui kwa wafanyabiashara.

# Canada yapiga jeki sekta ya afya

**Na Nebart Msokwa,** SUMBAWANGA

SERIKALI ya Canada kupitia Shirika lake la Maendeleo (Global Affairs Canada), imekarabati miundombinu ya maji katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Rukwa na vituo viwili vya afya kisha kiikabidhi serikali kwa ajili ya kupambana na vifo vitokanavyo na uzazi.

Aidha, imekabidhi mashine maalumu za kupimia wingi wa damu kwa kinamama wajawazito na mashine za kuongeza joto kwenye vyumba vya kuhifadhia watoto waliozaliwa na uzito pungufu ili kuokoa maisha yao.

Ukarabati wa vituo hivyo umetekelezwa na Serikali ya Canada kupitia Mradi wake wa Uzazi Salama Rukwa ambao unatekelezwa na mashirika matatu ambayo ni Plan International, Africare na Jhpiego.

Akizungumza juzi katika ukumbi wa Hospitali ya Mkoa ya Rufani ya Rukwa wakati wa kukabidhi miradi hiyo pamoja na vifaa, Mkurugenzi wa Mradi wa Uzazi Salama, Gasper Materu alisema ukarabati wa miundombinu hiyo ya maji umegharimu zaidi ya Sh. milioni 542.

Materu alivitaja vituo vya afya vilivyonufaika na mradi huo ni cha Milepa kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Kituo cha Afya cha Matai katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

Alisema mashine za kuongeza joto kwenye vyumba vya kulelea watoto waliozaliwa na uzito pungufu na za kupimia wingi wa damu kwa wanawake wajawazito, zilinunuliwa kwa zaidi ya Sh. milioni 226 na kwamba zitagawiwa kwenye halmashauri zote za mkoa huo.

"Hii ni ahadi yetu ambayo tuliahidi kushirikiana na serikali kuimarisha huduma za mama na mtoto, baadhi ya huduma hasa za upasuaji zinatakiwa maji ya kutosha na safi, lakini pia watoto wanaozaliwa na uzito pungufu wanahitaji mashine hizi," alisema Materu.

Akikabidhi miradi hiyo pamoja na vifaa kwa niaba ya Serikali ya Canada, Mwakilishi wa Shirika la Global Affair Canada, Stefan Paquette, alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi washirika wa Canada na ndio maana wameamua kusaidia katika afya ya uzazi.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa mataifa yanayopokea misaada mikubwa kutoka Canada kwa ajili ya masuala ya afya ya uzazi ambapo alisema tangu mwaka 2010 mpaka sasa wametoa misaada isiyopungua dola milioni 292.

"Mpango wa Tanzania wa mwaka 2008 mpaka 2015 ulikuwa ni kupunguza vifo vya mama na mtoto ambapo nguvu kubwa iliwekezwa kupambana na hali hiyo hivyo mpango huo unatakiwa kuendelezwa hasa katika maeneo ya vijijini ambako huduma nyingi hazifiki," alisema Paquette.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, aliishukuru Canada kwa msaada huo akisema utasaidia mkoa wake kupunguza vifo vya mama na mtoto ambalo ni tatizo kubwa katika mkoa huo.

Alisema Mradi wa Uzazi Salama ambao umetekeleza miradi hiyo pia unashirikiana na Serikali ya Mkoa huo kwenye mapambano ya mimba za utotoni hasa kwa wanafunzi ambazo hivi karibuni Rais John Magufuli alikemea vikali.

"Nimekuwa nikipokea taarifa za utekelezaji wa miradi hii kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa akinieleza shughuli mnazofanya, nafurahi leo mnatukabidhi miradi hii pamoja na vifaa hivi, tunaomba ndugu zetu Wakanada msichoke kuendelea kutusaidia," alisema Wangabo.

# Fimbo za mwalimu zaua mwanafunzi

**BUJUMBURA, Burundi**

MWANAFUNZI mwenye umri wa miaka 14 nchini Burundi, amefariki dunia baada ya kupigwa viboko kadhaa na mwalimu wake, baba wa mtoto huyo ameiambia BBC.

Mtoto huyo, Chadia Nishimwe, alipigwa viboko shingoni na miguuni , kipigo ambacho kilimpelekea kutokwa damu puani na masikioni hadi kupoteza maisha, alisema Jean-Marie Misago.

"Alikufa darasani mara baada ya kupigwa na mwalimu wake na wakaenda kumtelekeza katika ofisi ya mwalimu mkuu," Misago aliongeza.

Mkuu wa Shule alijaribu kumuwahisha hospitalini mtoto huyo wakati huo, alikuwa ameshakufa tayari, aliongeza baba huyo.

BBC ilitafuta taarifa zaidi katika sekta ya elimu bila mafanikio.

Mtoto huyo aliuawa Jumanne wiki hii na kuzikwa siku hiyo hiyo.

Nchini Burundi, adhabu ya wanafunzi kuchapwa viboko ni kinyume na sheria ingawa bado wanafunzi wanachapwa.

Tukio kama hilo la mwalimu kumuua mwanafunzi lilitokea nchini Tanzania mwaka 2018 ambapo mwanafunzi mmoja wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Kibeta, Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, alidaiwa kupigwa na mwalimu wake mpaka kufariki kwa tuhuma ya kuiba mkoba.

Mara baada ya tukio hilo Waziri wa Elimu, Profesa Joyce Ndalichako, aliwataka watu wawe watulivu hadi upelelezi wa tukio hilo utakapomalizika.

"Shule ni sehemu salama sasa isitokee mtu akaondoa hiyo dhana, hiyo ni bahati mbaya iliyotokea na isitafsiriwe kuwa shule sio mahali salama, serikali itawashughulikia wale wote ambao wanahatarisha amani na usalama"Waziri Ndalichako alieleza wakati huo.

**BBC**

**Tukio kama hilo la mwalimu kumuua mwanafunzi lilitokea nchini Tanzania mwaka 2018 ambapo mwanafunzi mmoja wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Kibeta, Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, alidaiwa kupigwa na mwalimu wake mpaka kufariki kwa tuhuma ya kuiba mkoba.**

# UN yaonya kuhusu machafuko ya Kivu

**KINSHASA, Congo**

UMOJA wa Mataifa (UN) umewaonya wahusika kuhusu mgogoro wa kikabila unaoendelea katika eneo la Fizi lililoko katika jimbo la Kivu Kusini, nchini Congo.

UN imetahadharisha kuhusu machafuko ya kikabila ambayo yanaweza kutokea katika eneo la Fizi jimboni Kivu ya Kusini ambako makundi ya wapiganaji wa kikabila yameendesha mashambulizi kwa zaidi ya miezi sita sasa.

Akiwa kwenye mkutano na waandishi habari hapa jijini Kinshasa, kiongozi wa Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa nchini Kongo, Abdoulaziz Thioye alisema kwamba hali ya kiusalama kwenye mtaa wa Fizi, huko Kivu ya Kusini, ni lazima iboreshwe haraka iwezekanavyo.

Thioye alisema miito kwa ajili ya kuchochea chuki za kikabila inahatarisha amani kwenye eneo hilo.

"Machafuko hayo ambayo yametokea huko Minembwe tangu Machi mwaka huu, yanaonyesha kuna maneno ya uchochezi wa chuki yanaoripotiwa baina ya jamii zinazohasimia. Tumeshuhudia pia chuki za kikabila na hata uraia wa Kongo, hali hiyo inaleta tatizo. Kuna umuhimu wa kurejesha kila mtu kwenye njia ya busara, wakiwamo wale wanaochochea kisirisiri machafuko hayo...," alisema Thioye.

Umoja wa Mataifa ulielezea kwamba zaidi ya vijiji 73 vimechomwa moto na makundi ya wapiganaji wa kikabila. Huku vijiji vingine vinne ambavyo ni vya jamii ya kabila la Benyamulenge vikiharibiwa pia.

"Tumewakumbusha wote kwamba uchochezi wa chuki za kikabila ni makosa ambayo mahakama ya kimataifa inaweza kuhukumu, na wale wanaohusika na machafuko hayo watafuatiliwa na mahakama ya kitaifa ama kimataifa. Tuna uwezo wa kuchunguza vyanzo vya machafuko hayo na vilevile kubainisha wale wanaosambaza ujumbe wa chuki za kikabila. "

Vijiji kadhaa vya mtaa wa Fizi, vikiwamo Minembwe, Bijombo na Lulenge vinakabiliwa na machafuko hayo ambayo UN inaelezea kwamba ni kutokana na misingi ya kikabila.

Kila jamii ina wanamgambo wake na makabila yanayoishi kwenye maeneo hayo ni pamoja na wa Babembe, Benyamulenge, Banyindu, Bafuliru,Bavira na Banyindu.

Wazaliwa wa Kivu ya Kusini wanaoishi mjini Kinshasa,wameanzisha juhudi za upatanishi ili kumalizisha machafuko hayo.

Norbert Basengezi, aliyeanzisha mazungumzo ya makundi ya kikabila kutoka mtaa wa Fizi, alisema juhudi za mazungumzo zimekwama kutokana na misimamo mikali ya baadhi ya viongozi wa makabila hayo.

Umoja wa Mataifa ulisema kwamba mbali na juhudi za mazungumzo ni lazima jeshi kuingilia kati na kurejesha mamlaka ya kitaifa.

**DW**



Wakimbizi kutoka Congo waliokimbia makazi yao kwasababu ya machafuko. **PICHA: AFP.**

# Waandishi wauguza majeraha ya risasi

**KAMPALA, Uganda**

WAANDISHI wa habari nchini Uganda wametangaza kususia mikutano na taarifa za habari vya polisi kupinga kile wanachokitaja kuwa ni mwenendo wa kuwashambulia wanahabari wakiwa kazini.

Picha zinazoonyesha majeraha makubwa waliyopata waandishi habari watatu wakati walipokuwa wakifuatilia mapambano kati ya polisi na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Makerere zimeibua hasira miongoni mwa wandishi habari nchini humo.

Wandishi hao wana vidonda na michubuko ambayo madaktari wamelezea kuwa itahitaji matibabu ya hali ya juu ikiwamo upasuaji.

Huku waandishi habari hao wakiwa wamelazwa hospitalini, wenzao wameamua kususia vikao vya polisi vinavyoitishwa kila mara kwenye makao makuu ya jeshi hilo pamoja na vituo vingine vya polisi. Rais wa chama cha wanahabari UJA Bashir Kazibwe, alisema.

Kwa upande wao polisi wamekanusha madai kuwa askari wake walikusudia kuwashambulia wanahabari. Waliwalaumu wanahabari kwa kutojiweka maeneo salama wakati wa makabiliano na wanafunzi.

Lakini waandishi wa habari waliojeruhiwa wanasisitiza kuwa jinsi walivyoshambuliwa ni wazi kwamba polisi hawakutaka watekeleze kazi zao katika mazingira hayo ili kuonyesha hali halisi ya mambo.

Kwa mfano walisema bomu moja la kutoa machozi lilimlipukia mmoja wao mapajani na kumjeruhi.

Wabunge nchini humo walishutumu vitendo hivyo kwa kusema kuwa katika kipindi cha wiki mbili ambapo ghasia za wanafunzi zimedumu, waandishi habari walinyanyaswa kwa namna mbalimbali. Baadhi walikamatwa na kulazimishwa kufuta picha walizopiga na zile za video walizorekodi.

Vitendo hivyo ndivyo wanahabari wanaelezea kuwa ni hila za polisi kuwakosesha kufanya kazi yao ya kupasha jamii habari kuhusu hali halisi.

Huku mgomo wa wandishi habari dhidi ya polisi ukianza kufanyika kuanzia jana , wadau wengine katika taaluma hiyo wamehimizwa kutowasaliti wenzao kwa kuitikia na kuhudhuria shughuli na vikao vya polisi.

Aidha, waandishi habari watafanya maandamano ya amani wiki ijayo wakielekea bungeni watakakowasilisha malalamiko yao kwa Spika wa Bunge. Aidha, walieleza kuwa watawasilisha malalamiko kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, ni kwa mujibu wa Bashir Kazibwe wa Chama cha Waandishi cha UJA.

Alisema angalau hali ni tulivu katika chuo kikuu cha Makerere lakini polisi wameendelea kuweka doria na hakuna mwanahabari anayeruhusiwa kuingia chuoni hapo.

**DW.**

# Upepo waezua nyumba Ruvuma, Katavi

**Na Waandishi Wetu**

UPEPO mkali ulioambatana na mvua ya wastani umeezua nyumba sita na vibanda vya biashara sita katika Kijiji cha Mgombasi, Kata ya Mgombasi wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma.

Kaimu Mhandisi wa Wilaya hiyo, Amon Ngonyani, alisema nyumba zilizoezuliwa zilijengwa chini ya kiwango na wahusika hawakuzingatia tahadhari ya upepo mkali kwa kufunga tengo kwenye kenchi.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Sophia Kizigo, aliiagiza kamati ya maafa ya wilaya kufanya tathmini ya uharibifu wa nyumba hizo na taarifa ziwasilishwe ofisini kwake.

Mwenyekiti wa kamati ya maafa ya wilaya hiyo, Enock Nduguru, alisema upepo huo haukusababisha kifo.

Ndunguru aliwataja walioezuliwa nyumba zao za kuishi ni Issa Nkule (60), Aina Kaboma (50), Maljani Hega (30), Mohamed Moyo (60), Walivyo Manamba (25) na Tafuta Hashimu (35).

Diwani wa Mgombasi, Mrisho Mbawala, aliwataka wananchi kupanda miti ili kuzuia upepo katika maeneo yao.

Wilayani Tanganyika mkoani Katavi, nako nyumba 19 zimeezuliwa na upepo katika Kijiji cha Mchakamchaka, huku mtoto akiripotiwa kujeruhiwa.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, John Mpina, alisema jana kuwa upepo huo ulioambatana na mvua ya mawe, ulivuma juzi majira ya 12 jioni.

Alisema wakazi wa kijiji hicho ambao nyumba zao zimeezuliwa, kwa sasa wanahifadhiwa kwa majirani zao na wanahitaji msaada wa haraka.

Paul Kavinza, mmoja wa watu ambao nyumba zao zimeezuliwa, alisema wanaomba halmashauri iwasaidie kutokana na nyumba zao kuharibiwa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Salehe Muhando, alisema serikali inajipanga kuona namna nzuri ya kuwasaidia watu hao.

*Imeandikwa na Gurian Adolf (KATAVI) na Stevie Chindiye (NAMTUMBO)



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mtwara-Mikindani, Emanuel Mwaigobeko, akizungumza wakati wa hafla ya chakula cha jioni kwa ajili ya wadau wa zao la korosho mkoani Mtwara kwa ajili ya kupata wasaa wa kujadili fursa za kibiashara. Wadau hao walikutanishwa na Benki ya Exim Tanzania mapema wiki hii. **MPIGAPICHA WETU**

# Jiji Dodoma latangaza neema viwanja 9,000

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, ametangaza neema ya viwanja zaidi ya 9,000 kwa ajili ya uwekezaji pamoja na makazi katika maeneo mbalimbali kwa gharama nafuu.

Aidha, fursa hiyo inakuja ili kuwezesha kila mtu kushiriki katika kuujenda mji huo kufuatia ujio rasmi wa makao makuu ya serikali ya Jiji la Dodoma.

Akizungumza na vyombo vya habari jijini hapa, Kunambi, alisema lengo la jiji hilo ni kumwezesha kila mtu kuwa na kiwanja kilichopimwa ambacho atakiendeleza kwa ajili ya ujenzi wa makazi au viwanda katika kufikia uchumi wa viwanda ifikapo 2025.

Kunambi alisema viwanja ambavyo wamepanga kuviuza vipo katika maeneo mbalimbali ya jiji ambapo kila mwananchi atakuwa na uwezo wa kumiliki kutokana na gharama nafuu ambazo wamezipanga.

"Lengo letu ni kumwezesha kila mwanachi kumiliki kiwanja chake mwenyewe, ndiyo maana katika viwanja hivi ambavyo tumepima tumeweka bei za wanyonge za kuanzia Sh. 3,000 kwa mita moja ya mraba," alisema Kunambi.

Alisema viwanja hivyo vimeanza kuuzwa kwa watu mbalimbali kuanzia Oktoba 30, mwaka huu na kuendelea katika ofisi za zamani za jiji kuanzia saa 2, asubuhi katika siku za kazi.

"Viwanja hivi ni kwa watu wote kwa ajili ya makazi pamoja na uwekezaji ambapo malipo yake yatafanyika ndani ya miezi mitatu baada ya mteja kukabidhiwa hati ya malipo," alisema Kunambi.

Aliyataja maeneo ambayo viwanja hivyo vimepimwa ni Nala, Chahwa, Ipala, Mapinduzi, Vikonje pamoja na Mtumba ambavyo vyote ni kwa ajili ya makazi na biashara.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Upimaji Ardhi jijini hapa ya Land Network, Samweli Kwabe, alisema viwanja hivyo ambavyo vinauzwa vimelenga makundi yote.

"Watu washindwe wenyewe, lakini jiji limeweka usawa kwa watu wote kila aina ya kiwanja kipo na kwa bei ambayo mtu mwenyewe anaweza kuimudu labda atake mwenyewe kukosa," alisema Kwabe.

## Tigo yazindua 'Kitochi 4G Smart'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Simu ya Tigo, jana imezindua simu yenye sifa za 'smartphone' 'Kitochi 4G Smart' ya kwanza kwenye soko la simu Tanzania yenye uwezo wa intaneti ya 4G kwa Watanzania wote ili kufungua fursa za kijamii na kiuchumi.

Simu hiyo inayojulikana kama 'Kitochi 4G Smart' iko sokoni kwa Sh. 49,000 na inapakua mitandao ya WhatsApp, Facebook, Twitter na Youtube.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa simu hiyo, Ofisa Mkuu wa Biashara wa Tigo, Tarik Boudiaf, alisema "Kama waanzilishi wa kwanza wa mtandao wa kasi wa 4G hapa nchini tangu mwaka 2014, tunavunja mipaka tena kwa kuhakikisha kila mmoja anapata simu ya 4G kwa gharama nafuu ili kuwa sehemu ya mabadiliko ya kidigitali na hatimaye kuchangia ujumuishwaji wa kidigitali hapa nchini," alisema Boudiaf.

Boudiaf aliongeza kuwa kwa muda mrefu gharama kubwa ya simu zenye uwezo wa 4G imekuwa kikwazo kwa Watanzania wengi kumiliki simu zenye uwezo wa intaneti ya kasi hivyo ujio wa simu hiyo ni msaada kwa wengi.

"Kwa ujio wa simu hii ya 'Kitochi 4G Smart' kwenye soko yenye uwezo wa Facebook ya bure kwa miezi mitatu itawapa wateja wetu uwezo wa kujumuika kwenye mitandao na hivyo kufanya kila mmoja kuwa sehemu ya mageuzi ya kidigitali," alisema.

Naye Mkuu wa Bidhaa na Huduma wa Tigo, David Umoh, alisema "Kitochi 4G Smart|", inadhihirisha dhamira ya Tigo ya kuwahudumia wateja wake katika kila hatua ya maisha. Kwa hatua hii ni imani yetu kuwa hakuna mtu ambaye atashindwa kupata manufaa yatokanayo na intaneti ya kasi ya 4G."

"Kitochi 4G Smart" itaongeza wigo wa upatikanaji wa intaneti ya 4G kwa Watanzania wote na kusaidia katika ufikiwaji wa taarifa na maarifa yatakayosaidia katika kutumia vyema fursa za kijamii na kiuchumi."

Tigo inapanua wigo wa uvumbuzi kwa kuendelea kutoa bidhaa na huduma zenye kukidhi mahitaji ya wateja sokoni na zaidi kuchangia mageuzi ya kidigitali nchini. Kitochi 4G Smart ni hatua nyingine kutoka Tigo baada ya Smartphone ya Kiswahili, Facebook ya bure, App ya Tigo Pesa na App ya Tigo.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**LAND CRUISER INAUZWA TOYOTA LANDCRUISER VX AMAZON, DIESEL, AUTOMATIC, INATEMBEA IPO KWENYE HALI NZURI. TSHS 24.5 Milioni. 0719 774 474.**

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA**

Shamba la Ekari 13 linauzwa liko Mlandizi barabara iendayo Bagamoyo, lina miti ya matunda inayozaa, lina umeme. Lina maji ya DAWASCO na maji ni matamu. Pia kuna kisima kirefu. Kwa mawasiliano piga simu namba 0655 099825 / 0767 237404 / 0715 237404.



## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA

BEI NAFUU SANA


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS
IMMIGRATION DEPARTMENT

**APPLICATION FOR TANZANIA CITIZENSHI**




LUKIA MAKA NAGADIA whose photograph provided above, is applying to the Minister of Home Affairs for Tanzania Citizenship. Her Nationality at present is UGANDAN. Country of origin UGANDA. Employment: HOUSE WIFE. She has been living in Tanzania since 2010. Any person who knows any reason why Citizenship should not be granted to the applicant, should send a written and signed statement of facts to the Principal Commissioner of Immigration Services, P.O. BOX 512, Dar es salaam. Use reference DN. 609512.

MSILLO MGAZA

FOR: COMMISSIONER GENERAL OF IMMIGRATION

## KUPOTEA KWA CHETI



**DEVIS MUTA KAGARUKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0800-0073** kilichotolewa na LOYOLA HIGH SCHOOL mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/430473/2019.**

115492902

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA MADAI NAMBA: 70..2019
Mdai: HADIJA MOSES SADIKI
DHIDI YA

Mdaiwa: MAJALIWA JOHN MKOMBOZI

Kwa:
MAJALIWA JOHN MKOMBOZI

Ombi la Mdai:
HADIJA MOSES SADIKI
Madai ya: PESA SHILINGI 3,852,500/=

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 22 mwezi 11 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 31 mwezi 10 mwaka 2019.

115494002

## DEED POLL

By this deed, I the undersigned **ERICK BUBERWA EMANUEL** formerly known as **ERICK BUBERWA IJUMBA** do hereby absolutely renounce and abandon the said named of **ERICK BUBERWA IJUMBA** and in pursuance of such change of name as afore said I hereby declare that I will be known at all times hereafter in all actings and proceedings, in all dealing and transactions and upon all occasions whatover use and sign the name of **ERICK BUBERWA EMANUEL.** As my name in lieu of my former name of **ERICK BUBERWA IJUMBA.**

And I do hereby authorize and request all persons to designate, describe and address me by such assumed name of **ERICK BUBERWA EMANUEL** only.

**IN WITNESS WHERE OF I** have hereinto signed my name **ERICK BUBERWA EMANUEL** the assumed name this 30th day of October 2019.

**Sworn before me this 30th Day of October 2019**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

115493902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BERNADETA AGGREY MSONGOLE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye namba ya usajili **T976 DRS** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/420966/2019**

115492202

## KUPOTEA KWA VYETI



**CHRISTINA CHARLES MWAIJIBE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0330/0019 kilichotolewa na **MBEYA SEKONDARI** mwaka 2016. Result slip ya kidato cha sita index namba S0853/0515 iliyotolewa na **KIZWITE SEKONDARI** mwaka 2019 pamoja na cheti cha kuzaliwa.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MOR/MOR/RB/421152/2019.

115494302

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPH MARTIN SIZYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0303-0008** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Arusha Meru International. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **UD/RB/2144/2019**

115492302

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**NASSOR RASHID AHMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 986 DPL TRACTOR HEAD.** Chassis No. **LFWNHXPHXJAD34705.** Engine No. **1618H095573.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/RB/427232/2019.**

115495002

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**NASSOR RASHID AHMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 984 DPL TRACTOR HEAD.** Chassis No. **LFWNHXPH8JAD34704.** Engine No. **1618H095566.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/RB/427228/2019.**

115495002

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**NASSOR RASHID AHMED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 988 DPL TRACTOR HEAD.** Chassis No. **LFWNHXPHIJAD34706.** Engine No. **1618HO97144.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/RB/427221/2019.**

115495002

## ANATAFUTWA



**ANDREW C. SABAYA** anatafutwa na Polisi. Yeyote atakayemuona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0714 859191.** ***Taarifa ya polisi: TBT/RB/1035/2019.***

115492802

## KUPOTEA KWA CHETI



**DIANA LAIZER** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0679-0007** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2008 katika Shule ya Sekondari Kimandolu. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **IR/RB/6545/2017**

115492402

IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
FOR GEITA AT GEITA
APPLICANT NO. 37 OF 2019
LUGEGA FESTO PERTO…APPLICANT
VERSUS
MRASHI AUCTION MART & BROKERS
LTD……….RESPONDENT

**SUMMONS/NOTICE**

TO: MRASHI AUCTION MART & BROKERS LTD

**SUBSTITUTED SERVICE**

Take notice that the above matter is coming for mention/hearing on 6th November, day of 2019 before the Hon. A. M. KAPINGA Chairman of the tribunal. You are hereby commanded to appear at 3:00 am when the case will be mentioned heard.

GIVEN under my hand and the seal of this tribunal this 16th day of October.

154946

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VIJAY KUMAR SOMGAL** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA HILUX yenye namba ya usajili **T880 AKT** ilitotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcochcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MAG/RB/5042/2019**

115492502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HUMPHREY VENANCE TARIMO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA PRADO yenye namba ya usajili **T989 BAF** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcochcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MAG/RB/5043/2019**

115492602


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# PIQUE

## ATOA SIRI NEYMAR BARCA



**BARCELONA, Hispania**

BEKI wa Barcelona, Gerard Pique amebainisha kwamba timu ilitoa ofa ya kubadilisha mishahara yao ili kumrudisha Neymar kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Neymar alikuwa akitaka kurejea Barca wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita, ikiwa ni miaka miwili baada ya kusajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 222 kule Paris Saint-Germain.

Hata hivyo, dili hilo halikufanikiwa kwani PSG walikuwa wakitaka fedha nyingi ili kumuachia mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kurudi pale Camp Nou.

Pique amesema wachezaji wenzake walijaribu kusaidia uwezekano wa Neymar kurudi kwa miamba hao wa Catalunya akiiambia El Larguero: "Hatukuangalia fedha.

"Tulimwambia rais wetu kwamba tunaweza kubadilisha mikataba yetu kwa sababu tulijua kwamba, kuna sheria ya haki ya kifedha... hivyo tulimwambia rais kuliko kupata kitu fulani kwa mwaka mmoja ni afadhali tukapata kwa miaka miwili, mitatu au minne.

"Mwisho wa siku tulitaka kwenda sambamba na klabu na tulikuwa tayari kubadilisha mishahara yetu."

Alipoulizwa kama Neymar anaweza kurudi Barca, Pique aliongeza: "Katika soka chochote kinaweza kutokea."

## KLOPP ATISHIA KUJITOA CARABAO CUP

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpoool, Jurgen Klopp, ametishia kutopeleka timu uwanjani, endapo Chama cha Soka nchini England (FA), hakitabadilisha ratiba ya mchezo wa robo fainali ya Kombe la Ligi (Carabao Cup).

Klopp alitoa kitisho hicho, mara baada ya kikosi chake kuisasambua Arsenal kwa mikwaju ya penati 5-4, kwenye Uwanja wa Anfield usiku wa kuamkia jana, baada ya timu hizo kufungana mabao 5-5 katika muda wa dakika 90.

Mjerumani huyo amesema kuna haja ya FA kufikiria upya ratiba ya mchezo wa robo fainali, ambayo dhahiri itaingiliana na ratiba ya kikosi chake kwenda kushiriki michuano ya Klabu Bingwa ya Dunia hapo Desemba.

Ratiba ya mchezo wa robo fainali inaonyesha timu zilizofuzu hatua hiyo zitacheza kuanzia Desemba 17 na 18, mwaka huu huku Liverpool ikitarajia kuondoka juma hilo kuelekea kwenye michuano ya dunia.

"Hatuwezi kuwa waathirika wa tatizo hili," alisema Klopp.

"Kama watashindwa kupanga ratiba vizuri ya robo fainali ya Carabao Cup kwa ajili yetu, sitopeleka timu uwanjani, ni bora wakaangalia upya namna ya kumaliza hili tatizo."

"FIFA wameshatuambia ni lazima tuwe kwenye michuano ya klabu ndani ya muda maalum, huku FA wanaendelea kusisitiza ratiba ya ligi na michuano mingine ya ndani lazima ifuatwe."

"Kama itaendelea kuwa hivi, ni vigumu kwa timu moja kukabiliwa na ratiba zaidi ya moja tena ya michuano tofauti, FA wanapaswa kujipanga upya na kuangalia wanalimaza vipi hili tatizo.

"Lengo letu kubwa ni kushiriki michuano ya dunia na kutwaa ubingwa, hatutaki kuipoteza hiyo nafasi, naamini ratiba iliyopo ingekua na nafasi kubwa endapo wapinzani wetu (Arsenal) wangepita, lakini imekua tofauti," aliongeza meneja huyo Mjerumani.

Kikosi cha Liverpool kinatarajiwa kuondoka England Desemba 16 kuelekea Qatar kwa ajili ya michuano ya Klabu Bingwa ya Dunia, tarehe ambayo inaonyesha watapaswa kucheza mchezo wa robo fainali ya Kombe la Carabao.

## ADVOCAAT AMRITHI STAM FEYENOORD

**AMSTERDAM, Uholanzi**

ALIYEKUWA kocha wa Klabu za Rangers na Sunderland, Dick Advocaat ametangazwa kuwa mkuu wa benchi la ufundi la Feyenoord, hadi mwishoni mwa msimu huu.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 72, ametangazwa kushika nafasi hiyo, akirithi mikoba iliyoachwa na beki wa zamani wa Manchester United Jaap Stam, ambaye alichukua maamuzi ya kujiuzulu mwishoni mwa juma lililopita, kufuatia kikosi chake kufungwa mabao 8-0 dhidi ya Ajax Amsterdam.

Feyenoord wameshinda michezo mitatu kati ya 11 waliocheza msimu huu, na wanakamata nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Uholanzi.

Baada ya kutangazwa kuwa kocha wa klabu hiyo kongwe nchini Uholanzi, Advocaat alisema: "Nina uwezo wa kuisaidia klabu hii, nitahakikisha ninafanikisha hilo kwa moyo mkunjufu."

Naye mkurugenzi wa ufundi wa Feyenoord, Sjaak Troost alisema: "Tuna imani kubwa na Dick Advocaat , tutajitahidi kushirikiana naye kwa hali yoyote, ili kufikia mipango na malengo tuliyokusudia msimu huu, ninafarijika kuona amekubali kuwa nasi hadi mwishoni mwa msimu huu."

"Tunaamini uzoefu wake wa ukufunzi katika soka, utakisaidia kikosi chetu kurejea kwenye harakati za mapambano na kushinda michezo inayotukabili, baada ya kupoteza Jumapili dhidi ya Ajax Amsterdam."



## HABARI MICHEZO

# 'BAO LA RASHFORD KAMA LA RONALDO'




**LONDON, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema Marcus Rashford amefunga bao maridadi zaidi sawa na Ronaldo.

Mabao ya Rashford likiwamo la mkwaju wa mpira wa adhabu, yaliing'oa Chelsea katika mchezo wa Kombe la Ligi na Man United imefuzu robo fainali kwa ushindi wa mabao 2-1.

Mshambuliaji huyo alifunga bao la mpira wa adhabu ndogo lililofananishwa na yale anayofunga nyota wa Juventus 'Kibibi Kizee' cha Turin, Cristiano Ronaldo.

Mshambuliaji huyo wa England, alifunga bao hilo baada ya beki Marcos Alonso kumchezea madhambi Daniel James.

Michy Batshuayi aliyecheza kwa kiwango bora mechi saba za Chelsea, alifunga bao la kusawazisha akiwa ndani ya eneo la hatari.

"Ni kama vile Ronaldo. Amekuwa akifanyia kazi mipira ya adhabu. Ni bao maridadi,"alisema Solskjaer.

Kocha huyo alisema anaamini kinda huyo mwenye miaka 22, atakuwa katika ubora wake kwenye mechi zinazofuata baada ya kufunga mabao hayo mawili.

Kauli ya Solskjaer imekuja siku chache baada ya Rashford kukosa penalti katika mchezo wa Ligi Kuu England ambao Man United ilishinda mabao 3-1 dhidi ya Norwich City.

Chelsea ilifanya mabadiliko ya wachezaji sita waliocheza mechi ya Jumamosi dhidi ya Burnley. Christian Pulisic, aliyefunga mabao matatu kwenye Uwanja Turf Moor, jana hakucheza kwa kiwango bora.

Kocha wa Frank Lampard alisema kipindi cha kwanza hawakutengeneza nafasi nyingi kama ilivyokuwa kipindi cha pili ambapo walitumia nguvu kubwa.

Distributed via ippmedia

# Juve wamfungia kazi Mo Salah



**TURIN, Juventus**

KLABU ya Juventus ilituma skauti wake kwenda kule Anfield kwenye mechi ya Liverpool na Tottenham Hotspur zilizomenyana Ligi Kuu England kwa kazi moja tu, kumtazama Mohamed Salah.

Juventus wanaamini Mo Salah anaweza kuwa mtu sahihi kwa maana kwenda kurithi mikoba ya Ronaldo kwenye kikosi chao.

Ukimweka kando Mo Salah, hivi karibuni Juventus iliripotiwa kutenga fungu kubwa la pesa kwa ajili ya kumsajili Kylian Mbappe, lengo likiwa hilo hilo la kusajili mchezaji walau anayekaribiana kiasi fulani na Ronaldo.

Mabingwa hao wa Serie A wametenga kitita cha pauni milioni 335 kwa ajili ya kunasa mastaa hao, Mo Salah na Mbappe kwenye fowadi yao, pia wakiwafikiria wakali wengine, Son Heung-min, Toby Alderweireld na Christian Eriksen ili kuboresha kikosi chao na kukifanya kuwa na nguvu zaidi ya kufanya kweli kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ronaldo akiondoka Juventus, jambo hilo litazigusa timu nyingi kuhofia kupoteza mastaa wao, hasa PSG ambao Neymar na Mbappe wanaweza kuwekwa kwenye mpango wa kwenda kuziba pengo lake huko Turin, lakini kwa Ligi Kuu England, Mo Salah wa Liverpool na Harry Kane wa Tottenham Hotspur wanaweza kuhusishwa.

# Zidane: Benzema ndio kaanza mjue

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amesifia kiwango kilichoonyeshwa na Karim Benzema wakati timu hiyo ikiibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Leganes juzi, Jumatano.

Zidane amesema mambo mazuri zaidi bado yanakuja kutoka kwa Benzema.

"Karim mara zote huwa analeta tofauti," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni muhimu zaidi kwamba anafunga kwa sababu anahitaji kufanya hivyo kwa kuwa yeye ndiye namba tisa wa Madrid.

"Lakini ana mchango mkubwa zaidi kuliko mabao yake. Nina furaha na kiwango chake."

"Kwa uhakika kabisa, nasema Benzema yupo kwenye kiwango cha kuvutia zaidi kwa sasa na naamini ataendelea kuwa bora zaidi."

Benzema alifunga bao la nne kwenye mchezo huo kwa mkwaju wa penalti na hivyo kuifanya Real Madrid kupata pointi zote tatu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# EMERY SASA AVULIA KOFIA KIWANGO OZIL

●●●Alicheza vizuri dhidi ya Liverpool, tuna mechi tena Jumamosi na tutatazama uwezekano wa kumtumia...

**LIVERPOOL, England**

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Unai Emery amemsifu Mesut Ozil kwa kiwango chake bora wakati wakitolewa kwa penalti kwenye Kombe la Ligi ['EFL Cup'] dhidi ya Liverpool.

Mashabiki walipoozwa na wingi wa mabao katika Uwanja wa Anfield, ambapo Liverpool na Arsenal walitoka sare ya mabao 5-5 kabla ya wenyeji kutinga robo fainali kwa mikwaju ya penalti 5-4. Arsenal mara mbili ilikuwa mbele katika mechi hiyo ya Jumatano wakati kiungo asiyekubalika, Ozil akijumuishwa katika kikosi cha kwanza na kuonyesha soka la kvutia hapo Merseyside.

Soka la kuvutia kwa Ozil alionyesha wakati alipouwahi mpira uliokuwa unatoka na kummegea Ainsley Maitland-Niles ambaye aliiweka Arsenal mbele kwa mabao 4-2 kabla ya Liverpool kutokea nyuma na kusawazisha.

"Nadhani alicheza vizuri sana," Emery aliwaambia wanahabari. "Usiku wa leo, umeona alikuwa mchezaji mwenye akili sana katika timu na alikuwa chanya sana kila saa nadhani amecheza mchezo mzuri sana.

"Tulizungumza kabla ya mechi, na tulifanya uamuzi katika kipindi cha pili kumtoa nje kwa sababu hajacheza kwa kipindi kirefu kidogo na tunataka kumfanya kuendelea kuwa fiti kama alivyojaribu sana lakini kwake yeye ilikuwa ni vizuri kucheza dakika 60/65."

"Nadhani kwa kipindi hicho ni vizuri kufanya uamuzi huo kama ambavyo tulikuwa wapole na alifanya kazi vizuri sana na tuliamua ilikuwa vizuri kumpumzisha," aliongeza.

Alipoulizwa kama atajumuishwa tena kwa siku zijazo, Emery ambaye hana uhakika lini nahodha Granit Xhaka atarudi baada ya kukosekana kufuatia kutimuana na mashabiki, alijibu: "Ndiyo atajumuishwa. Tuna mechi Jumamosi na tutatazama uwezekano wa kumtumia tena pembeni ya wachezaji wengine na hii ndio njia wakati mwingine."

Katika mechi yenyewe, Emery alisema: "Ilikuwa mechi ya kijinga. Nadhani ilikuwa yakushangaza kwa mashabiki, kwetu sisi na kila mmoja. Kwa soka, nadhani kama shabiki nimeifurahia.

"Ulichezwa katika kipindi cha kwanza kwa hali ya juu. Kilikuwa kiwango kizuri sana kwa ujumla, tunaweza pia kuzungumza kuhusu mbinu za safu ya ulinzi bali kwa ushambuliaji, mabao matano. Lakini hatuwezi kuwa na furaha kwa asilimia 100 hata kama tungeshinda.

"Wakati mwingine nadhani katika mechi hizi, inaweza kusaidia mashabiki kuwa na furaha na nguvu, na moyo wa kujitoa kutoka kwa timu nzima. Tulikaribia sana kushinda na walisawazisha baadaye na penalti ni 50/50. Tulikatishwa tamaa mwishoni, kiulinzi kwa sababu tuliruhusu mabao matano, lakini kulikuwa na mengi chanya kwetu ya kutumia kwa baadaye."

## KWA UFUPI

**MOURINHO ATAKA KUREJEA EPL**
KOCHA wa zamani wa Manchester United na Chelsea, Jose Mourinho yupo tayari kurudi katika soka la England kwa sababu ya kutamani kushinda mataji makubwa akiwa na klabu ya tatu tofauti Ligi Kuu England. ***(Sky Sports)***

**ISCO LULU CITY, ARSENAL**
Manchester City na Arsenal wanatazama uwezekano wa kumsajili kiungo wa Real Madrid na Hispania Isco, 27. ***(Mundo Deportivo, via Manchester Evening News)***

**PEDRO WA WATFORD JANUARI**
MSHAMBULIAJI wa Brazil, Joao Pedro, 18, hatimaye amehakikishiwa kibali cha kufanya kazi na sasa atajiunga na Watford dirisha la Januari. Klabu hiyo imekubali ada ya pauni milioni mbili kwa Fluminense Oktoba 2018, lakini ilikuwa ikisubiri maombi yao ya kibali cha kazi kukubaliwa. ***(Standard)***

**TORRES AIVUTIA LIVERPOOL**
Liverpool, Borussia Dortmund na Barcelona zinavutiwa na winga wa Valencia, Mhispania Ferran Torres, 19. ***(Sport Bild, via Metro)***

**MOURINHO AITAKA ARSENAL**
JOSE Mourinho atavutiwa kuinoa Arsenal kama nafasi ya kufanya kazi hiyo itakuwapo. ***(ESPN)***

**SANCHO KUIGHARIMU CITY**
Manchester City inataka kumsajili kwa mara nyingine mshambuliaji wa England, Jadon Sancho kutoka Borussia Dortmund, lakini kinda huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye alitokea shule ya makinda ya City kabla ya kutua Ujerumani, anaweza kuwagharimu zaidi ya pauni milioni 100. ***(Sport Bild, via Sport Witness)***

**BAYERN YAMTAKA POCHETTINO**
Bayern Munich inamtazama kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino kama mbadala wa kocha Niko Kovac. ***(Sport1, via Sun)***

**PIQUE ATOA SIRI NEYMAR BARCA**
BEKI wa Barcelona, Gerard Pique, 32, amesema baadhi ya wachezaji wa klabu hiyo wamejitolea kubadilishiwa mishahara yao ili kutoa ofa ya kusaidia klabu hiyo kumsajili kwa mara ya pili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Brazil, Neymar, 27. ***(AS)***

**IBRAHIMOVIC, GALAXY KUKETI**
MENEJA Mkuu wa LA Galaxy, Dennis te Kloese anapanga kukutana na Zlatan Ibrahimovic, 38, kujadili mustakabali wa baadaye wa Msweden huyo akilenga kumbakisha klabuni hapo. ***(ESPN)***

**MILAN KUMRUDIA LOVREN**
AC Milan ipo tayari kujaribu tena kumsajili beki wa Liverpool na Croatia, Dejan Lovren, 30. ***(Tuttosport, via Mail)***

**MANDZUKIC BEI CHEE SOKONI**
Juventus ipo tayari kumuuza mshambuliaji Mcroatia Mario Mandzukic, 33, kwa Manchester United ama Sevilla katika dirisha la Januari, lakini inahitaji pauni milioni 4.6. ***(Calciomercato, via Mirror)***

**MADRID WAMKUBALI BALE**
MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale, 30, amerejesha sapoti yake kutoka kwa wachezaji wenza wa Real Madrid. ***(Marca)***

**WOLVES, WATFORD KWA BUTA**
Wolves na Watford zinajiandaa kwenda kumsajili beki wa kulia wa Royal Antwerp, Mreno Aurelio Buta, 22, kwa pauni milioni tano katika dirisha la Januari. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# TFF SASA KUANDAA MAKOCHA WANAWAKE

Na Shufaa Lyimo

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), limesema lipo kwenye mchakato wa kuandaa kozi nyingi za makocha na waamuzi kwa wanawake lengo likiwa ni kuinua soka la wanawake nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Athumani Nyamlani, wakati akifunga semina ya siku mbili kwa waandishi wa habari za michezo wanawake iliyofanyika katika Hoteli ya Serene jijini Dar es Salaam.

Nyamlani alisema TFF kwa sasa imefika mbali na kwamba kutokana na mafanikio wanayoyapata wanauhakika watapata wadhamini wengi ambao watasaidia kupeleka mbele soka la nchi hii.

"Tunawategemea sana kwa weledi wenu katika kazi hii hususan kwa kutoandika mambo chanya, vilevile tunaamini mtaisapoti vizuri timu ya wanawake," alisema Nyamlani.

Kwa upande wa msemaji wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema wanatarajia kufanya chaguzi mbalimbali za viongozi ambapo miongoni mwao anaamini watatoka kwa waandishi hao.

"Katika chaguzi zetu ambazo tunatarajia kuzifanya naamini tutapata viongozi kutoka miongoni mwenu," alisema Ndimbo.

# NDAYIRAGIJE ATAJA MFUMO WAKE ATAKAOTUMIA STARS

Na Focus Nicus

WAKATI mashabiki, wadau wa soka na Watanzania kwa ujumla wakitaka kujua falsafa ya soka la Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mrundi Etienne Ndayiragije, hatimaye amefunguka kuwa yeye ni muumini wa soka la kumiliki zaidi huku akitaja namna litakavyokinufaisha kikosi chake hicho.

Ndayiragije ambaye alikuwa akikaimu nafasi ya Kocha Mkuu wa Stars, wiki moja iliyopita Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilimuidhinisha rasmi kukalia kiti hicho akirithi mikoba ya Mnigeria Emmanuel Amunike aliyetimuliwa kutokana na kuvurunda kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) iliyofanyika Misri Juni mwaka huu.

Akizungumza kupitia kituo kimoja cha redio jijini Dar es Salaam jana, alipoulizwa kama yeye ni muumini wa soka la Jose Muorinho [anayependa kupaki na kushambulia kwa kushtukiza] ama falsafa zake ni kama za Pep Guardiola [pasi nyingi na kumiliki mpira], Ndayiragije alisema yeye atabaki kuwa Ndayiragije na hawezi kubadilika.

"Nitabaki kuwa Ndayiragije, ila kuhusu mfumo mimi napenda soka la kumiliki, unajua unapomiliki mpira unaweza kucheza kwa kushambulia kwa nafasi na kuzuia, lakini aina hii ya soka ni nzuri kwa wachezaji wetu ambao hawana maumbo makubwa," alisema.

Alisema aina ya wachezaji wa Kitanzania ambao anaamini ni kati ya wenye vipaji vya hali ya juu ukilinganisha na nchi tisa tofauti alizowahi kufundisha soka, wakicheza soka la kumiliki ni nzuri zaidi kwao kuweza kupata matokeo.

Kuhusu mkataba wake wa mwaka mmoja kuweza kutimiza malengo yake, alikiri ni kweli mkataba huo ni wa muda mfupi sana, lakini amejipanga vizuri kuweza kuiandaa Stars vema pamoja na kuwa na programu nzuri ili kama akiondoka kocha ajae aweze kuendeleza atakapoishia.

Alisema kinachotakiwa ni kila mmoja kutimiza majukumu yake ipasavyo kuanzia TFF, mashabiki na hata waandishi wa habari kulisaidia benchi la ufundi katika kufanya uchambuzi kwa timu ambazo Taifa Stars itakuwa ikielekea kucheza nazo, lakini pia kuchambua kwa kina kuhusu viwango vya wachezaji wa Tanzania waliopo ndani na nje ya nchi ili aweze kuwamulika katika kikosi chake.

"Waandishi wa habari hamtakiwi kuwa wahamasishaji tu, bali kazi yenu kubwa iwe kufanya uchambuzi wa kina kuhusu timu ambazo Stars itakuwa ikielekea kucheza nazo katika mashindano mbalimbali pamoja na wachezaji wetu waliopo ndani na nje ya nchi.

"Mkifanya hivyo mtakuwa mkilisaidia sana benchi la ufundi wakati huo pia TFF nayo ikitekeleza majukumu yake," alisema.

Distributed via ...

SAMAGOAL...



Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta (chini) akishangilia pamoja na wenzake baada ya kuifungia timu yao ya KRC Genk bao la kwanza wakati ikitoka nyuma kwa mabao 2-0 na kupata sare ya 2-2 dhidi ya wageni wao, Royal Antwerp FC katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza A Ubelgiji iliyopigwa Uwanja wa Luminus Arena mjini Genk juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Mlandege wataka tatu za Mafunzo

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Mlandege inayoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar, Sheha Khamis, amesema matumaini yake ni kuona timu hiyo inatoka na alama tatu katika mchezo wake wa mzunguko wa nane watakaposhuka Dimba la Amaan kesho kumenyana na Maafande wa timu ya Mafunzo.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo ambaye msimu uliopita alikuwa akikinoa kikosi cha KVZ, alisema ana matumaini ya kupata ushindi katika mchezo huo kutokana na tayari ameshafanyia kazi mapungufu yaliyopo kikosini mwake.

Alisema washambuliaji wake walikuwa na mapungufu ya kutokuwa na umakini wa kupachika mabao na hata kupiga mipira ya adhabu huku wakipoteza pasi nyingi.

Khamis alisema ilimpa muda kuizoe timu yake hiyo mpya kwa kuwa wachezaji walipaswa kuzoea aina ya mazoezi ya kocha huyo hali iliyopelekea kutopata matokeo mazuri katika michezo ya mwanzoni mwa ligi.

Alisema kuwa kuhusu mchezo wa mzunguko wa nane dhidi yao na Mafunzo, alisema anakifahamu vema kikosi cha wapinzani wake na asilimia kubwa ya wachezaji wa mafunzo wanauzoefu wa kucheza Ligi Kuu Zanzibar, hivyo atatumia mbinu mpya ili aweze kutoka na ushindi.

Timu ya Mlandege ambayo ipo nafasi ya nne ikiwa na alama 12 katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar kutokana na kushuka dimbani mara saba wakiwa wameshinda michezo mitatu, sare tatu huku mchezo mmoja wakifungwa.

# Kaseja ataka mashabiki KMC kutoinamisha vichwa chini

Na Focus Nicus

BAADA ya kukubali kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, nahodha wa KMC FC, Juma Kaseja amewataka mashabiki wao kutoinamisha vichwa chini na badala yake waendelea kuwaunga mkono kwa kuwa muda si mrefu timu hiyo itainuka na kuanza kushinda.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani juzi, bao pekee la wenyeji hao lilipachikwa nyavuni na Santos Mazengo dakika ya 17, hivyo kuifanya KMC kupoteza mechi yake ya tatu msimu huu baada ya kushuka dimbani mara sita na kushinda mchezo mmoja huku ikitoka sare mbili.

Hata hivyo, licha ya matokeo hayo mabaya kwa KMC ambayo msimu uliopita ilimaliza nafasi ya nne nyuma ya mabingwa Simba wakifuatiwa na Yanga na Azam iliyomaliza ya tatu, Kaseja amesema ana matumaini kikosi chao kitaamka na kuanza kushinda kwa kuwa kinaonyesha soka la kuvutia ila bahati tu ndiyo inayowagharimu.


"Timu inatengeneza nafasi na inacheza vizuri, hakuna sababu ya mashabiki kuinamisha vichwa chini, waendelee kutuunga mkono kwa sababu tunauhakika tutaamka kutoka huku tulipo kwa timu kuanza kushinda," Kaseja alisema.

"Mechi bado ni nyingi na huu ndiyo kwanza kama msimu umeanza, hivyo mashabiki waendelee kutuunga mkono, kilichotokea tumefanya makosa na kuadhibiwa ila ninaamini timu itafanya vizuri," alisema kipa huyo wa zamani wa Simba na Yanga.

Kaseja ambaye ameiwezesha Taifa Stars kucheza hatua ya makundi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022 pamoja na kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) nchini Cameroon hapo mwakani, amekuwa katika kiwango cha juu tangu msimu uliomalizika.

Aidha, KMC inayoshika nafasi ya tatu kutoka mkiani ikiwa na alama tano, itashuka Dimba la Uhuru Jumatatu ijayo kuikabirisha Biashara United ya Musoma iliyopo nafasi ya 14 ikiwa na pointi nane baada ya kushuka dimbani mara nane.

Michezo
Ijumaa Novemba 1, 2019
Nipashe



Emery sasa avulia kofia kiwango Ozil

HABARI UK 30

TUTA NYAVUNI...



Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo akipiga mkwaju wa penalti kabla ya kuuzamisha kimyani baada ya kuchezewa madhambi ndani ya boksi na straika wa Genoa, Antonio Sanabria kwenye mechi Serie A iliyopigwa Turin na Juve kushinda 2-1 juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

Distributed via ippmedia

# SABABU MWADUI KUITOBOA SIMBA

●●● Dilunga atajwa kuwabeba wachimba madini hao, huku wakieleza mkakati alioundiwa Mzamiru kuhakikisha...

**Na Somoe Ng'itu, SHINYANGA**

HUKU Simba ikiendelea kuugulia maumivu ya 'kutobolewa' (kufungwa) mechi yao ya kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu, Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, amesema kitu kilichoifanya timu yake ipate pointi tatu katika mechi hiyo ni namna walivyofanikiwa kuidhibiti idara ya kiungo ya mabingwa hao watetezi.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa CCM Kambarage juzi, Mwadui FC ilipata ushindi wa bao 1-0, kupitia kwa mshambuliaji wake, Gerald Mathias na kuondoka na pointi tatu zilizowafanya wafikishe idadi ya pointi 11 na kupanda hadi nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 20 nchini.

Mechi hiyo ilikuwa ya kwanza kwa Simba kupoteza, tangu msimu wa 2019/20 ulipoanza hapo Agosti 23, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Khalid, alisema ushindi wa mechi hiyo ulianza mapema baada ya kuona kikosi cha Simba kilichotangazwa kuanza katika mchezo huo kwa kutoliona jina la kiungo, Hassan Dilunga.

Khalidi alisema kuwa baada ya kuona "kikosi" hicho, aliwaambia wachezaji wake wanatakiwa kuhakikisha wanambana na kumdhibiti kiungo Mzamiru Yassin na watakapofanikiwa, watakuwa wamefaulu mchezo huo.

"Niliwaambia kwa kikosi hiki kilichopangwa, hapa anayepaswa kudhibitiwa ni Mzamiru, hii ndio "switch" ya Simba leo (juzi), kama mtafanikiwa kuizima, naamini ile furaha tuliyokuwa tunaitarajia, tutaipata, na walifanikiwa kufanya hivyo," alisema Khalidi, ambaye kutimuliwa na kurejeshwa katika kikosi hicho ni jambo la kawaida kwake.

Kocha huyo aliongeza kuwa, aliwaandaa wachezaji wake kutokuwa na woga, na kucheza kwa kujiamini na kwa kufanya hivyo, asilimia zisizopungua 70, walifanikiwa na kuwa klabu ya kwanza kuondoka na pointi msimu huu kutoka kwa mabingwa hao watetezi wa ligi hiyo.

"Pia niliwaambia Simba ni timu kubwa, ina wachezaji wazoefu, lazima tuipe heshima yake, nashukuru makosa yalikuwa machache, sisi kwanza tulikuwa bora sana, ila nashukuru tumepata kile tulichokitarajia, halafu sikutaka kuwabana sana wachezaji, hata baada ya kumaliza mazoezi jana (juzi), tuliwaacha huru," Khalid aliongeza.

Naye beki tegemeo wa timu hiyo, Joram Mgeveke, alisema walikuwa makini na walikumbushana kufuata maelekezo ya kocha wao kila mara ili kuhakikisha wanapata ushindi.

"Siri ya ushindi ni kujituma kwetu, tulifuata maelekezo kwa kiasi kikubwa, hatukuwa na presha, tulijiandaa kupata matokeo mazuri, hata sare kwetu ilikuwa inatutosha, lakini tulisema ushindi pia unawezekana, tukaongeza juhudi na hatimaye tukafanikiwa," alisema Mgeveke.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema wanashukuru Mungu wamemaliza mchezo salama na matokeo waliyopata yalitokana na kutocheza vizuri kama walivyokuwa wachezaji wa Mwadui FC.

"Mpira ndivyo ulivyo, tulitafuta nafasi tukashindwa kuzitimua, wenzetu wametafuta na kuitumia, unaweza ukashambulia na unaweza pia kushambuliwa, kuna mazuri tulifanya na makosa pia, mwalimu ameyaona, atayarekebisha kwa ajili ya mchezo unaofuata," alisema

Rweyemamu alisema kuwa, mchezo huo umemalizika, sasa wanarejea jijini Dar es Salaam ili kujiandaa kuwakaribisha Mbeya City kwa ajili ya mchezo mwingine wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumapili wiki hii kwenye Uwanja wa Uhuru.

## Zahera: Pakuishika Pyramids ni hapa

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI ratiba ya Yanga kuelekea Misri ikibadilika na kuondoka jana jioni badala ya alfajiri, kikosi hicho kimeondoka na matarajio makubwa ya ushindi baada ya Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera kueleza tayari amebaini udhaifu wa wapinzani wao Pyramids FC ulipo.

Yanga itarudiana na Pyramids Jumapili kusaka tiketi ya kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya mechi ya awali mwishoni mwa wiki iliyopita kukubali kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Waarabu hao kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Hata hivyo, licha ya mchezo wa awali Yanga kuzidiwa, Zahera amesema tayari amebaini udhaifu na mbinu za Waarabu hao, hivyo kama wachezaji wake wakifuata vema maelekezo aliyowapa ana uhakika wa kupata matokeo katika mchezo huo ambao wanahitaji ushindi kuanzia mabao 2-0 ili kufuzu hatua ya makundi.

"Moja ya mbinu zao ni kwamba wanacheza kwa kasi sana dakika 20 za mwanzo na baada ya hapo wanapunguza kasi kutokana na kuchoka, hivyo nimewaeleza wachezaji wangu kuwa makini katika dakika hizo.

"Kama tutaweza kuwadhibiti na kisha dakika za mwisho kuongeza umakini tunaweza kupata matokeo mazuri," alisema Zahera.

Alisema wamejiandaa vizuri na kinachotakiwa ni wachezaji kuzingatia maelekezo yake ili kuweza kushinda mchezo huo.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kikosi hicho kilichoondoka na ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia, kinajumuisha msafara wa watu 26 badala ya 27 kama walivyotangaza awali kutokana na kocha wa makipa kubaki kwa ajili ya kuhudhuria kozi.

"Msafara unajumuisha wachezaji 20, na tayari Makamu Mwenyekiti wetu, Frederick Mwakalebela ambaye alitangulia huko kuandaa mazingira ya sehemu timu itakaposhukia, amesema kila kitu kinakwenda vizuri na mipango yote kwa ajili ya mapokezi ya timu yamekamilika," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >